**24 MEI, 2023**

# BUNGE LA TANZANIA

---

## MAJADILIANO YA BUNGE

---

## MKUTANO WA KUMI NA MOJA

**Kikao cha Thelathini na Mbili – Tarehe 24 Mei, 2023**

*(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Spika (Mhe. Dkt. Tulia Ackson) Alisoma Dua*

**SPIKA:** Waheshimiwa, tukae.

Katibu.

**NDG. RUTH MAKUNGU – KATIBU MEZANI:**

**HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI**

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na: -

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:**

Randama za Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024.

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:**

Hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kwa mwaka wa fedha 2023/2024.

**MHE. FELISTA D. NJAU K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA MAMBO YA NJE, ULINZI NA USALAMA:**

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama kuhusu Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kwa mwaka wa fedha 2022/2023 pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa mwaka wa fedha 2023/2024.

**SPIKA:** Ahsante sana. Katibu.

**NDG. RUTH MAKUNGU – KATIBU MEZANI:**

## MASWALI NA MAJIBU

**SPIKA:** Maswali. Waheshimiwa Wabunge, tutaanza na Ofisi ya Waziri Mkuu; Mheshimiwa Hawa Mchafu Chakoma, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 415

### Mchakato wa Pensheni kwa Wazee Wote

**MHE. HAWA M. CHAKOMA** aliuliza: -

Je, Serikali imefikia wapi kuhusu mchakato wa pensheni kwa wazee wote?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu, Mheshimiwa Patrobass Katambi, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU (MHE. PASCHAL P. KATAMBI)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Hawa Mchafu Chakoma, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, pensheni kwa wazee wote inajumuisha wazee ambao walikuwa katika ajira ambao kwa sasa wanalipwa pensheni na Mifuko waliyochangia wakati wanafanya kazi na pili, wazee ambao hawajawahi kuajiriwa kwa sasa hawalipwi.

Mheshimiwa Spika, mchakato wa kuwalipa pensheni wazee wote ambapo utajumuisha wazee ambao hawajawahi kuajiriwa ni utaratibu mpya ambao utahitaji kugharamiwa na bajeti ya Serikali. Hivyo, itahitaji kufanyika utafiti wa kina ili kuona uwezo wa Serikali katika kulipa pensheni kwa wazee wote. Hata hivyo, kwa sasa Serikali imekuwa inahudumia wazee kutoka katika familia au kaya zenye umaskini uliokithiri kupitia Mradi wa *TASAF* ambapo wazee ni sehemu ya familia hizo, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Hawa Mchafu Chakoma, swali la nyongeza.

**MHE. HAWA M. CHAKOMA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuuliza maswali mawili madogo ya nyongeza. Swali la kwanza; kwa mujibu wa sensa, wazee wako asilimia 5.7 tu, idadi hii ni ndogo sana ikilinganishwa na umuhimu na mchango mkubwa wa wazee hawa katika Taifa hili. Je, Serikali haioni haja na umuhimu wa kutenga chanzo kimoja mahususi kwa ajili ya pensheni ya wazee hawa?

Mheshimiwa Spika, swali langu la pili; Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ni pamoja na upande wa Zanzibar. Kwa kuwa wazee wa upande wa Zanzibar wanapatiwa pensheni kwa wazee wote, ni kwa nini Serikali inachukua muda mrefu wa kufanya utafiti tusijifunze kwa wenzetu wa Zanzibar, japo kuanza na wazee wa umri wa miaka 70 ambao kwa mujibu wa sensa wako asilimia 2.7 tu? Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU (MHE. PASCHAL P. KATAMBI):** Mheshimiwa Spika,

ahsante. Naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Hawa Mchafu Chakoma, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, wazee kwa mujibu wa sensa ni kweli ni asilimia 5.7, lakini katika kuangalia umuhimu huo wa wazee na ndiyo maana nikasema kwenye jibu la msingi kwamba Serikali itaendelea kufanya utafiti na kuangalia *best practice* ya uwezekano pia wa Serikali wenyewe kuangalia katika masuala ya kibajeti kama inaweza kuhudumia kundi hili.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, tayari hata ukiangalia kwenye swali lake la pili ambalo linaelezea kufananisha ulinganifu wa upande wa Tanzania Zanzibar, kwamba wazee wamekwishaanza kulipwa, vivyo hivyo, ni mambo yote haya ya kifedha ambayo katika kuangalia lazima tuone namna ambayo tunaweza tukapata fedha za uhakika kuwalipa wazee hawa.

Mheshimiwa Spika, wazee waliokuwa wanafanya kazi wamejumuishwa kwenye Mifuko ya Hifadhi ya Jamii na katika Mifuko hiyo kuna skimu maalum ambayo inaruhusu sasa mtu yeyote, hata akiwa hajaajiriwa, kutoa michango yake katika mifuko hiyo na baadaye kuja kupata pensheni yake.

Mheshimiwa Spika, la mwisho, niseme tu kwamba katika utafiti ambao tunaufanya kwa kipindi hiki, haitachukua muda ili kuweza kuliangalia ikiwa ni zingatio, kama jinsi ambavyo Serikali inatambua mchango wa wazee hawa, umuhimu wao, lakini pia kama chemchemi ya busara na waliochangia kwa sehemu kubwa uchumi wa Taifa. Kwa hiyo tumewaangalia pia na tumeendelea kuweka utaratibu kama huu wa *TASAF* wa kuwapa fedha ambapo kaya maskini wanasaidiwa wazee hawa, lakini pia kuna taratibu za utoaji wa mikopo ambazo nazo pia zinaendelea.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo wakati haya mambo yanaendelea sambamba na hilo, ni pamoja pia na kujiridhisha sasa kwenye masuala ya kibajeti kama tutaona umuhimu. Tutalileta

kwenye Bunge lako Tukufu kwa ajili ya kupata ushauri, maoni na mapendekezo ya wadau, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Ester Bulaya, swali la nyongeza.

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Mheshimiwa Naibu Waziri, kumekuwa na malalamiko kwa baadhi ya wazee katika maeneo mbalimbali wakiwemo wa Mkoa wa Mara, kwamba hawapati ile pensheni yao kwa wakati. Je, ni nini mkakati wa Serikali kuhakikisha wazee hawa ambao wamelitumikia Taifa wanapata pesa yao kwa wakati?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU (MHE. PASCHAL P. KATAMBI):** Mheshimiwa Spika, ahsante. Naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Ester Amos Bulaya, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, niombe tu kwa sababu hilo ni suala mahususi kabisa la Mkoa wa Mara, niwasiliane na Mheshimiwa Mbunge niweze kupata taarifa za kwa nini ucheleweshwaji unafanyika kwa sababu ni jambo ambalo kwa sasa tunalipa kimtandao na taarifa zinapatikana kwa wakati na tumekuwa tukilipa kwa wakati kabisa katika kipindi hicho. Kwa hiyo jambo hili litakuwa mahususi, nimwombe Mheshimiwa Ester Bulaya anipatie taarifa hizo niweze kufanya ufuatiliaji mara tu baada ya Bunge hili, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Boniphace Mwita Getere, swali la nyongeza.

**MHE. BONIPHACE M. GETERE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Hili suala la upande wa Zanzibar kupata pensheni ya wazee wote na Tanzania Bara kukosa wakati ni nchi moja, naomba kujua, nini tamko la Serikali kuhusu wazee wa Bara ambao wanatakiwa kupata pensheni sawa na wazee wa Zanzibar?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU (MHE. PASCHAL P. KATAMBI):** Mheshimiwa Spika, ahsante. Naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Boniphace Mwita Getere, Mbunge wa Bunda, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kama nilivyojibu kwenye swali la msingi kwamba kwenye masuala ya kipensheni tayari tunayo Mifuko ya Hifadhi ya Jamii, kwa hiyo mtu yeyote kwa sasa, hata kabla ya uzee, unaweza ukaanza kupeleka fedha.

Mheshimiwa Spika, katika upande wa pili, kuhusiana na kwamba tutoe tamko; ni hilo la kufanya utafiti ili kuweza kujiridhisha uwezo wa Serikali katika kuhudumia wazee hawa.

Mheshimiwa Spika, tatu, suala hili tayari wazee wanahudumiwa kwa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kwa sasa tunavyo vituo 14 vya wazee wasiojiweza ambavyo ni vya Serikali, vinahudumia hawa wazee na vituo 15 vya watu binafsi na jumla ya wazee 496 wanapata huduma kwenye hayo maeneo.

Mheshimiwa Spika, sambamba na hilo, Serikali ya Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan, iliweka mpango wa *TASAF* ambao unanufaisha wazee. Serikali ya Dkt. Samia Suluhu Hassan imeona bado pia kuna umuhimu wa kuwahudumia wazee, imeweka utaratibu wa mikopo, utoaji wa fursa na mitaji; Serikali hii hii imeweza kuendelea kuwaangalia wazee kwa kuwatolea huduma ya matibabu bure na kuna *desks* zaidi ya 588 kwenye hospitali zetu kwa ajili ya kuwahudumia.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo hili suala Serikali inaliangalia kwa kina sana kuona namna gani wazee wetu tunawaenzi na kuwaheshimu katika mchango mkubwa walioutoa wakati wa ujana wao kuchangia uchumi wa Taifa. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Asha Abdullah Juma, swali la nyongeza.

**MHE. ASHA ABDULLAH JUMA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Wazee wengi ambao walikuwa wafanyakazi wa Shirika la Posta na Simu na *ATCL* na Mashirika mengine kama Reli, mpaka sasa hivi wanahangaika kupata vipensheni vyao. Je, ni lini Serikali itamalizana na wazee hawa ili wakifa wakapumzike kwa amani?

**SPIKA:** Hapo kwenye kifo kidogo naona mtihani, kama vile wazee wanapangiwa kufa.

Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU (MHE. PASCHAL P. KATAMBI):** Mheshimiwa Spika, ahsante. Naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Asha Abdullah Juma, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kifo ni mpango wa Mungu lakini hatuombei itokee hivyo kwa wazee wetu, waishi na waendelee kudumu.

Mheshimiwa Spika, kwenye swali hilo la Mheshimiwa Asha kuhusiana na wazee hawa waliokuwa watumishi wa Shirika la Posta pamoja na Reli kupata pensheni zao; itakumbukwa vizuri kwamba tayari kulikuwa na mashauri mbalimbali ya wazee ambao walikuwa wanafanya kazi kwenye mashirika hayo. Wapo tayari ambao wamekwishalipwa pensheni zao lakini pia wapo ambao wameendelea kuwa na madai. Hii imetokana zaidi na kutokuwepo kwa taarifa sahihi za madai yale lakini Serikali imeendelea kufanya ufuatiliaji.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo nimwombe pia Mheshimiwa Mbunge, mama yangu Asha, baada ya hapa pia nipate taarifa ya madai hayo, kama kuna watu *specific* au mahususi tuweze kwenda kufanya ufuatiliaji kwamba wamekwama wapi katika kulipwa kama walikuwa kweli wafanyakazi halali, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Mheshimiwa Jacqueline Ngonyani Msongozi, Mbunge wa Viti Maalum, swali lake litaulizwa kwa niaba yake na Mheshimiwa Abdallah Dadi Chikota.

Na. 416

**Ujenzi wa Barabara ya Majengo – Ruvuma – Subira hadi Muungano – Songea**

**MHE. ABDALLAH D. CHIKOTA K.n.y. MHE. JACQUELINE N. MSONGOZI** aliuliza: -

Je, lini Barabara ya Majengo – Ruvuma – Subira - Muungano itajengwa kwa kiwango cha lami?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Mheshimiwa Deo Ndejembi, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Jacqueline Ngonyani Msongozi, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali imeshaanza mipango ya ujenzi wa Barabara ya Majengo – Ruvuma - Subira na Muungano kwa kiwango cha lami ambapo katika Mwaka wa Fedha wa 2023/2024, jumla ya shilingi milioni 517.50 zimetengwa kwa ajili ya ujenzi wa barabara hii kwa kiwango cha lami nyepesi kilomita moja.

Mheshimiwa Spika, Serikali itaendelea kutenga fedha kwa ajili ya ujenzi wa barabara hiyo kwa kiwango cha lami kulingana na upatikanaji wa fedha.

**SPIKA:** Mheshimiwa Abdallah Dadi Chikota, swali la nyongeza.

**MHE. ABDALLAH D. CHIKOTA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Pamoja na majibu mazuri yenye matumaini ya Serikali, eneo husika lina umbali wa takribani kilometa 10. Je, Serikali inatoa *commitment* gani ya kumaliza kilometa tisa zilizobaki?

Mheshimiwa Spika, swali langu la pili; Halmashauri ya Mji wa Nanyamba imeazimiwa kujengwa kilometa 20 kwa lami kwa mpango wa *TACTIC*. Je, lini ujenzi huo utaanza?

Mheshimiwa Spika, nakushukuru.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI):** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Abdallah Dadi Chikota, Mbunge wa Nanyamba, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, la kwanza, hii *commitment* ya fedha kwa barabara kilometa zilizosalia. Kwanza, barabara hii ina jumla ya kilometa 9.5 na tayari katika Mwaka wa Fedha 2021/2022, Serikali ilitenga shilingi milioni 270 kwa ajili ya ujenzi wa madaraja mawili, vilevile kuhakikisha kwamba mifereji ya maji kilometa mbili inajengwa.

Mheshimiwa Spika, hivi sasa kama nilivyokwishasema kwenye majibu yangu ya msingi, kwamba Serikali imetenga hiyo kilometa moja kwa shilingi milioni 517, tutaendelea kutenga fedha kwa ajili ya ujenzi wa barabara hii kwa kadri ya upatikanaji wa fedha.

Mheshimiwa Spika, tayari Mheshimiwa Mbunge mwenyewe, Mheshimiwa Msongozi, lakini vilevile Mheshimiwa Dkt. Ndumbaro, Mbunge wa Jimbo pale naye amekuwa akiifuatilia sana barabara hii; Mheshimiwa Nyoka, Mheshimiwa Judith Kapinga, wote walikuwa

wakifuatilia sana barabara hii na tutaendelea kuitafutia fedha kama Serikali ili kuweza kuhakikisha kilometa zote 9.5 zinakwisha.

Mheshimiwa Spika, nikienda kwenye swali la pili la kilometa 20 za Nanyamba kule Mkoani Mtwara. Mradi huu wa *TACTIC* hivi sasa upo katika kupata wale wakandarasi ambao watajenga barabara za *TACTIC* hapa nchini. Tayari timu zile za *evaluation* zilishakaa kule Jijini Arusha kuhakikisha kwamba tunapata wakandarasi wenye uwezo wa kukamilisha mradi huu. Nimtoe mashaka Mheshimiwa Chikota kwamba muda si mrefu mradi huu utaanza.

**SPIKA:** Mheshimiwa Amsabi Mrimi, swali la nyongeza.

**MHE. JEREMIAH M. AMSABI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Tunaishukuru Serikali kwa kuanza ujenzi wa kilometa 600 za lami kutoka Benki ya *CRDB* pale Mjini Mugumu kuelekea Hospitali ya Wilaya. Pamoja na ujezni huu barabara hii imesimama sasa kwa muda, na kwa vile inaelekea hospitali ya wilaya, imekuwa na usumbufu mkubwa sana kwa wananchi. Pamoja na jitihada nyingi za mawasiliano na *TARURA,* wilaya na mkoa bado ujenzi huu hauendelei. Je, ni lini changamoto hizi zitatatuliwa na ujenzi ule ukamilike? Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI):** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Jeremiah Mrimi Amsabi, Mbunge wa Serengeti, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, barabara hii anayozungumzia Mheshimiwa Mrimi ya *CRDB* – Hospitali katika Mji wa Mugumu imekuwa na changamoto ya mkandarasi mwenyewe kuwa anafanya kazi kwa taratibu sana. Mkandarasi huyu ameshaitwa kwenye Kamati mbalimbali za pale katika Wilaya ya Serengeti kuangalia ni namna gani anaweza akamaliza barabara hii.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge tukitoka hapa tutakaa naye tuweze kuona tunaweka mkakati gani na Meneja wa *TARURA* wa Mkoa wa Mara na Meneja wa *TARURA* wa Wilaya ya Serengeti kuona mkandarasi huyu anarudi *site* vipi kwa haraka sana kumalizia barabara hii.

**SPIKA:** Mheshimiwa Saashisha Mafuwe, swali la nyongeza.

**MHE. SAASHISHA E. MAFUWE:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Ni lini Serikali itajenga barabara ya Mijengweni – Shiri Njoro, kilometa 15 tu? Barabara hii ni muhimu sana kwa kusafirisha mazao ya wananchi, lakini wananchi kuja kupata huduma huku Bomang'ombe.

Mheshimiwa Spika, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI):** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Saashisha Elinikyo Mafuwe, Mbunge wa Hai, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, barabara hii ya Mijengweni itajengwa kwa kadri ya upatikanaji wa fedha, lakini Mheshimiwa Mbunge ni shahidi kwa jitihada za Serikali ambazo zimefanyika katika Wilaya ya Hai, tayari kupitia *TARURA* tumejenga Barabara ya Nyerere yenye mita 600; tumejenga Barabara ya Stendi – *TTCL* kwenda *RC Church;* tumejenga Barabara ya Bomang'ombe pale na tunaendelea. Kuna barabara nne kwa jitihada zake ambazo zinaendelea kujengwa na tutatafuta fedha kwa ajili ya kujenga hizi kilometa 15 kama ambavyo Mheshimiwa Mbunge ameomba.

**SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Charles Kimei, swali la nyongeza.

**MHE. DKT. CHARLES S. KIMEI:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Swali langu ni hili hili nalirudia kila wakati. Ile *bypass road* kutoka

Chekereni kwenda Kahe – Mabogini na *TPC* wataifanya nini au wana mkakati gani kwa sababu hii iko kwenye Ilani na ahadi za viongozi wetu wakubwa? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI):** Mheshimiwa Spika *bypass road* hii Serikali inaifanyia kazi kupitia Wakala wa Tanzania ambao ni *TANROADS* na tutakaa pamoja na wenzetu wa *TANROAD* kuona mipango yao ni ipi kuhakikisha barabara hii inatekelezwa kama Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ambavyo ilielekeza.

**SPIKA:** Mheshimiwa Ghati Zephania Chomete, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 417

**Ujenzi wa miundombinu ya maji mashuleni**

**MHE. GHATI Z. CHOMETE** aliuliza: -

Je, Serikali ina mpango gani wa kujenga miundombinu ya maji mashuleni ili kuepusha milipuko ya magonjwa?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI)** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI), naomba kujibu swali la Mheshimiwa Ghati Zephania Chomete, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea kuhakikisha kuwa shule zote za Msingi na Sekondari zinakuwa na miundombinu ya maji safi na salama pamoja na vifaa vya kunawia mikono vikiwemo ndoo, jaba tiririka na miundombinu iliyojengwa kwa pamoja *(mass*

*handwashing facilities)*. Aidha, katika mwaka wa fedha wa 2022/2023 Serikali kupitia mradi wa usafi na mazingira *(SRWSS)* imejenga miundombinu bora ya kunawia mikono pamoja na vifaa vya kuhifadhia maji katika shule za msingi 1853.

Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea kuhamasisha usafi mashuleni kupitia vilabu vya uhamasishaji usafi mashuleni *(Swash Clubs)*.

**SPIKA:**Mheshimiwa Ghati Chomete swali la nyongeza.

**MHE. GHATI Z. CHOMETE:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa majibu mazuri ya Serikali lakini nina maswali mawili ya nyongeza.

Kwa kuwa, changamoto hii ya miundombinu ya maji mashuleni bado ni kubwa sana hasa katika Mkoa wa Mara. Je, Serikali ina mkakati gani wa kuhakikisha ina peleka miundombinu hii ya maji katika shule za Mkoa wa Mara?

Swali la pili, kwa kuwa sasa Serikali inatekeleza miradi ya ujenzi wa madarasa, ujenzi wa mabweni katika shule zetu. Je, haioni haja sasa ya kutenga fungu maalum wakati ikitekeleza miradi hiyo, inaweka na fungu la utekelezaji wa miundombinu hiyo? Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI):** Mheshimiwa Spika, nikijibu maswali mawili ya Mheshimiwa Chomete, swali la kwanza juu ya mkakati wa Serikali kuhakikisha changamoto hii inaisha.

Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema kwenye majibu yangu ya msingi, mradi huu wa *SRWSS* ni wa miaka mitano na utaisha mwaka wa fedha 2024/2025 na *value* yake jumla ni shilingi bilioni 119.6, hivyo basi Serikali inaendelea kadri siku zinavyokwenda kupunguza changamoto kwenye mashule kupitia mradi huu.

Mheshimiwa Spika, kuhusu swali lake la pili la miradi yote inayotekelezwa sasa ya ujenzi wa madarasa na ujenzi wa shule mpya, katika shule zinazojengwa hivi sasa, shule mpya lakini katika ukarabati wa vyumba vya madarasa kwenye shule mbalimbali nchini kupitia miradi ambayo ipo ya *EP4R, SEQUIP, BOOST na LANES* na mingineyo, *component* ya matundu ya vyoo vilevile na maeneo ya kuoshea mikono ipo, kwa hiyo sasa hivi Serikali inapopeleka fedha katika maeneo mbalimbali inahakikisha na hizi *facilities* zinakuwepo.

**SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. John Danielson Pallangyo, Mbunge wa Arumeru Mashariki sasa aulize swali lake.

Na. 418

**Hitaji la Soko la Kisasa Tengeru**

**MHE. DKT. JOHN D. PALLANGYO** aliuliza: -

Je, ni lini mradi wa ujenzi wa soko la kisasa Tengeru utatekelezwa ili kuongezea mapato na kuboresha huduma kwa wananchi?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI)** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI), naomba kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. John Danielson Pallangyo, Mbunge wa Jimbo la Arumeru Mashariki, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali kwa kushirikiana na Halmashauri ya Wilaya ya Meru imetenga eneo la Madiira lenye ukubwa wa ekari 15.5 kwa ajili ya ujenzi wa soko litakalokuwa na miundombinu muhimu ya soko ikiwemo huduma za wafanyabiashara wadogo wadogo.

Mheshimiwa Spika, Halmashauri inaandaa michoro ya soko la Madiira na itakapokamilika itawasilisha Ofisi ya Rais – TAMISEMI kama mradi wa kimkakati kwa hatua zaidi.

**SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. John Danielson Pallangyo, swali la nyongeza.

**MHE. DKT. JOHN D. PALLANGYO:** Mheshimiwa Spika,ahsante kwa kunipa nafasi sasa niulize maswali mawili ya nyongeza.

Kwanza, nishukuru sana kwamba Serikali ina mpango wa kutekeleza mradi wa ujenzi wa soko la kisasa eneo la Madiira, lakini ningependa kujua kwamba huo mradi utaanza lini?

Pili, soko hili la Tengeru tunalolizungumzia hapa ni soko maarufu sana la wafanyabiashara hasa akina mama wanafanya biashara zao kwa mateso makubwa wakati wa mvua, kwa sababu wanafanya kwenye matope na mvua nyingi lakini pia wakati wa jua wanaungua jua.

Je, Serikali haioni sasa ni busara kuliboresha soko hili kwa kujenga hanga kama Machinga *Complex* ya Dodoma? Nashukuru sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI):** Mheshimiwa Spika, nikijibu maswali yake mawili Mheshimiwa Pallangyo kwanza kuhusu mradi huu utaanza lini?

Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema kwenye majibu yangu ya msingi, mradi huu utaanza pale ambapo Halmashauri ya Wilaya ya Meru itawasilisha michoro yake Ofisi ya Rais, TAMISEMI ili na sisi tuweze kuipitia na kuona ni namna gani ambavyo tunaweza tukafanya marekebisho na baadae tukaipeleka Wizara ya Fedha

kwa ajili ya kupata fedha kwenye miradi ya kimkakati kama Halmashauri nyingine zinavyopata.

Mheshimiwa Spika, kuhusu swali lake la pili la kuboresha eneo la soko hili. Hizi zinatakiwa pia ziwe jitihada za Mkurugenzi wa Halmashauri pale ya Meru. Tumeona hapa katika mradi anaoutaja wa Jiji la Dodoma ilikuwa ni mradi wao wenyewe wa Jiji na wametumia mapato yao ya ndani kama Jiji la Dodoma, tumeona katika Halmashauri nyingine nchini kama Shinyanga ambapo wamejenga soko la machinga wadogo wadogo hawa kwa hela zao wenyewe za ndani na maeneo mengine ya Halmashauri zetu hapa Tanzania. Hivyo basi, nichukue nafasi hii kumwelekeza Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Meru kuhakikisha anatenga fedha kwa ajili ya kuanza ujenzi wa soko kwa ajili ya wafanyabiashara wadogo wadogo.

**SPIKA:** Maswali ya nyongeza yawe mafupi na moja kwa moja bila mchango wowote. Mheshimiwa Noah Lemburis Saputu Mollel swali la nyongeza.

**MHE. NOAH L. S. MOLLEL:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Wakati Mheshimiwa Rais alipofanya ziara Arusha, wananchi wa Jimbo la Meru Magharibi katika Kata ya Kisongo Mateves…

**SPIKA:** Swali lako.

**MHE. NOAH L. S. MOLLEL:** Rais alituahidi soko. Je, ni lini sasa Serikali kupitia TAMISEMI itajenga soko la Kisongo Mateves.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI):** Mheshimiwa Spika, kwa sababu hii kama anavyosema Mheshimiwa Lembris ni ahadi ya Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano ya Tanzania, tutakaa na wenzetu wa Halmashauri ya Wilaya kuona kama michoro iko tayari

iwasilishwe Ofisi ya Rais, TAMISEMI ili tuweze kuiombea fedha Hazina na kuanza ujenzi wake mara moja.

**SPIKA:** Mheshimiwa Sophia Hebron Mwakagenda, swali la nyongeza.

**MHE. SOPHIA H. MWAKAGENDA:** Mheshimiwa Spika,ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, katika Wilaya ya Rungwe soko la Kiwira ni soko maarufu kwa ndizi lakini lina mazingira magumu. Ni lini Serikali itatuongezea fedha kwa ajili ya kulijenga liwe la kisasa?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI):** Mheshimiwa Spika, Serikali itaongeza fedha kwa ajili ya soko hili la Kiwira pale Wilayani Rungwe kadri ya upatikanaji wa fedha lakini ni wao wenyewe kupitia Mkurugenzi wa Halmashauri kuwasilisha maombi hayo Ofisi ya Rais, TAMISEMI ili tuweze kuweka katika miradi ya kimkakati na kuanza ujenzi wa soko hili la Kiwira.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mohamed Monni swali la nyongeza.

**MHE. MOHAMED L. MONNI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Mji wa Chemba ni Mji ambao unakuwa kwa kasi sana lakini hauna soko, naomba kujua nini mkakati wa Serikali kujenga soko katika Mji wa Chemba?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI):** Mheshimiwa Spika, mkakati wa Serikali unaanza na wao wenyewe Halmashauri ya Wilaya, hatuwezi tukakaa Ofisi ya Rais, TAMISEMI tukajua kuna uhitaji wa soko katika Halmashauri ya Wilaya ya Chemba, ni wao kupitia

Baraza lao la Madiwani liibue mradi huu na kisha kufanya andiko kupitia Mkurugenzi na Afisa Mipango wake na kuwasilisha Ofisi ya Rais, TAMISEMI ili tuweze kutafuta fedha kwa ajili ya kuwajengea soko wananchi wa Chemba.

**SPIKA:** Mheshimiwa Kenneth Ernest Nollo Mbunge wa Bahi, sasa aulize swali lake.

Na. 419

**Wananchi kuwasilisha Hoja Mabaraza la Madiwani**

**MHE. KENNETH E. NOLLO** aliuliza: -

Je, kuna mpango gani wa kuweka utaratibu kwa wananchi kuwasilisha Hoja Binafsi mbele ya Mabaraza ya Madiwani?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais - TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Kenneth Ernest Nollo, Mbunge wa Jimbo la Bahi, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni za Kudumu za Halmashauri, Mwananchi wa kawadia hawezi kuwasilisha hoja binafsi katika Vikao vya Baraza la Madiwani kwa kuwa tayari yupo mwakilishi wake katika kikao hicho ambaye ni Diwani wa Kata husika.

**SPIKA:** Mheshimiwa Kenneth Ernest Nollo swali la nyongeza.

**MHE. KENNETH E. NOLLO:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa majibu ya Serikali. Pamoja na demokrasia yetu ya uwakilishi nchi zilizoendelea wamekuwa na utaratibu wa kupokea hoja za wananchi za kimaendeleo na pale wanapoziona zina maana mwananchi huyo huitwa kuja kutetea hoja yake na ambayo

inaweza kutumika kwa ajili ya kuendeleza eneo husika, jambo hili limeendelea kufanyika katika nchi nyingi zilizoendelea.

Mheshimiwa Spika, swali la pili, hivi karibuni Serikali imesitisha utoaji wa asilimia kumi kwa akina mama, vijana na watu wenye ulemavu. Kwa kuwa jambo hili lina maslahi mapana ya nchi yetu. Je, Serikali haioni haja ya kuruhusu kwamba sasa wananchi watoe maoni kuhusu jambo hili, namna bora ya kuweza kulitekeleza?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, nadhani unaweza kujibu swali la kwanza hapo, hilo swali la pili Mheshimiwa Rais aliagiza, Mheshimiwa Waziri Mkuu alilizungumzia utakuwa unamuweka mazingira magumu Mheshimiwa Naibu Waziri hapa kuanza kulizungumzia hilo.

Mheshimiwa Naibu Waziri majibu kwa hoja yake ya kwanza.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI):** Mheshimiwa Spika, nikijibu swali la Mheshimiwa Nollo ni kwamba wananchi wanapewa fursa ya kuhudhuria Mabaraza ya Madiwani na kusikiliza mijadala ambayo inaendelea, kama kuna hoja mahsusi kwa mwananchi au ana *idea* yoyote ambayo anataka kuiwasilisha anaweza akaonana na Mwenyekiti wa Halmashauri, akazungumza nae na kumpa wazo hilo, kisha Mwenyekiti wa Halmashauri anawasilisha lile kwa wenzake ambao ni Baraza la Madiwani, wakiona inafaa anaalikwa yule mwananchi ili aweze kutoa *presentation* mbele ya Baraza la Madiwani.

Mheshimiwa Spika, utaratibu huo upo, kwa hiyo niombe tu wananchi wa kule Bahi na maeneo mengine, kuhakikisha kwamba kama kuna mwananchi ana *idea* nzuri ya kusaidia jamii na Halmashauri, basi awasiliane na Mwenyekiti wa Halmashauri ili Mwenyekiti wa Halmashauri aweze kuongea na Madiwani wenzake na kumkaribisha mwananchi huyo katika Mabaraza ya Madiwani kwenda kufanya *presentation*. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge. Tunaenda Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira, Mheshimiwa Latifa Khamis Juwakali, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 420

**Changamoto za Muungano**

**MHE. LATIFA KHAMIS JUWAKALI** aliuliza:-

Je, zimebaki changamoto ngapi za Muungano kutatuliwa baada ya kufanyika jitihada za kuzipunguza?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kwa niaba ya Ofisi ya Makamu wa Rais majibu.

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI K.n.y WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, ahsante. Kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Latifa Khamis Juwakali, Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, changamoto au hoja Muungano zilizobaki na ambazo zinaendelea kutafutiwa ufumbuzi ni nne (4). Hoja hizo ni Mapendekezo ya Tume ya Pamoja ya Fedha, Usajili wa Vyombo vya Moto, Uingizaji wa sukari inayozalishwa Zanzibar katika Soko la Tanzania Bara, na Mgawanyo wa mapato yatokanayo na hisa za *SMZ* zilizokuwa katika Bodi ya Sarafu ya Afrika Mashariki na faida ya Benki Kuu.

Mheshimiwa Spika, changamoto hizo zipo katika hatua mbalimbali za majadiliano na ni matumaini ya Serikali zetu mbili kuwa changamoto zote zitapatiwa ufumbuzi.

**SPIKA:** Mheshimiwa Latifa Juwalikali.

**MHE. LATIFA KHAMIS JUWAKALI:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Kwanza nimpongeze Mheshimiwa Waziri kwa majibu mazuri ya Serikali lakini nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, wakati mwingine kusuasua kwa utekelezwaji wa changamoto inapelekea kuibuka kwa changamoto mpya za Muungano. Ni nini *commitment* ya Serikali kuweza kuzuia changamoto yoyote nyingine ya Muungano isijitokeze?

Swali langu la pili, Serikali inatoa *commitment* gani ya kutatua changamoto hizi nne zilizobakia? Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI K.n.y WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Nikianza na swali la kwanza la Mheshimiwa Mbunge namna ya kuzuia changamoto nyingine mpya zisijitokeze, hili ni juhudi ya Serikali zote mbili kuhakikisha wakati wote mara baada ya maamuzi yale yanayojitokeza katika vikao vile vya majadiliano vilivyotatua ile migogoro kuanza utekelezaji mara moja wa yale makubaliano waliyofikia.

Mheshimiwa Spika, jambo la pili, hizi changamoto nne zilizobaki mkononi tunatarajia kwamba kikao chetu kitakuwa mwezi wa Agosti, ambapo katika mazingira ya kawaida hizi zilizobaki ni chache sana tunaweza tukafika mahali, Mungu jalia tutazimaliza zote nne na watu tutaanza kufaida matunda ya Muungano wetu. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Fakharia Shomar Khamis, swali la nyongeza.

**MHE. FAKHARIA SHOMAR KHAMIS:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kuniona. Kwa kuwa kero za Muungano zina zungumzika, Je, vile vikao vya Wizara moja moja baina ya *SMT* na *SMZ* ambao hukaa kuzungumza kero zao bado vinaendelea au vimefunikwa na hivyo vikao vikubwa?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI K.n.y WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Kwanza kwa msingi wa mazungumzo ya utatuzi wa migogoro hii ambayo iko kati yetu, kitu cha kwanza kabisa ni Wizara zile zenye matatizo yanayosababisha tukasoma kama tatizo kuu kukutana mara kwa mara, kwa sababu hawa ni kama *Technical Committee* ambazo zinatafuta majibu kwa ajili ya kupeleka kwenye kile kikao kikuu. Kwa hiyo, nikuhakikishie Mheshimiwa Mbunge, tunaendelea na vikao vya Wizara kati ya Wizara na Wizara. Kwa mfano, katika haya yaliyobaki Wizara ya Fedha Zanzibar na Wizara ya Fedha Tanzania Bara wanaendelea kuchakata mambo mbalimbali ambayo mwisho wa yote yatatuletea majibu ya utekelezaji. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri tunakushukuru sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge. Wizara ya Katiba na Sheria, Mheshimiwa David Mwakiposa Kihenzile, Mbunge wa Mufindi Kusini, swali lake litaulizwa kwa niaba yake na Mheshimiwa Judith Salvio Kapinga.

Na. 421

**Kukamilisha Usajili wa IFRC nchini**

**MHE. JUDITH S. KAPINGA K.n.y. MHE. DAVID M. KIHENZILE** aliuliza: -

Je, ni lini Serikali itakamilisha usajili wa Shirikisho la *International Federation of Cross and Crescent nchini*?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri Ofisi ya Waziri Mkuu kwa niaba ya Wizara ya Katiba na Sheria majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU (MHE. PASCHAL P. KATAMBI) K.n.y WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Katiba na Sheria naomba kujibu swali la Mheshimiwa David Mwakiposa Kihenzile Mbunge wa Mufindi Kusini, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, Shirikisho la Kimataifa la Msalaba Mwekundu *(International Federation of Red Cross and Crescent - IFRC)* ni Shirika la Kimataifa linalounganisha vyama vya nchi mbalimbali vya Msalaba Mwekundu. Nchini Tanzania Chama cha Msalaba Mwekundu kilianzishwa chini ya Sheria Na. 71 mwaka 1962 kufuatia nchi yetu kuridhia mikataba ya Geneva yam waka 1949. Kazi kubwa ya Shirikisho hili ni kufanya shughuli za kusaidia wahanga wa maafa na kuimarisha uwezo wa wanachama wake katika kukabiliana na maafa. Kutokana na umuhimu wa Shirikisho hilo kwa nchi yetu, tayari Serikali imekamilisha majadiliano na uongozi wa *IFRC* na zoezi la kuwashirikisha wadau wote wanaohusika hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, kwa sasa, Serikali iko katika hatua za mwisho kukamilisha mkataba na shirikisho hilo, hatua hizo zitakapokamilika mkataba utasainiwa na Ofisi za *IFRC* kufunguliwa nchini na kuanza kufanya kazi. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Judith Salvio Kapinga swali la nyongeza.

**MHE. JUDITH S. KAPINGA:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Naishukuru Serikli kwa kuanza mchakato huu muhimu kwa nchi yetu, hata hivyo nina maswali mawili kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, mchakato huu wa kusajili Shirikisho la Kimataifa la Msalaba Mwekundu *(IFRC)*tumeambiwa uko kwenye mchakato kwa kipindi kirefu sana, takribani miaka thelathini sasa. Serikali sasa inatuambia mchakato utakamilika lini na mkataba kusainiwa ili shirika hili lianze kufanya kazi hapa nchini kwetu?

Swali la pili Serikali imejipanga vipi kulinda maslahi ya Watanzania katika mikataba itakayosainiwa ili kuhakikisha shirika hili la Kimataifa litakapoanzishwa ajira kwa Watanzania zitakuwepo kuliko kuajiri watu wa nje zaidi? Ahsante.*(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Nasibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU (MHE. PASCHAL P. KATAMBI) K.n.y WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Judith Kapinga kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, kwanza niwapongeze sana *Red Cross* Tanzania wamekuwa wakisimamia mchakato huu kwa muda mrefu sana kuweza kuhakikisha hata hatua hii inaweza kufikiwa na wamekuwa wakifanya kazi kubwa, kazi mbalimbali za Kitaifa, sherehe za Kimataifa, wakati wa maafa, pia wamekuwa wadau muhimu sana wa Serikali katika masuala ya maafa kwa hiyo ninawapongeza sana, pili ninawapongeza uongozi ambao umefanya kazi kubwa.

Mheshimiwa Spika, swali la kwanza ambalo ameeleza kuhusiana na kuchukua muda mrefu, kama nilivyoeleza kwenye jibu langu la msingi, tayari itifaki zote zimeshafanyika. Kwanza kuwasiliana na Shirikisho lenyewe; pili, kukutana na wadau na tatu, sasa iko kwenye hatua ya Wizara ya Mambo ya Nje katika kukamilisha tu itifaki za Serikali na taratibu za ndani ili kuweza kufanikisha jambo hili. Ndiyo maana tukasema kama Serikali kwamba sasa limefikia mwisho. Kwa hiyo, nawapongeza sana kwa hatua za ufuatiliaji.

Mheshimiwa Spika, pili, swali lake la kuhusiana na masilahi, ni kweli kwamba mashirika haya kimataifa yamekuwa yakija kufanya kazi nchini lakini tunaangaliaje ajira za wazawa?

Mheshimiwa Spika, Bunge lako Tukufu lilipitisha Sheria hapa ya Mwaka 2005 inayoruhusu uratibu wa ajira za wageni. Imekuwa ni wakati wote, hata kwenye Sheria ya Usajili wa Makampuni Sura Na. 212 inaelekeza namna unaposajiliwa kama kampuni, taasisi au asasi za kiraia, sharti ni kwamba waajiriwe Watanzania. Inapotokea ameajiriwa mgeni ni pale tu ambapo aidha taaluma yake ni maalum sana, au ufahamu au *knowledge* aliyonayo ni adimu hapa nchini kwamba hatuwezi kumpata Mtanzania mwenye sifa hiyo. Kwa hiyo, nitoe agizo hapa kwa taasisi zote, mashirika ya Kimataifa pamoja na Makampuni ya kiuwekezaji ya nje yaendelee kuzingatia utekelezaji wa Sheria ya Mwaka 2005 ya Kuratibu Ajira za Wageni inayowataka waangalie matakwa ya ajira za Watanzania.

Mheshimiwa Spika, pia usajili wa *IFRC* utakuwa chini ya msukumo wa *Red Cross* Tanzania. Tutawaomba *Red Cross* nao waendelee kutusaidia kupata taarifa na kuratibu ili ajira za Watanzania zisipotee, ahsante sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge. Wizara ya Maji, Mheshimiwa Joseph Zacharius Kamonga, Mbunge wa Ludewa, sasa aulize swali lake.

Na. 422

**Kutenga fedha kwa ajili ya mradi wa kutoa maji Ziwa Nyasa kwenda Ludewa**

**MHE. JOSEPH Z. KAMONGA** aliuliza:-

Je, lini fedha itatengwa kufanya usanifu na upembuzi yakinifu wa Mradi wa kutoa maji Ziwa Nyasa kupeleka Tarafa ya Masasi – Ludewa?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji, Mhandisi Maryprisca Mahundi, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, ahsante. Kwa niaba ya Waziri wa Maji, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Joseph Zacharius Kamonga, Mbunge wa Ludewa, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Tarafa ya Masasi Wilaya Ludewa ina jumla ya vijiji 15, ambapo vijiji 12 vinapata huduma ya maji na vijiji viwili vya Igalu na Kiyogo utekelezaji wa miradi unaendelea na unatarajia kukamilika mwezi Juni, 2023.

Mheshimiwa Spika, mojawapo ya vipaumbele vya Wizara kwa mwaka 2023/2024 ni kusanifu na kutekeleza miradi ya maji kwa kutumia vyanzo vya uhakika ikiwemo maziwa makuu, kupeleka maji kwenye maeneo yenye uhaba pamoja na vijiji vilivyomo pembezoni mwa maziwa hayo. Kwa upande wa Ziwa Nyasa, fedha za awali zimeshatengwa kwa ajili ya usanifu na tathmini ya athari za kimazingira na kijamii ambapo vijiji vya Tarafa ya Masasi Wilayani Ludewa vitanufaika na miradi ya maji kupitia chanzo hicho.

**SPIKA:** Mheshimiwa Joseph Kamonga, swali la nyongeza.

**MHE. JOSEPH Z. KAMONGA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa majibu mazuri sana ya Mheshimiwa Naibu Waziri, hasa kwenda kwenye chanzo cha uhakika. Pamoja na majibu hayo mazuri, naomba kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, Kata ya Mlangali na Lugarawa ni kata ambazo zina ongezeko na kasi ya idadi ya watu tofauti na uwepo wa huduma za maji. Nini mpango wa Serikali kutenga fedha hizo kwenye bajeti ijayo ili kata hizo mbili ziweze kupata maji?

Mheshimiwa Spika, swali la pili. Kitongoji cha Lutala la Kisaula, vina idadi kubwa ya wananchi na hadhi ya vijiji, lakini kwa muda mrefu vimekuwa na changamoto ya maji. Mheshimiwa Naibu Waziri, alishaelekeza wataalam wa-*extend* Mradi wa Iwela kuhudumia maeneo hayo...

**SPIKA:** Swali lako Mheshimiwa.

**MHE. JOSEPH Z. KAMONGA:** Mheshimiwa Spika, je, ni lini maelekezo hayo ya Serikali yatatekelezwa?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Kamonga, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli Mlangali na Lugarawa Mheshimiwa Mbunge, tulikwenda na tumeshudia kwa pamoja, lakini tayari kama Wizara tunaendelea kuchukua hatua mbalimbali ili tuweze kutumia vyanzo vile vya uhakika; ile mito yetu miwili, Mto Salali na Mto Mbiliwili. Tutahakikisha tunatumia mito hii pale ambapo usanifu utakapokamilika na kuonekana na maji ya kutosha, ndiyo mto ambao tutautumia. Hili Mheshimiwa Mbunge amefuatilia kwa muda mrefu na tulikwenda pamoja.

Mheshimiwa Spika, vile vile, masuala ya Kitongoji cha Kisaula na Lutala, wakati Mheshimiwa Waziri anahitimisha hapa hoja za bajeti yetu ya mwaka 2023/2024, tayari imeonesha tumetenga Shilingi milioni 20.7 kwa ajili ya kufanya upimaji, usanifu na kupanua mtandao wa maji kutoka Mradi wa Maji Iwela. Kwa hiyo, hili tayari tumeshalifanyia kazi. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu waziri, ahsante sana kwa majibu yako, kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi, Mheshimiwa Dkt. David Mathayo David, Mbunge wa Same Magharibi, sasa aulize swali lake.

Na. 423

**Ujenzi wa Barabara ya Mwembe - Mbaga – Mamba**

**MHE. DKT. DAVID M. DAVID** aliuliza:-

Je, lini Serikali itaanza ujenzi wa Barabara ya Mwembe – Mbaga hadi Mamba kwa kiwango cha lami?

**SPIKA:** Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Mheshimiwa Mhandisi Godfrey Kasekenya Msongwe, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. David Mathayo David, Mbunge wa Same Magharibi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali inaendelea kutafuta fedha kwa ajili ya kuifanyia upembuzi yakinifu na usanifu wa kina kwa ajili ya ujenzi kwa kiwango cha lami barabara ya kutoka Mwembe – Mbaga hadi Mamba ambayo inaitwa Mwembe – Myamba – Ndungu yenye urefu wa kilometa 90.19. Baada ya usanifu kukamilika Serikali itatafuta fedha kwa ajili ya kuanza ujenzi.

**SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. David Mathayo David, swali la nyongeza.

**MHE. DKT. DAVID M. DAVID:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, hii ni mara ya tatu kama siyo ya nne tunauliza swali hili tunaambiwa kwamba Serikali itatafuta fedha.

Tunaomba kauli ya Serikali, ni lini fedha itapatikana? Hii ni ahadi ya Rais toka mwaka 2005 mpaka leo fedha za upembuzi yakinifu na usanifu wa kina hazijapatikana? Hilo la kwanza.

Mheshimiwa Spika, swali la pili, katika Kata ya Mhezi, Mshewa na Msindo, barabara hii inaponyesha mvua kidogo inaharibika sana kiasi ambacho magari hayapiti kabisa. Kwa hiyo, mawasiliano yanafungwa kati ya Kata hizo na Same: Je, ni lini Serikali itaweka zege katika barabara hiyo kwa maeneo hayo niliyoyataja kabla ya upembuzi yakinifu na upembuzi wa kina kukamilika ili barabara hii ijengwe kwa kiwango cha lami? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema, naomba kujibu maswali mawili ya Mheshimiwa Mbunge, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema katika jibu la msingi, tunatambua umuhimu wa barabara hii na ndiyo maana katika jibu la msingi nimesema tunaendela kutafuta fedha kwa ajili ya kuifanyia upembuzi yakinifu na usanifu wa kina.

Mheshimiwa Spika, bahati nzuri barabara hii mimi nimetembelea yote na tulishatoa maagizo na tayari tumeshaainisha maeneo yote korofi likiwemo eneo hilo la Msindo, Mshewa na Mhenzi. Meneja wa *TANROADS* Mkoa wa Kilimanjaro ameshatengeneza bajeti na hivi ninavyoongea amesha-*submit* kwa Mtendaji Mkuu wa *TANRIOAD* ili aweze kutoa fedha kujenga hayo maeneo korofi ama kwa lami nyepesi ama kwa zege ili barabara hii iweze kupitika yote kwa mwaka mzima, ahsante.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, pamoja na maelezo yote yaliyotoka jana na yale makofi, bado mmesimama! Nilifikiri barabara zenu zote mmeziona jana.

Mheshimiwa Jerry Silaa, swali la nyongeza.

**MHE. JERRY W. SILAA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Barabara ya Msongola – Mbande nilipewa ahadi kwenye bajeti ya mwaka 2022/2023 itakamilishwa yote kilometa 4.95 kwa kiwango cha lami. Naomba *commitment* ya Serikali kutimiza ahadi hii iliyotolewa mwaka 2022 hapa Bungeni? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mbunge, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli barabara aliyoitaja ambayo inaanzia Pugu – Mvuti – Msongola – Mbande inaunganisha majimbo mawili; Jimbo la Mheshimiwa Silaa na Jimbo la Mbagala la Mheshimiwa Chaurembo. Tuna kilometa nne *point* ambazo bado hazijakamilika. Nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba katika bajeti tunayokwenda kuitekeleza tutakamilisha kwa lami kipande kilichobaki, ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Iddi Kassim Iddi, swali la nyongeza.

**MHE. IDDI K. IDDI:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Ni lini Serikali itaanza ujenzi wa kiwango cha lami barabara inayotoka Kahama – Busangi – Chela – Nyang'wale mpaka Busisi?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali nyongeza la Mheshimiwa Mbunge, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, barabara aliyoitaja tunakamilisha upembuzi yakinifu na usanifu wa kina kwa maana ya kutoka Kahama kwenda Busisi. Pia, baada ya hapo ndiyo tutaanza kuijenga kwa kiwango cha lami, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Asia Halamga, swali la nyongeza.

**MHE. ASIA A. HALAMGA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii ya kuuliza swali la nyongeza. Je, ni lini Serikali itajenga kwa kiwango cha lami barabara ya Galapo, Orkasmet hadi Kibaya Kiteto? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Spika, tunapoongea sasa hivi, barabara aliyoitaja ndiyo tunakamilisha usanifu wa kina na baada ya hapo tutatafuta fedha kuanza kuijenga kwa kiwango cha lami, ahsante.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Mheshimiwa Hassan Zidadu Kungu, Mbunge wa Tunduru Kaskazini,

Na. 424

**Ujenzi wa barabara ya Tunduru - Mtwara Pachani**

**MHE. HASSAN Z. KUNGU** aliuliza:-

Je, lini Serikali itajenga angalau kilometa tano kwa kiwango cha lami Barabara ya Tunduru - Mtwara Pachani?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Hassan Zidadu Kungu, Mbunge wa Tunduru Kaskazini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali imeanza ujenzi wa barabara ya Mtwara Pachani – Lusewa – Lingusenguse – Nalasi hadi Tunduru

yenye urefu wa kilometa 300 kwa awamu ambapo jumla ya kilometa 3.23 zimejengwa kwa lami nyepesi katika maeneo ya miji midogo ya Mkongo, Ligela, Lusewa na Sasawala. Aidha, mwezi Machi, 2023 Serikali kupitia Wakala wa Barabara Tanzania *(TANROADS)* imesaini mkataba kwa ajili ya ujenzi kwa kiwango cha lami wa kipande cha mita 500 katika eneo la Tunduru Mjini. Vile vile, Serikali imekamilisha kazi ya Upembuzi yakinifu na usanifu wa kina kwa ajili ya ujenzi kwa kiwango cha lami wa barabara hii.

Mheshimiwa Spika, baada ya Usanifu kukamilika Serikali inaendelea kutafuta fedha za kuendelea na ujenzi, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Hassan Zidadu Kungu, swali la nyongeza.

**MHE. HASSAN Z. KUNGU:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Serikali, naomba kuuliza maswali mwili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, swali la kwanza: Je, ni lini ujenzi huo wa mita 500 utaanza?

Mheshimiwa Spika, swali la pili. Barabara hii ya lami inapita katikati ya Mji na ndiyo kwenye sura ya Wilaya ya Tunduru: Je, ni lini Serikali itatufungia taa za barabara ili kusaidia ulinzi na usalama nyakati za usiku? Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Mbunge, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, mita 500, tunavyoongea mkandarasi ameshapatikana na sasa hivi anajiandaa, yuko kwenye *mobilization* kuanza kujenga hizo mita 500 kwa mwaka huu wa fedha.

Mheshimiwa Spika, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, habari njema kwamba mwaka ujao katika huo mji ambao taasisi zote zinapita katika barabara ya *TANROADS,* tutajenga kilometa 2.1 na kuweka taa eneo lote katika mji huo wa Tunduru, ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Daimu Iddi Mpakate, swali la nyongeza.

**MHE. DAIMU I. MPAKATE:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Katika barabara ya Tunduru – Nalasi, kipande cha kutoka Chiwana mpaka Mbesa kina matatizo ya kupitika wakati wa mvua: Je, ni lini Serikali itaweka lami nyepesi kwenye kipande hicho wakati wanasubiri fedha za kujenga kipande hicho?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mbunge, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema katika jibu langu la msingi na barabara hii niliitembelea, Waziri alishaahidi na mimi nilipita. Maeneo yote korofi tumeyaainisha na tumetoa maelekezo kwa Meneja wa Mkoa wa Ruvuma kwamba barabara hii yenye urefu wa kilometa 300 maeneo yote ayafanyie kazi kwa maana ya kuainisha maeneo korofi na pia kujenga kwa kiwango cha zege ama lami maeneo yote korofi ili barabara hii iweze kupitika kwa mwaka mzima, ikiwa ni pamoja na eneo alilolitaja Mheshimiwa Mbunge, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Issa Mtemvu, swali la nyongeza.

**MHE. ISSA J. MTEMVU:** Mheshimiwa Spika, barabara ya njia nane kilometa 19.2 kutoka Kimara hadi Kibaha, imekosa kabisa vituo vya dala dala kwa abiria kupumzika; kwa hiyo, wanaumia na jua na mvua: Je, ni lini Serikali itatengeneza hivi vituo?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Spika, ahsante. Japo suala hili Mheshimiwa Mbunge amekuwa akilileta mara kwa mara, lakini nimhakikishie kwamba pia Kamati ya Miundombinu imeshatoa maelekezo kwa Wizara kuhakikisha kwamba suala hili inalifanyiwa kazi. Kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba suala hili tumeshaliona na tayari Wizara imeshalipokea kwa ajili ya kutengeneza hivyo vituo kama alivyovitaja Mheshimiwa Mbunge, ahsante sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Tunza Issa Malapo, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Mheshimiwa Naibu waziri, ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Na. 425

**Utekelezaji wa Mradi wa *Mtwara Corridor***

**MHE. TUNZA I. MALAPO** aliuliza:-

Je, Utekelezaji wa mradi wa Mtwara *Corridor* umefikia hatua gani?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Mheshimiwa Atupele Fredy Mwakibete, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI (MHE. ATUPELE F. MWAKIBETE)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Tunza Issa Malapo, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Ushoroba wa Mtwara *(Mtwara Corridor)* unajumuisha miradi ya Sekta mbalimbali ikiwa pamoja na Madini, Uchukuzi na Kilimo. Kwa upande wa Sekta ya Uchukuzi, Serikali

kupitia Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania *(TPA)* imetekeleza miradi ya ujenzi wa gati kubwa na la kisasa katika Bandari ya Mtwara lenye urefu wa mita 300. Ujenzi wa Bandari ya Ndubi ambao ulikamilika tangu Desemba, 2021 na Ujenzi wa bandari mpya ya *Mbamba Bay* ambao upo katika hatua za manunuzi ya Mkandarasi.

Mheshimiwa Spika, aidha, Serikali kupitia Shirika la Reli *(TRC)* imekamilisha kazi ya upembuzi yakinifu na usanifu wa awali kwa ajili ya ujenzi wa reli ya *Standard Gauge* ya Mtwara - *Mbamba Bay* na matawi yake kuelekea Liganga na Mchuchuma. Mradi huu unatarajiwa kutekelezwa kwa utaratibu wa ubia kati ya sekta ya Umma na sekta binafsi.

Mheshimiwa Spika, pamoja na taarifa hizo za miradi, naomba kulifahamisha Bunge lako kuwa, gati jipya lililojengwa katika Bandari ya Mtwara limeanza kuhudumia meli za makasha pamoja na shehena ya Kichele na takriban kila baada ya wiki moja kuanzia tarehe 20/04/2023 limekuwa likihudumia mizigo ya makasha ya yanayokwenda visiwa vya Comoro.

Mheshimiwa Spika, vikao vya wadau wa Ushoroba wa Mtwara vimeanza kuratibiwa chini ya Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi ili kuweka mikakati ya kuendelea kuutangaza zaidi ushoroba huo na kuwavutia wananchi waishio ukanda huo pamoja na nchi jirani kutumia Bandari ya Mtwara na kuufanya ushoroba huo kutumika ipasavyo, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Tunza Malapo, swali la nyongeza.

**MHE. TUNZA I. MALAPO:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Reli ya Kutoka Mtwara mpaka *Mbamba Bay* ni miongoni mwa miradi midogo iliyopo katika Mradi huu mkubwa wa Mtwara *Corridor*. Serikali imesema itatekeleza mradi huu kwa ubia. Mimi nataka kujua kwa nini Serikali isitekeleze mradi huu yenyewe ikizingatia umuhimu wake kuliko kusubiria ubia ambao hauna uhakika utapatikana lini?

Mheshimiwa Spika, swali langu la pili, mwaka 2004 Lilongwe – Malawi kulisainiwa mkataba wa utekelezaji wa Mradi huu wa *Mtwara Corridor* na Tanzania inatakiwa iitishe Mkutano ili kutathmini utekelezaji wa mradi huu umefikia hatua gani? Mpaka leo Tanzania haijaitisha: Nataka kujua, ni lini Serikali ya Tanzania itaitisha mkutano huo wa nchi nne; Msumbiji, Malawi, Zambia na Tanzania yenyewe ili kutathmini mradi huu umefikia hatua gani kwa sababu ni mradi muhimu sana katika mikoa ya kusini?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI (MHE. ATUPELE F. MWAKIBETE):** Mheshimiwa Spika, ahsante. Napenda kujibu maswali mawili ya Mheshimiwa Tunza Issa Malapo, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali imefanya uamuzi wa kuzishirikisha sekta binafsi ili kuongeza tija. Pia, kwa sababu Serikali ina *commitment* nyingi, inaweza ikachelewa kupata fedha kwa ajili ya huu mradi. Hata hivyo, kuna makampuni zaidi ya manne kutoka China, *South Africa*, *Australia* pamoja na Marekani, ambao wameonesha nia ya kuwekeza katika mradi huu wa ubia, ukizingatia kwamba eneo hili tayari ni *potential* kubwa. Uwepo wa makaa ya mawe pamoja na chuma unasababisha wawekezaji hawa waje. kwa sababu tayari mzigo upo *metric ton* zaidi ya milioni 428 ambapo tunaweza tukachimba zaidi ya miaka 100. Kwa hiyo, sekta binafsi tayari imeonesha utayari huo. Kwa hiyo, tutaendelea kuwa-*engage* ili mradi huu uweze kuanza mara moja.

Mheshimiwa Spika, swali la pili anataka kujua ni lini sasa Mkutano wa Wakuu wa Nchi utaitishwa. Tarehe 15 ya Mwezi wa Sita kutakuwa na mkutano wa wadau wote wa sekta na Wizara ya Madini, Wizara ya Viwanda, Wizara ya Uchukuzi, wadau kutoka sekta binafsi pamoja na taasisi zote za Serikali hususani *TRA*, *MSCL*, *TPA, RAS* Mtwara, *RAS* Lindi na Waheshimiwa Wabunge wa Mtwara na Lindi mnakaribishwa kwa ajili ya kujadili jambo hili kama

maandalizi ya kuzi–*engage* nchi zingine za Msumbiji pamoja na Malawi, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge. Tunaendelea na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, Mheshimiwa Stella Ikupa Alex, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 426

**Kuingiza Lugha ya Alama kwenye Mitaala ya Elimu nchini**

**MHE. STELLA I. ALEX** aliuliza:-

Je, nini mpango wa Serikali kuingiza lugha ya alama kwenye mitaala ya elimu nchini?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri Ofisi ya Rais TAMISEMI, kwa niaba ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI) K.n.y WAZIRI WA ELIMU SAYANSI NA TEKNOLOJIA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Elimu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Stella Ikupa Alex, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali inao mpango wa kuingiza lugha ya alama kwenye mitaala ya elimu nchini kwa lengo la kutatua changamoto ya mawasiliano kwa wanafunzi viziwi na katika jamii. Aidha, katika mchakato wa mapitio ya sera ya mitaala unaoendelea somo la Lugha ya Alama limependekezwa liwe la lazima kwa walimu wote tarajali katika vyuo vyote vya ualimu na vyuo vikuu nchini.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kuwepo kwa mpango na mapendekezo hayo, tayari Serikali imeandaa na kusambaza kamusi ya lugha ya alama ya Tanzania ya kidijitali katika shule na vyuo vinavyopokea wanafunzi viziwi. Aidha, kozi ya lugha ya alama ya Tanzania inatolewa katika Chuo cha Ualimu Patandi na Kabanga na katika Vyuo Vikuu vya Dodoma, Dar es Salaam na *Archbishop* Mihayo *University College* Tabora kwa lengo la kumudu darasa jumuishi. Aidha, Serikali imeendelea kutoa mafunzo kwa walimu maalum na wasio wa elimu maalum 3,650 wa shule za msingi na sekondari kwa lengo la kuwajengea uwezo wa namna bora ya kuwafundisha na kuwahudumia wanafunzi viziwi ili kujenga jamii jumuishi ya viziwi shuleni.

**SPIKA:** Mheshimiwa Stella Ikupa Alex.

**MHE. STELLA I. ALEX:** Mheshimiwa Spika, ninaishukuru na kuipongeza Serikali kwa hatua hii kubwa na muhimu iliyofikiwa kama ambavyo imeelezwa kwenye jibu la msingi. Kwa sababu haya yalikuwa ni maombi na mapendezo ya muda mrefu na mara kwa mara kupitia Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Spika, ninaomba niishauri Serikali, mapendekezo yaliyoelezwa kwenye jibu la msingi yaweze kuzingatiwa ili kwa siku za usoni lugha ya alama iweze kuwa lugha ya kufundishia na mawasiliano katika nchi yetu ya Tanzania. Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri ushauri huo nadhani umeupokea.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI):** Mheshimiwa Spika, ndiyo, ushauri huo Serikali imepokea.

**SPIKA:** Haya ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge. Wizara ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara, Mheshimiwa Michael Constantino Mwakamo, Mbunge wa Kibaha Vijijini, sasa aulize swali lake.

Na. 427

**Mwongozo kwa wawekezaji kuchangia katika shughuli za jamii**

**MHE. MICHAEL C. MWAKAMO** aliuliza:-

Je, kuna mpango gani wa kutoa mwongozo kwa wawekezaji kuchangia shughuli za maendeleo katika maeneo wanayowekeza?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Uwekezaji, Viwanda na Biashara, Mheshimiwa Exaud Kigahe, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UWEKEZAJI, VIWANDA NA BIASHARA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa niaba ya Waziri wa Uwekezaji, Viwanda na Biashara, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Michael Costantino Mwakamo, Mbunge wa Jimbo la Kibaha Vijijini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, katika kuhakikisha wawekezaji wanachangia shughuli za maendeleo za jamii katika maeneo wanayowekeza, Serikali ina sheria za kisekta na miongozo inayosimamia wawekezaji katika sekta ya uziduaji ambayo ni mwongozo wa ushiriki wa Watanzania katika sekta ndogo ya mafuta 2019, mwongozo wa kuwasilisha mpango wa ushiriki wa Watanzania katika sekta ya madini wa mwaka 2018 na mwongozo kwa Mamlaka za Serikali za Mitaa kuhusu uwajibikaji kwa jamii wa makampuni wa mwaka 2022. Aidha, Serikali iliandaa mwongozo wa Taifa wa ushiriki wa Watanzania katika sekta mbalimbali wa mwaka 2019 kwa ajili ya kusimamia masuala ya ushiriki wa Watanzania katika miradi ya kimkakati na uwekezaji. Utaratibu huo unaruhusu wawekezaji kuchangia sehemu ya mapato yake kwa jamii ikiwa ni sehemu ya uwajibikaji kwa jamii na kuchangia shughuli za maendeleo katika eneo la uwekezaji kupitia Mamlaka za Serikali za Mitaa. Nakushukuru.

**SPIKA:** Mheshimiwa Michael Mwakamo, swali la nyongeza.

**MHE. MICHAEL C. MWAKAMO:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa majibu mazuri ya Serikali lakini nina maswali mawili madogo ya nyongeza.

Swali la kwanza, kwa kuwa Jimboni Kibaha Vijijini kuna kongani kubwa ya viwanda Kwara na viongozi wa eneo hilo hawana uelewa wa kutosha juu ya miongozo hiyo. Je, Serikali haioni ipo haja sasa ya kufika Jimboni Kibaha kuwapa mwongozo ili waweze kusimamia chanzo hiki cha mapato?

Swali la pili, kwa kuwa maeneo ya Kibaha Vijijini , viwanda vingi vitajengwa na vingine vitatumia Sheria ya *EPZ*. Je, Serikali ina mpango gani sasa wa kubadilisha sheria ili viwanda hivi vitakavyojengwa kwenye *EPZ* viweze kuchangia shughuli ya maendeleo? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UWEKEZAJI, VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Ni kweli Kibaha katika Mkoa wa Pwani ni moja ya maeneo ambayo kuna uwekezaji mkubwa sana wa viwanda hapa nchini. Kwa takwimu tulizonazo kwa Aprili tu takribani miradi saba imewekezwa katika eneo hili ambalo ni muhimu sana kwa wawekezaji wengi.

Mheshimiwa Spika, Wizara na Serikali kama nilivyosema, maeneo yote ya uwekezaji pamoja na eneo la Kwala *Industrial Park* ambalo linajengwa pale, tunawaelekeza wawekezaji kuhakikisha wanachangia maendeleo na miradi ya kijamii. Pili katika maeneo hayo tumeshaweka kwenye Serikali za Mitaa Idara Maalum ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara ambao kazi yao wao ni kuwaelimisha wawekezaji hawa kwa kushirikiana na TAMISEMI kuhakikisha wanachangia mapato wanayopata kutoka na uwekezaji huo.

Mheshimiwa Spika, pili, kwenye maeneo ya uzalishaji kwa ajili ya mauzo nje *EPZ* tumeshasema na tunao mpango wa kuweka

utaratibu wa uwekezaji, ambao unaelekeza wawekezaji hawa ambao wanafaidika, wananufaika na vivutio maalum ambayo kimsingi ni kodi za Watanzania, kuhakikisha mapato wanaopata au faida wanazopata kutokana na uwekezaji huo waweze kurudisha kwa wananchi kupitia shughuli mbalimbali za kijamii, kama ni elimu, afya, maji au barabara kulingana na mahitaji ya maeneo husika ambayo wanawekeza wawekezaji hao, nakushukuru sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge. Wizara ya Kilimo, Mheshimiwa Flatei Gregory Massay, Mbunge wa Mbulu Vijijini, swali lake litaulizwa kwa niaba yake na Mheshimiwa Mhandisi Samweli Hhayuma.

Na. 428

**Kupeleka mbegu za mahindi ya ruzuku kabla ya masika Mbulu Vijijini**

**MHE. ENG. SAMWELI X. HHAYUMA K.n.y. MHE. FLATEI G. MASSAY** aliuliza:-

Je, kuna mpango gani wa kupeleka mbegu za mahindi kabla ya kipindi cha masika katika Jimbo la Mbulu Vijijini?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Kilimo, Mheshimiwa Antony Peter Mavunde, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Flatei Gregory Massay, Mbunge wa Mbulu Vijijini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, mpango wa kuwafikishia wakulima pembejeo za kilimo kwa wakati ikiwemo mbegu bora za mahindi katika Jimbo la Mbulu Vijijini na maeneo mengine nchini unahusisha

kukusanya takwimu za mahitaji halisi na kuratibu usambazaji wa pembejeo hizo kupitia sekta ya umma na sekta binafsi kabla ya msimu wa kilimo kuanza.

Mheshimiwa Spika, katika msimu wa mwaka 2022/2023 na mwaka 2023/2024 Serikali kupitia Wakala wa Mbegu za Kilimo *(ASA)* ambayo ni Taasisi ya Serikali imeendelea kusambaza mbegu bora za mahindi katika maeneo mbalimbali kwa bei nafuu ambayo ina ruzuku ndani yake. Ninaomba nitumie fursa hii kupitia Bunge lako Tukufu kuzishauri Halmashauri za Wilaya ikiwa ni pamoja na Halmashauri ya Wilaya ya Mbulu kutenga fedha zitakazowezesha kuendelea kununua mbegu za mahindi pamoja na mbegu za mazao mengine kupitia Wakala wa Mbegu za Kilimo *(ASA)* ambao huuza mbegu kwa bei nafuu zaidi.

**SPIKA:** Mheshimiwa Samwel Hhayuma, swali la nyongeza.

**MHE ENG. SAMWELI X. HHAYUMA:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Pamoja na majibu mazuri ya Serikali nina maswali madogo mawili ya nyongeza.

Swali la kwanza, mbegu za kisasa tunazozitumia unaweza kuzitumia mara moja tu na ni bei ghali. Je, Serikali ina mkakati gani wa kuendeleza mbegu zetu za asili ambazo unaweza kuzitumia zaidi ya mara moja ili kupunguza gharama kwa wakulima?

Swali la pili, mwaka 2020 Wizara ya Kilimo ilikuja Jimboni Hanang' na baadaye wakanunua ngano, tukielezwa kwamba zile ngano zilizoko Hanang' ni bora na zinafaa kuwa mbegu. Je, Serikali ina kauli gani juu ya upatikanaji wa mbegu bora za ngano Nchini? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu maswali mawili ya Mheshimiwa Mbunge, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kuhusu swali la kwanza mbegu za asili, mbegu hizi zimeendelea kutambuliwa na Taasisi ya Utafiti ya Kilimo Tanzania *(TARI)* inaendelea kuzifanyia utafiti, vilevile Mamlaka ya Afya, Mimea na Viuatilifu Nchini *(TPHPA)* na yenyewe sasa iko mbioni kwa ajili ya kutunga Sheria ya Nasaba za Mimea ili kuzitambua, kuzitunza na kuzitumia kwenye utafiti. Kwa hiyo, Serikali inaipa umuhimu suala hili la mbegu za asili.

Mheshimiwa Spika, swali la pili, ni kweli mwaka 2020 tulifanya utafiti huo na tulichukua sampuli ya mbegu 22, tano zikiwa kutoka nje ya nchi na 17 za ndani ya nchi, kwa ajili ya kwenda kuangalia ubora wake. Katika tafiti hii zaidi ya mbegu 10 zimeonekana zinafanya vizuri na zina kiwango kikubwa cha *gluten* kwa maana ya *protein* ambayo inazidi asilimia 10, hivi sasa zimeanza kusambazwa katika baadhi ya maeneo kuweza kutumika ili kusaidia upatikanaji wa mbegu bora za ngano.

Mheshimiwa Spika, katika mbegu hizi ziko mbegu za Kariege, Sasambua, Sifa, Chiriku pamoja na mbegu nyingine ya Mbayuwayu ambayo imeonekana kuwa na soko kubwa sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Condester Sichalwe, swali la nyongeza kwa kifupi.

**MHE. CONDESTER M. SICHALWE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi.

Je, Wizara ya Kilimo inaonaje ikitumia muda huu kufungua dirisha la kuwakopesha wakulima mbegu, mbolea, viuatilifu na vitendea kazi vingine ili kujiandaa na msimu wa kilimo ambao unakuja? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, hivi sasa Wizara ya Kilimo kupitia Wakala wa Mbegu tupo katika utaratibu wa kuanza kusambaza mbegu kwa msimu unaokuja, kwa kufungua madirisha kupitia hayo maeneo tofauti tofauti. Vilevile tunao Mfuko wetu wa pembejeo ambao nao ni mahsusi kwa ajili ya kuwasaidia wakulima kuweza kupata pembejeo hizi kwa wakati na kwa bei nafuu. Hivyo nitumie fursa hii kuwaomba wakulima wote nchini Tanzania kutumia madirisha haya mawili kwa ajili ya kuweza kupata pembejeo hizi kwa wakati ili wakati wa msimu wawe tayari wanazo na kuanza kutumia kwa ajili ya kilimo.

**SPIKA:** Mheshimiwa Ndaisaba George Ruhoro, swali la nyongeza.

**MHE. NDAISABA G. RUHORO:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Ninaomba kumuuliza Mheshimiwa Naibu Waziri kwamba ni kwa nini Serikali wanaendelea kufanya utafiti wa mbegu za asili ambazo zimetukuza wote mpaka hapa tulipo badala ya kuzalisha kwa wingi na kuzisambaza? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, katika majibu yangu nimezungumza kwamba tayari Mamlaka ya Afya ya Mimea na Viuatilifu pale Arusha wanayo benki na wanaendelea kuzitunza mbegu hizi kwa ajili ya usambazi. Kwa hiyo, zoezi la usambazi na kwenye kilimo utafiti haukomi vitakwenda sambamba lakini mwisho wa siku ni kuhakikisha kwamba mbegu hizi zinawafikiwa wakulima kwa wakati. Kwa hiyo, mamlaka inafanya kazi hiyo vilevile utafiti hauwezi kukoma kwa sababu ni kila siku mambo mapya yanajitokeza.

**SPIKA:** Mheshimiwa Cecil Mwambe, swali la nyongeza.

**MHE. CECIL D. MWAMBE:** Mheshimiwa Spika, ninashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Wizara ya Kilimo iliahidi kupeleka mbegu bora za soya kwenye vijiji vingi vilivyopo Jimbo la Ndanda ikiwemo Kijiji cha Mumburu kwa sababu soya ilikuwa inalimwa hapo zamani, ni mwaka wa tatu sasa mbegu hiyo haijaenda.

Je, ni lini Serikali itatimiza ahadi yake ya kupeleka mbegu kwenye maeneo hayo?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Spika, nimesikiliza hoja ya Mheshimiwa Mbunge nimeichukua tutakwenda kuifanyia kazi ili wakulima wake waweze kupata mbegu za soya. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge. *Microphone* ya hapo mbele izimwe.

Waheshimiwa Wabunge, tumefika mwisho wa kipindi chetu cha maswali kutoka kwenu na majibu kutoka upande wa Serikali. Sasa nilete matangazo niliyonayo hapa mbele na tutaanza na tangazo la wageni, tutaanza na wageni walioko Jukwaa la Spika.

Kwanza ni wageni wa Mheshimiwa Innocent Lugha Bashungwa, Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa; yupo Dkt. Faraji Kasidi Mnyepe ambaye ni Katibu Mkuu Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, karibu sana. *(Makofi)*

Yupo pia Jenerali Jacob John Mkunda ambaye ni Mkuu wa Majeshi ya Ulinzi, karibu sana. *(Makofi)*

Yupo pia Luteni Jenerali Salum Haji Othman - Mnadhimu Mkuu wa Jeshi, karibu sana. *(Makofi)*

Yuko pia Meja Jenerali Rajab Nduku Mabele ambaye ni Mkuu wa Jeshi la Kujenga Taifa, karibu sana. *(Makofi)*

Yuko pia Meja Jenerali Paul Kisesa Simuli aliyekuwa Mkuu wa Utumishi Jeshini ambaye kwa sasa ni Balozi Mteule, karibu sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, yupo pia Meja Jenerali Fadhiri Omary Nondo, Mkuu wa Kamandi ya Jeshi la Nchi Kavu, karibu sana. *(Makofi)*

Yupo pia Meja Jenerali Shaban Baraghashi Mani ambaye ni Mkuu wa Kamandi ya Jeshi la Anga, karibu sana. *(Makofi)*

Yupo pia Meja Jenerali Iddi Saidi Nkambi, Mkuu wa Kamandi Chini ya Makao Makuu ya Jeshi, karibu sana. *(Makofi)*

Yupo pia Ndugu Obedi Loyouni Sayore, Kamishna wa Sera na Mipango Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, karibu sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, sasa hapa sijajua itifaki nani anafuata, lakini wacha nimalize wastaafu maana kuna wengine hapa nimeletewa orodha ya ziada, kwa hiyo, mtatuwia radhi kama tutakuwa tumesoma kwa kufuata utaratibu wetu huku ndani. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunao Wakuu wa Majeshi ya Ulinzi wastaafu, yupo Jenerali Robert Phillemon Mboma ambaye ni Mkuu wa Majeshi wa Tano, huyu alikuwa Mkuu wa Majeshi kuanzia 1994 mpaka 2001, karibu sana mzee wetu. *(Makofi)*

Yupo pia Jenerali George Marwa Waitara Mkuu wa Majeshi wa Sita, huyu ni 2001 mpaka 2007. *(Makofi)*

Yupo pia Jenerali Davis Adolf Mwamunyange, Mkuu wa Majeshi wa Saba, yeye alikuwa Mkuu wa Majeshi kuanzia mwaka 2007 mpaka 2017. *(Makofi)*

Yupo pia Jenerali Venance Salvatory Mabeyo, Mkuu wa Majeshi wa Nane, huyu alikuwa Mkuu wa Majeshi kuanzia 2017 mpaka 2022. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, sasa kwa kusoma hapa, nadhani wanafuata Majenerali hawa wengine, haya wapo wageni wengine ambao nao wapo Jukwaa la Spika; tunaye Meja Jenerali Francis Mbindi ambaye ni Jaji Wakili Mkuu, karibu sana. *(Makofi)*

Yupo Meja Jenerali Amri Mwani ambaye ni Mkuu wa Tiba Jeshini, karibu sana. *(Makofi)*

Yupo pia Meja Jenerali Chelestino Msola, Mkuu wa Tawi la Mipango na Maendeleo, karibu sana. *(Makofi)*

Yupo pia Brigedia Jenerali Godfrey Nyoni, Mdhibiti Mkuu wa Jeshi, karibu sana. *(Makofi/Kicheko)*

Waheshimiwa Wabunge, wapo Majenerali Wanawake ambao naona wamewekwa pekee yao, Mheshimiwa Innocent Bashungwa ameamua hawa watangazwe kiaina, sawa.

Yupo Meja Jenerali Hawa Issa Kodi ambaye ni Mkuu wa Tawi la Lojistiki na Uhandisi Makao Makuu ya Jeshi, karibu sana. *(Makofi)*

Yupo pia Brigedia Jenerali Pili Mohamed Kambenga ambaye ni Mkuu wa Kikosi cha Utawala Kambi ya Twalipo Mgulani, karibu sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, yuko pia Brigedia Jenerali Anna Jonas Mkinga ambaye ni Mkurugenzi wa Uhakiki Mali Makao Makuu ya Jeshi, karibu sana. *(Makofi)*

Yupo pia Brigedia Jenerali Agatha Marry Katua, Mkuu wa Kikosi Lugalo Hospitali, karibu sana. *(Makofi)*

Yupo pia Brigedia Jenerali Anchira Kagombola ambaye ni Afisa Mahusiano masuala ya ulinzi katika Jumuiya ya Afrika Mashariki, karibu sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, hao nadhani waliwekwa peke yao ili ukiangalia kule juu ukiziona tu zile kofia ujue na wao wapo. Wako Wenyeviti wa Bodi za Taasisi chini ya Wizara.

Kwanza ni Luteni Jenerali Mstaafu Samuel Ndomba ambaye ni Mwenyekiti wa Bodi ya Shirika la Mzinga, karibu sana. *(Makofi)*

Yupo pia Luteni Jenerali Mstaafu Wynjones Kisamba ambaye ni Mwenyekiti wa Bodi ya Shirika la *TATC* – NYUMBU, karibu sana. *(Makofi)*

Yupo pia Meja Jenerali Mstaafu Farah Mohamedi ambaye ni Mwenyekiti wa Bodi ya SUMA JKT, karibu sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, wapo wageni wengine wa Mheshimiwa Innocent Bashungwa, wa kwanza ni Mjumbe wa Halmashauri Kuu ya Chama cha Mapinduzi Taifa, Mheshimiwa Hamoud Abuu Juma, karibu sana. *(Makofi)*

Wapo pia viongozi wa Chama cha Mapinduzi wakiongozwa na Katibu wa CCM Mkoa wa Kagera Ndugu Christopher Pallangyo. Sijui wamekaa upande gani, ama inawezekana hawajapata nafasi watakapopata nafasi ya kuingia basi mtakuwa mmetambua kwamba wapo. *(Makofi)*

Wapo pia viongozi wa TUGHE Tawi la Ulinzi wakiongozwa na Mwenyekiti wa TUGHE Tawi la Ulinzi Ndugu Markus Nyanda, karibuni sana. *(Makofi)*

Wapo pia viongozi wa Halmashauri ya Wilaya ya Karagwe wakiongozwa na Mwenyekiti wa Halmashauri hiyo Mheshimiwa Wallace Mashada. Haya hawa nao nadhani watapata nafasi ya kuingia baada ya wageni wengine kwamba wameshatangazwa.

Waheshimiwa Wabunge, wapo wageni wengine sasa sijui kama hawa ndiyo wamepata nafasi ama vipi; wawakilishi 15 wa Timu ya Mpira wa Miguu ya JKT Tanzania ambao ni wachezaji na viongozi wa Timu ya JKT Tanzania wakiongozwa na *Captain* Gwasabu Ekingo ambaye ni Mwenyekiti wa timu, karibuni sana, karibuni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, hilo kombe walilobeba hapo wao ni mabingwa wa Ligi Daraja la Kwanza ambao wamefanikiwa kupanda Ligi Kuu ya Tanzania Bara kwa msimu wa 2023/2024. Hongereni sana na tunawatakia kila la kheri. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, wapo pia wawakilishi 15 wa Timu ya *JKT Queens* ambao ni wachezaji na viongozi wa Timu ya *JKT Queens* wakiongozwa na Meja Eveline Ryoba ambaye ni Mwenyekiti wa timu. Karibuni sana, karibuni sana. Hawa nao naona hawajashika kombe pale lakini na hawa nao ni mabingwa wapya wa Ligi Kuu ya Wanawake. Ahaa, lipo nalo liko kule haya. Hawa nao ni mabingwa wapya wa Ligi Kuu ya Wanawake Tanzania, hongereni sana. Ahsante sana, haya naona Yanga wanataka kusema ligi ya wanaume hapa. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, Sajini Taji Selemani Kidunda ambaye ametwaa Ubingwa wa *World Boxing Federation in Africa.* Ahsante sana, jamani mnaonyeshwa mkanda ule alioshinda, ahsante sana, shukrani. *(Makofi)*

Pia yupo Sajini Alphonce Simbu aliyepata medali ya shaba katika mbio za *Osaka Marathon* na *Yangzhou Jianzhen International Half Marathon,* ahsante sana. *(Makofi)*

Yupo pia *Private* Kassim Mbudikwe na *Private* Yusuph Changarawe, hawa wamepata medali za shaba kila mmoja katika Mashindano ya Ngumi ya Jumuiya ya Madola. Wameshikilia na medali zao pale, tunawashukuru sana kwa kuliwakilisha Taifa letu vizuri na kulipa heshima Jeshi letu, karibuni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, sasa tunaanza wageni wetu sisi wengine maana hao ni wageni mahususi. Haya, wageni wetu sisi Wabunge tutaanza na wageni nane wa Mheshimiwa Exaud Kigahe, Naibu Waziri wa Uwekezaji, Viwanda na Biashara. Hawa ni viongozi wa Chama cha Mapinduzi Kata kutoka Jimbo la Mufindi Kaskazini Mkoa wa Iringa, karibuni sana. *(Makofi)*

Wapo pia wageni 40 wa Mheshimiwa Iddi Kassim Iddi, viongozi wa UVCCM kutoka Msalala Mkoa wa Shinyanga, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunaye pia mgeni wa Mheshimiwa Jackson Kiswaga, Mkurugenzi wa Hospitali ya Tosamaganga kutoka Kalenga Mkoa wa Iringa, karibu sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, wapo wageni 23 wa Mheshimiwa Michael Kembaki ambao ni viongozi wa Chama na Madiwani kutoka Tarime Mjini Mkoa wa Mara, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao wageni watatau wa Mheshimiwa Daniel Awack kutoka Karatu Mkoa wa Arusha, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao wageni wawili wa Mheshimiwa Omar Ali Omar kutoka Taasisi ya Wanawake Jijini Dodoma, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunaye mgeni wa Mheshimiwa Rashid Shangazi ambaye ni Mwenyekiti wa CCM kutoka Lushoto Mkoa wa Tanga, karibu sana. *(Makofi)*

Tunaye mgeni wa Mheshimiwa Joseph Tadayo kutoka Mkoa wa Kilimanjaro, karibu sana. *(Makofi)*

Tunaye mgeni wa Mheshimiwa Oran Njeza ambaye ni kiongozi wa *St. John's University Dodoma,* karibu sana. *(Makofi)*

Tunao wageni 10 wa Mheshimiwa Luhaga Mpina ambao ni Kampuni ya *Mkambuya Environmental Limited* kutoka Jijini Dodoma, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunaye mgeni wa Mheshimiwa Wanu Ameir ambaye ni Mwakilishi wa Taasisi ya Elimu kwa Vijana Tanzania, karibu sana. *(Makofi)*

Tunao wageni waliotembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo. Wanafunzi 100 na walimu 15 kutoka Shule ya Msingi ya Kiwanja cha Ndege iliyopo Mkoani Morogoro, karibuni sana, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao wanafunzi 60 na walimu 10 kutoka Shule ya *Good Victory* ya Mkoa wa Iringa, karibuni sana sana sana Bungeni. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, hao ndiyo wageni tulionao. Matangazo mawili, tangazo la kwanza linatoka kwa Mwenyekiti ama *Captain* wa mpira wa wavu; mnatangaziwa kwamba leo katika Viwanja vya Chinangali kutakuwa na michezo kuanzia saa 10 jioni, mpira wa wavu wanawake, mpira wa wavu wanaume, kutakuwa na mashindano ambayo yatakuwa yanaendelea hapo kati ya Bunge wanawake, Bunge wanaume na Chama cha Mpira wa Wavu Dodoma *(DOREVA).* Haya mnakaribishwa sana kushiriki katika michezo hii, na Mgeni Rasmi atakuwa Mwenyekiti wa Mpira wa Wavu Tanzania. Kwa hiyo Mheshimiwa Cecil Mwambe anawakaribisha sana.

Waheshimiwa Wabunge, tangazo lingine linatoka kwa Katibu wa Bunge. Mnatangaziwa kwamba Wizara ya Nishati itaendesha semina kuhusu maendeleo ya Uwekezaji wa Mradi wa Bomba la Mafuta Ghafi la Afrika Mashariki *(East African Crude Oil Pipeline – EACOP)*. Semina hii itafanyika kesho siku ya Alhamis tarehe 25 Mei,

2023 mara baada ya kusitisha shughuli za Bunge saa saba mchana katika Ukumbi wa Pius Msekwa. Waheshimiwa Wabunge wote mnakaribishwa kuhudhuria semina hii ambayo itawaeleza kuhusu maendeleo ya utekelezaji wa mradi huu wa kimkakati ambao unagusa sekta za nishati, biashara, viwanda, uwekezaji, mazingira, usafirishaji, uwezeshaji wananchi kiuchumi, elimu, afya na kijamii. Kwa hiyo mnaombwa msikose kwenye semina hiyo muhimu.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya matangazo hayo tunaedelea na ratiba iliyo mbele yetu. Katibu.

**NDG. RUTH MAKUNGU – KATIBU MEZANI:**

## HOJA ZA SERIKALI

### Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, ni mwite sasa Mheshimiwa Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa Mheshimiwa Innocent Lugha Bashungwa aje awasilishe hoja yake. *(Makofi)*

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:** Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu likubali kupokea na kujadili taarifa ya utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023 kwa Fungu 57 Wizara, Fungu 38 Ngome na Fungu 39 JKT pamoja na kupitisha Mpango na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024.

Mheshimiwa Spika, napenda nitumie fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujalia uzima na afya njema na kuendelea kuijalia nchi yetu amani na utulivu. Kwa heshima na unyenyekevu mkubwa namshukuru Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Amiri Jeshi Mkuu kwa kuniamini na kuniteua kuiongoza Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga

Taifa. Ninakuahidi Mheshimiwa Rais na Amiri Jeshi Mkuu kamwe sitakuangusha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais na Amiri Jeshi Mkuu kwa juhudi zake za dhati katika kuhakikisha Taifa letu linaendelea kuwa na umoja, amani, utulivu, ustawi na kasi ya maendeleo ya kiuchumi. Mafanikio makubwa haya yanastahili pongezi. Hongera sana Mheshimiwa Rais na Amiri Jeshi Mkuu Dkt. Samia Suluhu Hassan. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia napenda kuwapongeza Makamu wa Rais Mheshimiwa Dkt. Philip Isdori Mpango, Mheshimiwa Dkt. Husssein Ally Mwinyi Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi na Mheshimiwa Waziri Mkuu Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb) kwa uongozi na utendaji wao makini. Ninawashukuru kwa maelekezo wanayonipatia katika kufanikisha utekelezaji wa majukumu ya Wizara.

Mheshimiwa Spika, naomba kutumia fursa hii kukupongeza wewe binafsi, Mheshimiwa Dkt. Tulia Ackson Mwansasu (Mb) kwa kuliongoza Bunge kwa weledi na viwango vya hali ya juu. Vile vile nampongeza Mheshimiwa Mussa Azan Zungu (Mb), Naibu Spika pamoja na Waheshimiwa Wenyeviti wa Bunge kwa kazi nzuri ya kukusaidia vizuri sana katika kuliongoza Bunge. Aidha nawapongeza Katibu wa Bunge Bi. Nenelwa Mwihambi, *ndc,* na watumishi wa Bunge kwa namna wanavyoendelea kukusaidia katika utekelezaji wa Shughuli za Bunge. Pia ninawashukuru Mawaziri wenzangu na Naibu Mawaziri kwa ushirikiano wanaonipatia katika kuiongoza Wizara hii.

Mheshimiwa Spika, naomba kumpongeza Jenerali Jacob John Mkunda kwa kupandishwa cheo na kuteuliwa kuwa Mkuu wa Majeshi ya Ulinzi. Vile vile nampongeza Luteni Jenerali Salum Haji Othman kwa kupandishwa cheo na kuteuliwa kuwa Mnadhimu Mkuu wa Jeshi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninaishukuru Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama inayoongozwa na Mheshimiwa Vita Rashid Kawawa (Mb) na akisaidiwa na Makamu Mwenyekiti Mheshimiwa Vincent Paul Mbogo (Mb) pamoja na Wajumbe wa Kamati bila kusahau Sekretariet ya Kamati kwa ushirikiano na ushauri kwa Wizara. Wakati wote Kamati hii imekuwa mstari wa mbele katika kutoa ushauri na mapendekezo kwa Serikali. Wizara imezingatia ushauri na mapendekezo mliyotupa. Ahsanteni sana Kamati ya NUU. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninawashukuru pia ninyi Waheshimiwa Wabunge wenzangu kwa ushirikiano mnaonipa ili niweze kutekeleza majukumu aliyonikasimisha Mheshimiwa Rais na Amiri Jeshi Mkuu. Ahsanteni sana Waheshimiwa Wabunge wenzangu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa namna ya kipekee naomba kuwashukuru Wananchi wa Jimbo la Karagwe kwa ushirikiano wanaonipatia. Ni matumaini yangu kuwa tutaendelea kushirikiana kwa manufaa ya Karagwe yetu. Napenda kuishukuru familia yangu, Mke wangu Jenifa Bashungwa na watoto wangu Santo, Solana, Sankara na Samora kwa upendo na uvumilivu wao unaoniwezesha kutekeleza majukumu yangu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, natoa pongezi kwa Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi ikiongozwa na pacha wangu Mheshimiwa *Engineer* Hamad Yussuf Masauni, na vyombo vingine vya usalama kwa kufanikisha kukamatwa na kurejeshwa kwa mhalifu aliyetoroka katika gereza Nchini Afrika Kusini. Mara tu alipoingia nchini kwetu alikamatwa mhalifu huyu. Natoa pongezi kwa vyombo hivi kwa namna vinavyoshirikiana nasi kukabiliana na matishio mbalimbali na kuhakikisha nchi yetu inaendelea kuwa na amani na utulivu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nichukue fursa hii kutoa rai kwa Watanzania kuendelea kutoa ushirikiano kwa vyombo vya ulinzi na usalama katika kuimarisha ulinzi na usalama wa nchi yetu. Naomba kuipongeza JKT kwa kutimiza miaka 60 tangu kuanzishwa kwake. JKT

ilianzishwa rasmi mwezi Julai, 1963 na imeendelea kuwaandaa vijana kwa kuwapatia mafunzo ya ukakamavu, stadi za kazi, kuwajengea uzalendo na umoja wa kitaifa. Mwezi Julai mwaka huu wa 2023 tunatarajia kufanya maazimisho ya kutimiza miaka 60 katika Uwanja wa Jamhuri hapa Jijini Dodoma. Waheshimiwa Wabunge na wananchi wote mnakaribishwa kuhudhuria katika maazimisho hayo ambayo Mgeni Rasmi atakuwa Mheshimiwa Rais na Amiri Jeshi Mkuu Dkt. Samia Suluhu Hassan. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwenye majeshi pia tupo mstari wa mbele kwenye maendeleo ya michezo kwa vijana nchini. Nikushukuru kwa utambulisho kwa timu zetu kama ulivyozitambulisha, lakini napenda nitumie fursa hii kuwapongeza Sajini Taji Selemani Kidunda aliyetwaa Ubingwa wa *World Boxing Federation in Africa,* Sajini Alphonce Felix Simbu aliyepata medali ya shaba katika mbio za *Osaka Marathon* na *Yangzhou Jianzhen International Half Marathon, Private* Kassim Mbudikwe na *Private* Yusuph Changarawe waliopata medali ya shaba kila mmoja katika mashindano ya Jumuiya ya Madola. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ushiriki wa majeshi yetu kwenye michezo ngazi ya kimataifa umewezesha Jeshi la Wananchi Tanzania kuimarisha mahusiano na ushirikiano kati yake na nchi rafiki na vyombo vya usalama. Aidha, kupitia shughuli za Baraza la Michezo ya Majeshi Duniani, Jeshi la Wananchi Tanzania limeweza kujenga uhusiano baina yake na Jeshi la Nchi ya Ujerumani ambapo Jeshi hilo limetupatia wakufunzi wa michezo ya mpira wa wavu, mpira wa kikapu na ngumi.

Mheshimiwa Spika, timu ya mpira wa miguu ya *JKT Queens,* kama ulivyoitambulisha, imealikwa kushiriki katika mashindano ya *World Military Women Football Championship* yatakayofanyika kuanzia tarehe 27 mwaka huu Juni hadi tarehe 9 Julai, 2023 Nchini Uholanzi. Kutoka Afrika, nchi zitakazoshiriki ni tatu tu na sisi tumo na tunawakilishwa vyema na *JKT Queens.* Nchi hizi ni Tanzania, Cameroon na Nigeria. Tanzania itakuwa katika kundi moja na nchi za Ufaransa ambaye ni bingwa mtetezi, Korea Kusini na Canada.

Sasa washabiki wa Yanga na Simba na vilabu vyote na Watanzania tushangilie na kuunga mkono *JKT Queens* kwa sababu ndiyo inayokwenda kutuwakilisha kimataifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, timu za jeshi zimeshiriki katika mashindano yanayoandaliwa na *TFF* ambapo timu ya *JKT Queens* imefanikiwa kutwaa ubingwa wa Ligi Kuu ya Wanawake Tanzania kama walivyotuonyesha kombe lao. Vile vile JKT Tanzania ilishiriki Ligi Daraja la Kwanza na imefanikiwa kupanda daraja msimu wa ligi wa 2023/2024 itashiriki Ligi Kuu ya Tanzania Bara *(NBC Premier League)*. Nazipongeza timu hizi kwa mafanikio haya makubwa, ahsanteni sana kwa kutuheshimisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Wizara imeendelea kushirikiana na Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo katika kuibua vipaji na kuviendeleza kwa lengo la kuinua kiwango cha michezo nchini kama alivyotuagiza Mheshimiwa Rais na Amiri Jeshi Mkuu Dkt. Samia Suluhu Hassan kwamba Baraza la Michezo Tanzania na Baraza la Michezo ya Majeshi Tanzania (BAMATA) washirikiane kimkakati kuibua vipaji kwenye michezo na sanaa.

Mheshimiwa Spika, kwa mwaka wa fedha 2022/2023, hali ya ulinzi na usalama wa mipaka ya nchi yetu yenye urefu wa kilomita 5,461.20, ambayo inahusisha eneo la nchi kavu na eneo la maji, kwa ujumla imeendelea kuwa shwari. Katika mipaka hiyo, licha ya uwepo wa changamoto kadhaa, hapakuwa na matukio ya uhasama baina yetu na nchi tunazopakana nazo.

Mheshimiwa Spika, hali ya ulinzi na usalama wa mipaka ya nchi yetu na nchi tunazopakana nazo imeelezwa kwa kina kuanzia aya ya 12 hadi aya ya 23 ya hotuba yangu.

Mheshimiwa Spika, Kamati ya NUU ilipitia na kujadili utekelezaji wa mpango na bajeti ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023 na kutoa maoni ushauri na maelekezo yaliyolenga kuboresha utendaji kazi kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024. Napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa maoni, ushauri na maelekezo ya Kamati

yamefanyiwa kazi na kuzingatiwa wakati wa kuandaa na kukamilisha mpango na bajeti ya Mwaka wa Fedha 2023/2024 ninayowasilisha leo hapa Bungeni.

Mheshimiwa Spika, katika Bajeti ya Mwaka wa Fedha 2022/2023, Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa iliidhinishiwa jumla ya shilingi trilioni 2.714 kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na Maendeleo katika Mafungu yake matatu: Fungu 38 - Ngome, Fungu 39 - JKT na Fungu 57 - Wizara. Kati ya fedha hizo, shilingi trilioni 2.483 ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na shilingi bilioni 230.33 ni kwa ajili ya Matumizi ya Maendeleo. Muhtasari wa Mchanganuo umeoneshwa katika Jedwali Na.2.

Mheshimiwa Spika, Fungu 38 limepokea fedha za Matumizi ya Kawaida Shilingi Trilioni 1.749 na Fedha za Maendeleo shilingi bilioni 26.364; Fungu 39 limepokea fedha za Matumizi ya Kawaida shilingi bilioni 365.519 na Fedha za Maendeleo shilingi bilioni 7.0; na Fungu 57 limepokea fedha za Matumizi ya Kawaida shilingi bilioni 17.013 na Fedha za Maendeleo shilingi bilioni 82.8. Mchanganuo umeoneshwa katika Jedwali Na.3.

Mheshimiwa Spika, shughuli zilizotekelezwa na Wizara kwa fedha za matumizi ya kawaida zimeelezwa kwa kina katika hotuba yangu kuanzia aya ya 34 hadi ya 63.

Mheshimiwa Spika, Fungu 57 katika Mwaka wa Fedha 2022/2023, liliidhinishiwa kiasi cha Shilingi Bilioni 160 kwa ajili ya kugharamia Shughuli za Maendeleo. Hadi kufikia mwezi Aprili 2023, kiasi cha shilingi bilioni 82.8 kimepokelewa, sawa na asilimia 51.75 ya Bajeti iliyoidhinishwa. Fedha zilizopokelewa zimetumika kugharamia ununuzi na matengenezo ya zana na vifaa mbalimbali vya kijeshi.

Mheshimiwa Spika, kuhusu migogoro ya ardhi; Wizara inatambua changamoto zilizopo kwenye maeneo yanayomilikiwa na Jeshi la Wananchi Tanzania. Kwa muda mrefu kumekuwepo na migogoro ya ardhi baina ya jeshi na raia. Kutokana na migogoro hiyo Wizara inatekeleza mpango wa kuhakikisha maeneo yote ya

jeshi yanapimwa na kupatiwa hati miliki na hivyo kuondoa migogoro iliyopo. Hadi sasa, mpango huo umetekelezwa kwa asilimia 71.48 kwa kuhakiki, kupima na kufanya uthamini wa maeneo mbalimbali ya Jeshi nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2022/2023, kati ya fedha zilizopokelewa kwa ajili ya kugharamia shughuli za maendeleo tumetumia shilingi bilioni 13.427 kulipa fidia ya ardhi katika maeneo mbalimbali nchini. Maeneo yaliyolipwa fidia ni pamoja na Gurungu, Mtipa, Mkiwa, Mkwese na Choda Mkoani Singida; Kisakasaka na Chukwani Mkoa wa Mjini Magharibi; Ras Nondwa Mkoani Kigoma; Itaga na Usule Mkoani Tabora; Funta Kihangaiko na Mkupuka Mkoani Pwani; Bulifani Misenyi Mkoani Kagera na Machenje Kongwa Mkoani Dodoma.

Mheshimiwa Spika, Jeshi la Wananchi Tanzania linahitaji maeneo makubwa ya ardhi kwa ajili ya kutekeleza majukumu yake ya msingi ya ulinzi wa Taifa letu. Wananchi watambue kuwa maeneo ya jeshi ni muhimu kwa ajili ya mafunzo na mazoezi ya utayari wa kivita.

Mheshimiwa Spika, wananchi wetu wasiyaone kwa kupima kwa macho na kusema maeneo ya jeshi ni makubwa. Kwenye taaluma ya jeshi uhalisia ni kwamba wanahitaji maeneo makubwa ili mazoezi ya kivita wanayoyafanya yaweze kufanyika bila kuleta madhara kwa wananchi wetu. Kwa hiyo, naomba Waheshimiwa Wabunge pamoja na wananchi tuheshimu maeneo ya jeshi, tuache uvamizi.

Mheshimiwa Spika, JKT imeendelea kutekeleza Mkakati wa Kilimo (2019/2020 - 2024/2025) ambao unalenga kuongeza uzalishaji wa mazao na kujitosheleza kwa chakula ili kuipunguzia Serikali gharama za kulisha vijana wanaohudhuria mafunzo ya JKT na kuiwezesha nchi yetu kuwa na akiba ya chakula.

Mheshimiwa Spika, kuwezesha mkakati huo kutekelezwa ipasavyo, JKT imeendelea kushirikiana na Wizara ya Kilimo kupitia

Mkataba wa Makubaliano *(MoU)* katika maeneo ya teknolojia za kilimo, utafiti wa kilimo, uzalishaji wa mazao ya kimkakati na uzalishaji wa mbegu za chikichi, kahawa, mahindi, mpunga na alizeti. Utekelezaji wa Mkataba huo, umewezesha JKT kuongeza uzalishaji wa mazao husika. Naishukuru Wizara ya Kilimo inayoongozwa na Ndugu yangu Mheshimiwa Hussein Bashe kwa ushirikiano huo wa kimkakati unaolenga kuchangia uzalishaji wa ajira milioni nane zilizolengwa kwenye Ilani ya Chama cha Mapinduzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vilevile, Jeshi la Kujenga Taifa lipo katika hatua za kuingia makubaliano na Wizara ya Mifugo na Uvuvi ili kuwezesha vijana wa JKT kupata mafunzo kwa vitendo kupitia Vituo Atamizi vilivyoanzishwa na Wizara ya Mifugo na Uvuvi katika sehemu mbalimbali nchini. Nawashukuru Mawaziri, nishamshukuru Mheshimiwa Kaka yangu Hussein Bashe pia nimshukuru Mheshimiwa Abdallah Ulega, Waziri wa Mifugo na Uvivu kwa kukubali tushirikiane na kujipanga kimkakati kupitia JKT katika kutekeleza maagizo ya Mheshimiwa Rais na Amiri Jeshi Mkuu kwenye kupanua wigo wa Sekta ya Kilimo, Mifugo na uchumi wa *blue* ili kuzalisha ajira nyingi za vijana nchini. Kupitia JKT tupo tayari kwenda kwa mapana na marefu kwa kushirkiana na Wizara hizi za uzalishaji bila kusahau sekta ya viwanda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda kutumia fursa hii kuliarifu Bunge lako Tukufu pamoja na umma wa Watanzania kwamba dhumuni la mafunzo yanayotolewa kwa vijana ni kuwapatia ukakamavu, stadi za kazi, kuwajengea uzalendo na umoja wa kitaifa ili baada ya kumaliza muda wa mafunzo na kutumikia JKT waweze kurejea majumbani kwao wakiwa raia wema wazalendo na wenye uwezo wa kujitegemea na kulilinda Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, ninukuu maneno ya Hayati Mwalimu Julius Kambarage Nyerere wakati akizindua mafunzo ya Jeshi la Kujenga Taifa mwaka 1963 katika Kambi ya Mgulani JKT kule Dar es Salaam alisema hivi "umuhimu wa JKT unatokana na Taifa kuhitaji vijana na vijana kuitikia wito huo wa kulitumikia Taifa lao kwa jukumu lolote. Nitoe rai kwa vijana wote wanaopata fursa za kupata mafunzo hayo

kuzitumia stadi za kazi na maisha walizozipata kujiajiri na kujitegemea."

Mheshimiwa Spika, nitumie fursa hii kuwasisitiza wananchi kuwasiliana na mamlaka husika pindi nafasi za JKT na Jeshi la Wananchi Tanzania zinapotangazwa ili kujiepusha na matapeli ambao huwadanganya watawapatia nafasi katika vyombo hivi vya ulinzi na usalama. Niwaombe wananchi vijana ambao mnafuatilia na kuomba nafasi za kutumikia majeshi yetu mfuate utaratibu na maelekezo yanayotolewa na Jeshi la Wananchi Tanzania na JKT na si vinginevyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Jeshi la Ulinzi la Wananchi Watanzania limeendelea kukua na kuimarika kizana, kinyenzo na kiteknolojia kulingana na mahitaji ya wakati. Hali hii imeliwezesha jeshi letu kutekeleza majukumu yake kwa umahiri mkubwa na kuiwezesha Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuendelea kuwa na amani na usalama. Hata pale ambapo pametokea matishio yamedhibitiwa na majeshi yetu ipasavyo na kwa wakati.

Mheshimiwa Spika, naomba kuitumia fursa kuishukuru Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan Rais na Amiri Jeshi Mkuu wa Tanzania kwa kuendelea kuzipa kipaumbele shughuli za ulinzi wa Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, Wizara kupitia Shirika la Nyumbu, Shirika la Mzinga na Suma JKT inaendelea kutekeleza majukumu kama ilivyoelezwa katika Hotuba yangu aya ya 74 hadi ya 80.

Mheshimiwa Spika, viwanda vya kijeshi, huzalisha bidhaa mbalimbali kwa ajili ya matumizi ya kijeshi na kiraia. Naomba nitoe wito kwa washirika mbalimbali wa maendeleo wakiwemo Waheshimiwa Wabunge wenzangu kushirikiana nasi katika sekta hii muhimu kwa ajili ya kukuza viwanda vyetu nchini. Pia tunawakaribisha wawekezaji kuwekeza kwenye viwanda vya kijeshi ili kuwezesha uzalishaji wa dhana na vifaa vya kijeshi na hivyo kuipunguzia Serikali gharama za kuagiza kutoka nje ya nchi.

Mheshimiwa Spika, Wizara katika hatua za mwisho za kuangalia eneo maalum kwa ajili ya uwekezaji wa mambo ya kijeshi na dhana kwa ajili ya matumizi ya jeshi na matumizi ya kiraia. Lipo eneo la Singida tunalitathmini kuona kama linaweza likawa ni *exclusive zone* kwa ajili ya uwekezaji mahiri kwenye *defence industry*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba uniruhusu kuwasilisha mpango na makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kwa mwaka wa fedha 2023/2024, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, makusanyo ya maduhuli ni kama inavyoonekana katika jedwali Na.4.

Mheshimiwa Spika, Matumizi ya Kawaida na Maendeleo, katika mwaka wa fedha 2023/2024, Serikali inatarajia kutenga fedha kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na Maendeleo ikiwa na jumla ya shilingi 2,989,967,122,000.00 ambapo kati ya fedha hizo, shilingi 2,767,133,951,000.00 ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida, na shilingi 222,833,171,000.00 ni kwa ajili ya kugharamia shughuli za maendeleo. Mchanganuo kwa kila Fungu ni kama ilivyoainishwa katika jedwali Na.5.

Mheshimiwa Spika, shughuli zinazokusudiwa kutekelezwa katika mwaka wa fedha wa 2023/2024 zimeainishwa katika aya ya 85.

Mheshimiwa Spika, shukrani, naomba nitumie fursa hii kuwashukuru wale wote wanaonisaidia kuhakikisha dira ya Wizara inafikiwa. Nimeshashukuru Waheshimiwa Wabunge, nimekushukuru Mheshimiwa Spika, niishukuru Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama. Kipekee niwashukuru Wizara, watumishi wenzangu nikianza na Dkt. Faraji Kasidi Mnyepe, Katibu Mkuu wa Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa; Jenerali Jacob John Mkunda, Mkuu wa Majeshi ya Ulinzi; Luteni Jenerali Salum Haji Othman, Mnadhimu Mkuu wa Jeshi; Meja Jenerali Rajabu Nduku

Mabele, Mkuu wa Jeshi la Kujenga Taifa; Wakuu wa Kamandi, Wakuu wa Mashirika, Wakuu wa Idara na Vitengo, Wakuu wa Matawi, Maafisa, Askari na Watumishi wa Umma waliopo Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa nawashukuru sana sana kwa ushirikiano wanaonipa ili tuweze kumsaidia Mheshimiwa Rais na Amiri Jeshi Mkuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kipekee katika shukrani pia niwashukuru Wakuu wa Majeshi Wastaafu kama ulivyowatambulisha kwa kazi nzuri na iliyotukuka ya kutumikia Taifa letu tunawashukuru sana. Tunaomba Mwenyezi Mungu awajalie maisha marefu waendelee kuwa msaada kwa Taifa letu na majeshi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba pia kuwashukuru wananchi wote kwa ushirikiano wanaotoa kwa Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania katika ulinzi wa nchi yetu. Ni matumaini yangu kuwa wataendelea kushirikiana na Jeshi letu katika kuhakikisha nchi yetu inaendelea kuwa na amani na usalama kwa kuwa ndiyo msingi wa maendeleo ya Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba nitoe wito kwa wananchi wote kuwa ulinzi wa Taifa letu ni jukumu la kila Mtanzania na kila mmoja wetu ana jukumu la kutekeleza wajibu huo. Wanajeshi wetu wanafanya kazi kubwa sana usiku na mchana kwa weledi, uhodari na uzalendo wa hali ya juu. Nawapongeza sana maafisa na askari popote mlipo ndani ya nchi yetu na nje ya nchi yetu kwenye ulinzi wa amani kwa moyo wa kujituma na kwa kazi kubwa wanayoifanya ya kumsaidia Mheshimiwa Rais na Amiri Jeshi Mkuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kabla sijatoa hoja, nishukuru kama unavyojua Baraza la Mawaziri linaendelea lakini nina *backup* upande wa Serikali ya kutosha kwa Waheshimiwa Manaibu Mawaziri. Nimshukuru Mheshimiwa Ridhiwani Kikwete, Naibu Waziri kwa kusimama upande wa mambo ya kisheria, pia Mheshimiwa Naibu Waziri Pinda kwa hiyo tumejiandaa.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa fursa ya kuwasilisha hotuba hii, niwashukuru Waheshimiwa Wabunge kwa kunisikiliza.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**HOTUBA YA MHESHIMIWA INNOCENT LUGHA BASHUNGWA (MB.), WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA AKIWASILISHA BUNGENI MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2023/2024 - KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

## A. UTANGULIZI

1. ***Mheshimiwa Spika,*** kutokana na taarifa iliyowasilishwa leo hapa Bungeni na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama, naomba kutoa hoja kwamba, Bunge lako Tukufu likubali kupokea na kujadili Taarifa ya Utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023 kwa Fungu 57 - Wizara, Fungu 38 – NGOME, na Fungu 39 - JKT pamoja na kupitisha Mpango na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024.

2. ***Mheshimiwa Spika,*** napenda nitumie fursa hii, kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujalia uzima na afya njema, na kuendelea kuijalia nchi yetu amani na utulivu. Kwa heshima na unyenyekevu mkubwa namshukuru **Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan**, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Amiri Jeshi Mkuu, kwa kuniamini na kuniteua kuiongoza Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa. Ninamuahidi, kamwe sitamwangusha.

3. ***Mheshimiwa Spika,*** napenda kumpongeza **Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan**, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Amiri Jeshi Mkuu, kwa juhudi zake za dhati, katika kuhakikisha Taifa letu linaendelea kuwa na umoja, amani, utulivu, ustawi na kasi ya maendeleo ya kiuchumi ambayo inastahili pongezi kubwa. Hongera sana Mhe. Rais na Amiri Jeshi Mkuu **Dkt. Samia Suluhu Hassan.**

4. ***Mheshimiwa Spika,*** pia napenda kuwapongeza **Mhe. Dkt. Philip Isdor Mpango,** Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, **Mhe. Dkt. Hussein Ali Mwinyi,** Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, na **Mhe. Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb.),** Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa uongozi na utendaji wao makini. Ninawashukuru kwa maelekezo wanayonipatia katika kufanikisha utekelezaji wa majukumu ya Wizara.

5. ***Mheshimiwa Spika,*** naomba kutumia fursa hii, kukupongeza wewe binafsi Mhe. Dkt. Tulia Ackson Mwansasu (Mb.), kwa kuliongoza Bunge kwa weledi na viwango vya hali ya juu. Vilevile, nampongeza Mhe. Mussa Azzan Zungu (Mb.), Naibu Spika, pamoja na Waheshimiwa Wenyeviti wa Bunge, kwa kazi nzuri na kukusaidia vizuri sana katika kuliongoza Bunge. Aidha, nawapongeza Katibu wa Bunge Bi. Nenelwa Mwihambi na Watumishi wa Bunge kwa namna wanavyoendelea kukusaidia katika utekelezaji wa shughuli za Bunge. Pia, nawashukuru Mawaziri wenzangu na Manaibu Mawaziri kwa ushirikiano wanaonipatia katika kuiongoza Wizara hii.

6. ***Mheshimiwa Spika,*** naomba kumpongeza **Jenerali Jacob John Mkunda** kwa kupandishwa cheo na kuteuliwa kuwa Mkuu wa Majeshi ya Ulinzi. Vilevile, nampongeza **Luteni Jenerali Salum Haji Othman,** kwa kupandishwa cheo na kuteuliwa kuwa Mnadhimu Mkuu wa Jeshi.

7. ***Mheshimiwa Spika,*** ninaishukuru Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama (NUU) inayoongozwa na **Mhe. Vita Rashid Kawawa (Mb.),** akisaidiwa na Makamu Mwenyekiti **Mhe. Vincent Paul Mbogo (Mb.),** pamoja na Wajumbe wa Kamati, bila kusahau Sekretarieti ya Kamati kwa ushirikiano, maoni na ushauri kwa Wizara. Wakati wote Kamati hii, imekuwa mstari wa mbele katika kutoa ushauri na mapendekezo kwa Serikali, juu ya umuhimu wa kuimarisha utendaji wa Vyombo vya Ulinzi na Usalama vya nchi yetu. Wizara imezingatia ushauri na mapendekezo hayo. Naishukuru sana Kamati ya NUU.

8. ***Mheshimiwa Spika,*** natoa pongezi, kwa Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi na vyombo vingine vya usalama, kwa kufanikisha kukamatwa na kurejeshwa kwa mhalifu aliyetoroka katika gereza nchini Afrika Kusini, mara tu alipoingia nchini. Vilevile, natoa pongezi kwa vyombo hivi, kwa namna vinavyoshirikiana nasi kukabiliana na matishio mbalimbali, na kuhakikisha nchi yetu inaendelea kuwa na amani na utulivu. Hivyo, nichukue fursa hii, kutoa rai kwa watanzania kuendelea kutoa ushirikiano kwa vyombo vya ulinzi na usalama, katika kuimarisha ulinzi na usalama wa nchi yetu.

9. ***Mheshimiwa Spika,*** naomba kuipongeza JKT kwa kutimiza miaka 60 tangu kuanzishwa kwake. JKT ilianzishwa rasmi mwezi Julai 1963, na imeendelea kuwaandaa vijana kwa kuwapatia mafunzo ya ukakamavu, stadi za kazi, kuwajengea uzalendo na umoja wa kitaifa. Kwa muktadha huo, Mwezi Julai mwaka huu wa 2023 tunatarajia kufanya maadhimisho ya kutimiza miaka 60, katika Uwanja wa Jamhuri hapa Jijini Dodoma. Waheshimiwa wabunge na wananchi wote mnakaribishwa kuhudhuria katika maadhimisho hayo.

10. ***Mheshimiwa Spika,*** naomba kutoa pole kwa Serikali ya Malawi kutokana na mafuriko yaliyosababishwa na kimbunga *Freddy* kilichotokea mwezi Machi 2023 na kugharimu maisha ya watu wengi. Nimpongeze **Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan**, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Amiri Jeshi Mkuu, kwa misaada ya kibinadamu aliyotoa kwa nchi hiyo. Vilevile, nimpongeze Mkuu wa Majeshi na JWTZ kwa namna walivyoshiriki kwa weledi katika zoezi la uokozi na upelekaji wa misaada ya kibinadamu nchini Malawi.

11. ***Mheshimiwa Spika,*** baada ya maelezo hayo ya utangulizi, naomba kutumia fursa hii kuwasilisha Hotuba yangu ambayo imejikita katika maeneo makuu yafuatayo: Hali ya Ulinzi na Usalama wa Mipaka ya nchi; Utekelezaji wa Maoni na Ushauri wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama; Utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi ya Mwaka 2020 na Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025 kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023;

Mapitio ya Utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Mwaka wa Fedha 2022/2023; Mpango na Mwelekeo wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024; na Shukrani kwa wadau mbalimbali wa Wizara.

## B. HALI YA ULINZI NA USALAMA WA MIPAKA YA NCHI

12. ***Mheshimiwa Spika,*** kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023, hali ya ulinzi na usalama wa mipaka ya nchi yetu yenye urefu wa kilomita **5,461.20**, ambayo inahusisha eneo la nchi kavu na eneo la maji, kwa ujumla imeendelea kuwa shwari. Kwa upande wa eneo la nchi kavu, nchi yetu inapakana na nchi za Burundi, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo, Kenya, Malawi, Msumbiji, Rwanda, Uganda na Zambia. Kwa upande wa eneo la maji, hususan Bahari ya Hindi, inapakana na nchi za Comoro na Shelisheli. Katika mipaka hiyo, licha ya uwepo wa changamoto kadhaa, hapakuwa na matukio ya uhasama baina yetu na nchi tunazopakana nazo.

13. ***Mheshimiwa Spika,*** hali ya ulinzi na usalama wa mipaka ya nchi yetu na nchi tunazopakana nazo ni ifuatavyo;

### *Mpaka wa Tanzania na Uganda*

14. ***Mheshimiwa Spika,*** hali ya usalama katika Mpaka huu ni shwari. Hakuna tukio la kuhatarisha usalama wa nchi yetu lililoripotiwa. Hata hivyo, kuna changamoto ya kutokuhakikiwa kwa Mpaka, uhamiaji haramu, na kuingia nchini kwa mifugo kutoka Uganda kwa ajili ya malisho na maji. Serikali ya Tanzania na Uganda zinaendelea kushirikiana ili kutatua changamoto hizo.

### *Mpaka wa Tanzania na Kenya*

15. ***Mheshimiwa Spika,*** hali ya usalama wa Mpaka huu ni shwari. Hakuna tukio la kuhatarisha usalama dhidi ya Tanzania lililoripotiwa. Hata hivyo, ipo changamoto ya kuharibiwa kwa Alama za Mpaka na wahamiaji haramu katika Mkoa wa Tanga ambao wanahatarisha usalama wa nchi, kwani baadhi yao hujihusisha na vitendo vya kihalifu. Changamoto nyingine ni kutotambulika kwa

Mpaka wetu na nchi ya Kenya katika eneo la Bahari ya Hindi, hasa kwa wananchi wa kawaida. Hali hiyo imechangia baadhi ya wavuvi wa Tanzania kukamatwa na Vyombo vya Ulinzi na Usalama vya Kenya kwa kosa la kuvuka Mpaka.

16. ***Mheshimiwa Spika,*** kazi ya kuimarisha Mpaka huu inayotekelezwa na Timu ya Wataalamu kutoka Tanzania na Kenya inaendelea vizuri, ambapo kwa sasa kazi hiyo inaendelea kati ya eneo la Namanga na Ziwa Jipe.

***Mpaka wa Tanzania Katika Bahari ya Hindi***

17. ***Mheshimiwa Spika,*** hali ya usalama wa mpaka huu ni shwari. Kwenye Mpaka huu tumepakana na nchi za Comoro na Shelisheli. Katika kipindi husika hakuna tukio la kuhatarisha usalama lililoripotiwa. Pamoja na hali hiyo, Mpaka huu unakabiliwa na changamoto zifuatazo; uvuvi haramu, biashara za magendo, usafirishaji haramu wa binadamu na dawa za kulevya. JWTZ inaendelea kufanya doria za mara kwa mara katika eneo la Mpaka kwenye Bahari ya Hindi kukabiliana na changamoto hizo.

***Mpaka wa Tanzania na Msumbiji***

18. ***Mheshimiwa Spika,*** hali ya usalama wa mpaka huu ni ya wastani na isiyotabirika kutokana na uwepo wa kundi la kigaidi la Ansar Al Sunna Wal Jammah (AASWJ) Kaskazini mwa Msumbiji, katika maeneo ya mwambao na Mpaka mkabala na Mkoa wa Mtwara. Kundi hilo limeweka ngome katika Wilaya ya Macomia, Cabo Delgado na limeendelea kuhatarisha amani na usalama katika eneo hilo. Aidha, limebuni mbinu isiyotumia nguvu (Non – Violence Radicalization) ya kuwafikia na kuwalingania washirika wapya kwa njia ya amani. Vilevile, limeendelea kujiimarisha kwa kupata wafuasi na silaha kutoka vyanzo mbalimbali, ikiwemo kwa kupora kutoka vikundi vya ulinzi na usalama nchini Msumbiji.

19. ***Mheshimiwa Spika,*** hatua zilizochukuliwa kukabiliana na hali hiyo ni pamoja na kuimarisha ushirikiano kati ya nchi yetu na

Msumbiji kwenye nyanja za mafunzo, kubadilishana taarifa na kufanya operesheni za kijeshi za pamoja.

***Mpaka wa Tanzania na Malawi***

20. ***Mheshimiwa Spika,*** hali ya usalama ya mpaka huu ni shwari. Hakuna tukio la kuhatarisha usalama lililoripotiwa. Wananchi wanaoishi maeneo ya mpakani wameendelea kushirikiana hususan, katika shughuli za kiuchumi na kijamii.

***Mpaka wa Tanzania na Zambia***

21. ***Mheshimiwa Spika,*** hali ya usalama katika mpaka huu ni shwari. Katika kipindi husika, hakuna tukio la kuhatarisha usalama wa nchi yetu lililoripotiwa.

***Mpaka wa Tanzania na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo***

22. ***Mheshimiwa Spika,*** hali ya usalama wa mpaka huu ni shwari. Hakuna tukio lililoripotiwa la kuhatarisha usalama wa nchi yetu. Hata hivyo, uwepo wa vikundi vya uasi na kigaidi Mashariki mwa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo (DRC) vikiwemo vya *The March 23 Movement* (M23), *Allied Democratic Forces* (ADF), *The Cooperative for the Development of the Congo (CODECO), Democratic Force for the Liberation of Rwanda* (FDLR) na Maimai unaendelea kuwa tishio katika Mpaka huu.

23. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kupitia JWTZ imeendelea kuchukua hatua na kujipanga wakati wote kukabiliana na tukio lolote la kuhatarisha usalama wa nchi yetu litakalojitokeza. Vilevile, ushiriki wa Tanzania katika Misheni ya Umoja wa Mataifa nchini DRC (United Nations Organisation Stabilization Mission in the Democratic Republic of the Congo - MONUSCO) na Jeshi la pamoja la Jumuiya ya Afrika Mashariki (East African Community Regional Force - EACRF) inaisaidia kurejesha amani na usalama nchini DRC na kuimarisha usalama wa Mpaka wetu. Aidha, ushirikiano baina ya nchi yetu na

DRC katika masuala mbalimbali ya kiulinzi, ikiwemo mafunzo, unaimarisha usalama wa nchi zetu.

***Mpaka wa Tanzania na Burundi***

24. ***Mheshimiwa Spika,*** hali ya usalama wa Mpaka huu ni shwari. Pamoja na hali hiyo, Mpaka unakabiliwa na changamoto ya wahamiaji haramu ambao baadhi yao hujihusisha na uhalifu wa kutumia silaha na kuharibu mazingira kutokana na ukataji miti, kilimo na ufugaji. Serikali ya nchi yetu na Serikali ya Burundi zinaendelea kushirikiana kutatua changamoto hizo.

***Mpaka wa Tanzania na Rwanda***

25. ***Mheshimiwa Spika,*** hali ya usalama wa Mpaka huu ni shwari. Hata hivyo, Mpaka huu unakabiliwa na changamoto ya uhamiaji haramu, uhalifu wa kutumia silaha, uingizaji haramu wa mifugo kwa ajili ya malisho pamoja na uvunaji haramu wa mazao ya misitu. Wizara kupitia JWTZ inaendelea kuchukua hatua za kudhibiti changamoto hizo kwa kushirikiana na nchi ya Rwanda.

26. ***Mheshimiwa Spika,*** naomba nitoe wito kwenu Waheshimiwa Wabunge na wananchi wote, kuwa ulinzi wa Taifa letu ni jukumu la kila Mtanzania, na kila mmoja wetu anajukumu la kutekeleza wajibu huo. Wanajeshi wetu wanafanya kazi kubwa sana usiku na mchana, kwa weledi, uhodari, na uzalendo wa hali ya juu. Nawapongeza sana kwa moyo huo wa kujituma, na kwa kazi kubwa wanayoifanya.

## C. UTEKELEZAJI WA MAONI NA USHAURI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA MAMBO YA NJE, ULINZI NA USALAMA

27. ***Mheshimiwa Spika,*** Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama ilipitia na kujadili utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023 na kutoa maoni, ushauri, na maelekezo, yaliyolenga kuboresha utendaji kazi na utekelezaji wa majukumu kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024.

Napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa, maoni, ushauri na maelekezo ya Kamati yamefanyiwa kazi na kuzingatiwa wakati wa kuandaa na kukamilisha Mpango na Bajeti ya Mwaka wa Fedha 2023/2024, ninayowasilisha leo hapa Bungeni.

## D. UTEKELEZAJI WA ILANI YA UCHAGUZI YA CHAMA CHA MAPINDUZI (CCM) YA MWAKA 2020 KWA MWAKA WA FEDHA 2022/2023

28. ***Mheshimiwa Spika,*** katika utekelezaji wa Mpango na Bajeti katika Mwaka wa Fedha 2022/2023, Wizara imeendelea kutekeleza Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi ya Mwaka 2020 kwa masuala yaliyoainishwa katika Sura ya Tano, Ibara ya 105 ya Ilani, ambayo ni:

a. *"Kuimarisha ulinzi na usalama wa nchi na mipaka yake ili kudumisha Muungano, kulinda Mapinduzi Matukufu ya Zanzibar, umoja, mshikamano, amani na usalama wa raia na mali zao;*

b. *Kuendeleza jitihada za utatuzi wa changamoto za mipaka ya nchi yetu na nchi jirani;*

c. *Kuwezesha ushirikiano wa Vyombo vya Ulinzi na Usalama kufanya utafiti na ubunifu kwa kushirikiana na taasisi za utafiti;*

d. *Kuhusisha kikamilifu Majeshi ya Ulinzi na Usalama katika kulinda miradi mikubwa ya kimkakati;*

e. *Kuhamasisha na kuelimisha wananchi juu ya masuala ya ulinzi, uzalendo wa kitaifa, usalama na umuhimu wa kushiriki katika ulinzi ikiwa ni pamoja na Jeshi la Akiba na ulinzi shirikishi ili kuimarisha ulinzi na usalama wa nchi yetu;*

f. *Kuimarisha uwezo wa vyombo vyetu vya ulinzi na usalama katika kushiriki shughuli za kiuchumi ikiwa ni pamoja na kuanzisha viwanda katika sekta ya ulinzi na maeneo mengine ya kimkakati;*

g. *Kuimarisha viwanda vya NYUMBU na Mzinga ili viweze kutimiza azma ya kuanzishwa kwake;*

h. *Kuimarisha Jeshi la Kujenga Taifa (JKT) na Jeshi la Kujenga Uchumi (JKU) ili viwe vyombo vya kuwapatia vijana ujuzi wa kujiajiri na kuajiriwa na pia kuwa vyombo mahiri vya huduma na uzalishaji mali hasa katika ujenzi, kilimo, ufugaji na uvuvi;*

i. *Kupanua na kuongeza idadi ya kambi za JKT na JKU ili kuwezesha vijana wengi zaidi wakiwemo wahitimu wote wa kidato cha sita kupata fursa ya mafunzo ili kujenga uzalendo na moyo wa kujitolea; na*

j. *Kuboresha mazingira ya kazi kwa kuwapatia makazi bora na kuongezea uwezo wa vyombo vyetu vya ulinzi na usalama kwa kuvipatia mafunzo ya kitaaluma na kitaalam, vitendea kazi na zana za kisasa zinazoendana na teknolojia ya kisasa".*

## E. MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA MPANGO NA BAJETI YA MWAKA WA FEDHA 2022/2023

29. ***Mheshimiwa Spika***, katika Mwaka wa Fedha 2022/2023, Wizara ilikadiriwa kukusanya maduhuli yenye jumla ya **Shilingi 87,603,000.00** kutoka katika mafungu yake matatu; Fungu 38 - NGOME, **Shilingi 22,000,000.00,** Fungu 39 - JKT, **Shilingi 64,403,000.00** na Fungu 57 - Wizara **Shilingi 1,200,000.00**.

30. ***Mheshimiwa Spika***, hadi kufikia mwezi Aprili 2023, Wizara imefanikiwa kukusanya maduhuli ya jumla ya **Shilingi 81,684,151.48,** sawa na **asilimia 93.24** ya makadirio. Kwa upande wa Fungu 38 – NGOME, limekusanya maduhuli yenye jumla ya **Shilingi 17,281,151.48** sawa na **asilimia 78.55** ya makadirio, ambayo yametokana na uwakala wa kampuni mbalimbali za Bima na mauzo ya nyaraka za zabuni. Fungu 39 – JKT limekusanya **Shilingi 64,403,000.00** sawa na **asilimia 100** ya makadirio, ambazo zimetokana na mauzo ya mazao ya kilimo na nyaraka za zabuni. Fungu 57 – Wizara, halikuweza

kukusanya maduhuli kwa kipindi husika. Muhtasari wa mchanganuo wa maduhuli kwa kila Fungu umeoneshwa kwenye **Jedwali Na. 1**.

**Jedwali Na. 1: Muhtasari wa Mchanganuo wa Makusanyo ya Maduhuli uanzia Julai, 2022 hadi Aprili 2023**

| Na. | Fungu | Makadirio ya Mapato 2022/2023 | Makusanyo Julai 2022 hadi Aprili 2023 | Makusanyo (%) |
|---|---|---|---|---|
| 1. | 38 - NGOME | 22,000,000.00 | 17,281,151.48 | 78.55 |
| 2. | 39 - JKT | 64,403,000.00 | 64,403,000.00 | 100 |
| 3. | 57 - Wizara | 1,200,000.00 | - | - |
| | **Jumla** | **87,603,000.00** | **81,684,151.48** | 31.24 |

31. ***Mheshimiwa Spika***, katika Bajeti ya Mwaka wa Fedha 2022/2023, Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa iliidhinishiwa jumla ya **Shilingi 2,713,787,405,453.00** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na Maendeleo katika mafungu yake matatu: Fungu 38 - NGOME, Fungu 39 - JKT na Fungu 57 - Wizara**.** Kati ya fedha hizo, **Shilingi 2,483,454,234,453.00** ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na **Shilingi 230,333,171,000.00** ni kwa ajili ya Matumizi ya Maendeleo. Muhtasari wa Mchanganuo wa Bajeti kwa kila Fungu umeainishwa katika **Jedwali Na. 2.**

32. ***Mheshimiwa Spika,*** hadi kufikia Aprili 2023 fedha zilizopokelewa kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na Maendeleo ni jumla ya **Shilingi 2,248,025,373,347.37**, sawa na asilimia 82.84 ya Bajeti iliyoidhinishwa. Kati ya fedha hizo, **Shilingi 2,131,861,103,775.16** ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida, na **Shilingi 116,164,269,572.21** ni kwa ajili ya Shughuli za Maendeleo.

33. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kiasi hicho; Fungu 38 – NGOME limepokea fedha za Matumizi ya Kawaida **Shilingi**

**1,749,329,241,455.70** na Fedha za Maendeleo **Shilingi 26,363,978,372.26;** Fungu 39 – JKT limepokea fedha za Matumizi ya Kawaida Shilingi 365,518,946,999.94 na Fedha za Maendeleo Shilingi 7,000,000,000.00; na Fungu 57 – Wizara limepokea fedha za Matumizi ya Kawaida **Shilingi 17,012,915,319.52** na Fedha za Maendeleo **Shilingi 82,800,291,199.95.** Muhtasari wa mchanganuo wa mapokezi ya fedha kwa mafungu yote umeainishwa katika **Jedwali Na. 3.**

**Jedwali Na. 3: Muhtasari wa Mchanganuo wa Fedha Zilizopokelewa Kuanzia Julai, 2022 hadi Aprili, 2023**

| Fungu | Aina ya Matumizi | Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023 | Kiasi kilichopokelewa Hadi Aprili 2023 | Asilimia |
|---|---|---|---|---|
| 38 - NGOME | Malipo na Posho | 1,647,307,729,453.00 | 1,423,328,599,992.96 | 86.40 |
| | Chakula | 253,860,967,000.00 | 211,550,805,830.00 | 83.33 |
| | Posho ya msamaha wa kodi | 76,424,400,000.00 | 57,318,300,000.00 | 75.00 |
| | Matumizi Mengineyo | 70,130,407,000.00 | 57,131,535,632.74 | 81.46 |
| | **Jumla Ndogo (Matumizi ya Kawaida)** | **2,047,723,503,453.00** | **1,749,329,241,455.70** | **85.43** |
| | Maendeleo | 56,367,636,000.00 | 26,363,978,372.26 | 46.77 |
| | **Jumla ya Fungu** | **2,104,091,139,453.00** | **1,775,693,219,827.96** | **84.39** |

| Fungu | Aina ya Matumizi | Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023 | Kiasi kilichopokelewa Hadi Aprili 2023 | Asilimia |
|---|---|---|---|---|
| 39 - JKT | Malipo na Posho | 276,094,534,000.00 | 262,419,156,544.00 | 95.05 |
| | Chakula | 70,984,053,000.00 | 48,212,192,500.00 | 67.92 |
| | Posho ya msamaha wa kodi | 11,493,000,000.00 | 8,100,000,000.00 | 70.48 |
| | Matumizi Mengineyo | 37,292,054,000.00 | 30,787,597,955.94 | 82.56 |
| | Mafunzo ya Vijana wa Mujibu wa Sheria | 16,000,000,000.00 | 16,000,000,000.00 | 100.00 |
| | **Jumla Ndogo (Matumizi ya Kawaida)** | **411,863,641,000.00** | **365,518,946,999.94** | **88.75** |
| | Maendeleo | 13,965,535,000.00 | 7,000,000,000.00 | 50.12 |
| | **Jumla ya Fungu** | **425,829,176,000.00** | **372,518,946,999.94** | **87.48** |
| | | | | |
| 57 - Wizara | Mishahara | 10,206,672,000.00 | 7,090,067,972.33 | 69.47 |
| | Matumizi Mengineyo | 13,660,418,000.00 | 9,922,847,347.19 | 72.64 |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | **Jumla Ndogo (Matumizi ya Kawaida)** | **23,867,090,000.00** | **17,012,915,319.52** | **71.28** |
| | Maendeleo | 160,000,000,000.00 | 82,800,291,199.95 | 51.75 |
| | **Jumla ya Fungu** | **183,867,090,000.00** | **99,813,206,519.47** | **54.29** |
| | **Jumla Kuu** | **2,713,787,405,453.00** | **2,248,025,373,347.37** | **82.84** |

**Shughuli Zilizotekelezwa kwa Fedha za Matumizi ya Kawaida**

34. ***Mheshimiwa Spika,*** katika Mwaka wa Fedha 2022/2023, Wizara imefanikiwa kutekeleza shughuli mbalimbali kwa kutumia fedha zilizotolewa kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida. Shughuli hizo ni pamoja na; mafunzo na mazoezi ya kijeshi, mafunzo ya Jeshi la Kujenga Taifa, mafunzo ya Jeshi la Akiba, matunzo ya zana na vifaa vya kijeshi, huduma za afya na tiba, ushirikiano na mamlaka za kiraia, ushirikiano wa kiulinzi na nchi nyingine, ushiriki wa Jeshi katika michezo, mapambano dhidi ya magonjwa ambukizi na yasiyoambukiza, utawala bora na utunzaji wa mazingira.

***Mafunzo na Mazoezi ya Kijeshi***

35. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kupitia JWTZ imeendelea kutoa mafunzo mbalimbali yakiwemo ya awali na kuwaendeleza wanajeshi katika taaluma za ujuzi na uongozi kwenye shule na vyuo vya kijeshi. Aidha, imeendelea kupeleka Maafisa na Askari nje ya nchi kwa ajili ya kupata mafunzo mbalimbali ya kijeshi ambayo yameongeza weledi katika utendaji.

36. ***Mheshimiwa Spika,*** katika Mwaka wa Fedha 2022/2023 JWTZ ilifanikiwa kufanya mazoezi ya ndani katika maeneo mbalimbali nchini. Mazoezi hayo ni pamoja na; zoezi la LINDA KISIWA lililofanyika

Zanzibar mwezi Septemba 2022, mazoezi ya LINDA MPAKA na *DRAGON FLY* yaliyofanyika katika Mikoa ya Lindi, Mtwara na Ruvuma mwezi Oktoba na Novemba 2022 mtawalia, pamoja na mazoezi mawili ya KAA TAYARI yaliyofanyika Mkoani Tabora mwezi Novemba 2022 na mwanzoni mwa mwezi Mei 2023.

***Mafunzo ya JKT***

37. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kupitia JKT imeendelea kuwapatia vijana wa Kitanzania mafunzo ya ukakamavu, stadi za kazi, kuwajengea uzalendo na umoja wa kitaifa. Katika kipindi husika, mafunzo yamefanyika kwenye kambi mbalimbali za JKT kupitia **Operesheni Jenerali Venance Mabeyo.** Jumla ya vijana **24,458** wa Mujibu wa Sheria wamepatiwa mafunzo, kati yao **17,942** wa kiume na **6,516** wa kike. Aidha, vijana **11,358** wa Kujitolea wamepatiwa mafunzo, kati yao **7,483** ni wa kiume na **3,875** ni wa kike.

38. ***Mheshimiwa Spika,*** JKT imeendelea kutekeleza Mkakati wa Kilimo (2019/2020 -2024/2025) ambao unalenga kuongeza uzalishaji wa mazao na kujitosheleza kwa chakula ili kuipuguzia Serikali gharama za kulisha vijana wanaohudhuria mafunzo ya JKT na kuiwezesha nchi kuwa na akiba ya chakula.

39. ***Mheshimiwa Spika,*** kuwezesha Mkakati huo kutekelezwa ipasavyo JKT imeendelea kushirikiana na Wizara ya Kilimo kupitia Mkataba wa Makubaliano katika maeneo ya teknolojia za kilimo, utafiti wa kilimo, uzalishaji wa mazao ya kimkakati na uzalishaji wa mbegu za chikichi, kahawa, mahindi, mpunga na alizeti. Utekelezaji wa Mkataba huo, umewezesha JKT kuongeza uzalishaji wa mazao husika.

40. ***Mheshimiwa Spika,*** vilevile, JKT ipo katika hatua za kuingia makubaliano na Wizara ya Mifugo na Uvuvi ili kuwezesha vijana wa JKT kupata mafunzo kwa vitendo kupitia Vituo Atamizi vilivyoanzishwa na Wizara ya Mifugo na Uvuvi sehemu mbalimbali nchini.

41. ***Mheshimiwa Spika,*** pia, JKT inashirikiana na Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania kuwawezesha vijana kupata ujuzi katika ufugaji wa nyuki ambapo Wakala wa Huduma za Misitu imeipatia JKT mizinga 100 ya kisasa ya kufugia nyuki.

42. ***Mheshimiwa Spika,*** JKT imefanikiwa kuimarisha umoja wa Kitaifa kwani Vijana wengi waliopitia JKT wameonesha moyo wa kupenda kazi za mikono, kujituma na kujiheshimu; kutoa wanamichezo bora, wenye viwango vya kitaifa na kimataifa na hivyo kuiletea sifa nchi yetu; kuwaandaa vijana kuwa tayari kuitumikia nchi katika majanga ikiwemo mafuriko, ajali za moto na ajali nyinginezo; na kuwa mfano wa kuigwa na mataifa jirani na hivyo kuwa chachu kwa mataifa hayo kuanzisha shughuli za malezi ya vijana katika nchi zao ikiwemo Zambia na Msumbiji.

43. ***Mheshimiwa Spika,*** napenda kutumia fursa hii kuliarifu Bunge lako Tukufu pamoja na umma wa Watanzania kwamba, dhumuni la mafunzo yanayotolewa kwa vijana ni kuwapatia ukakamavu, stadi za kazi, kuwajengea uzalendo na umoja wa kitaifa ili baada ya kumaliza muda wa mafunzo na kutumikia JKT, waweze kurejea majumbani kwao wakiwa raia wema, wazalendo na wenye uwezo wa kujitegemea na kulilinda Taifa. Nitoe rai kwa vijana wote wanaopata fursa za kupata mafunzo hayo, kuzitumia stadi za kazi na maisha walizozipata kujiajiri na kujitegemea.

44. ***Mheshimiwa Spika,*** nitumie fursa hii kuwasisitiza wananchi kuwasiliana na Mamlaka husika pindi nafasi za JKT na JWTZ zinapotangazwa ili kujiepusha na matapeli ambao huwadanganya watawapatia nafasi katika vyombo hivi.

***Mafunzo ya Jeshi la Akiba***

45. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kupitia JWTZ imeendelea kutoa mafunzo ya Jeshi la Akiba kwa wananchi katika ngazi ya awali, kwenye Mikoa yote ya Tanzania. Katika kipindi cha Julai 2022 hadi Aprili 2023, wananchi walioandikishwa na kuhitimu mafunzo hayo wameongezeka kwa takribani **asilimia tisa** kutoka wahitimu **12,510**

kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022 na kufikia wahitimu **13,632** kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023, kati yao wanaume ni **11,680** na wanawake ni **1,952.** Aidha, Jeshi la Akiba limeendelea kushiriki katika mazoezi ya Kijeshi, ambapo katika Mwaka wa Fedha 2022/23, limeshiriki katika mazoezi mawili ya KAA TAYARI yaliyofanyika mkoani Tabora.

***Huduma za Afya na Tiba***

46. ***Mheshimiwa Spika,*** JWTZ imeendelea kutoa huduma za tiba kwa Maafisa, Askari, Watumishi wa Umma, Familia za Wanajeshi na Wananchi wanaoishi karibu na vituo vya tiba vya Jeshi. Katika kuboresha huduma za Afya, juhudi mbalimbali zimeendelea kufanyika ikiwemo; ununuzi wa vifaa tiba vinavyojumuisha *MRI Scanner, CT Scanner, digital X - ray, dental units, Advanced Ultra Sound Scanner,* mashine mbalimbali za uchunguzi katika maabara na Mtambo wa kuzalisha Hewa ya Oksijeni.

47. ***Mheshimiwa Spika,*** JWTZ inaendelea na Mradi wa Ujenzi wa Hospitali yenye hadhi ya Ngazi ya Nne (Level IV Military Hospital) kwa viwango vya Umoja wa Mataifa. Hospitali hiyo inajengwa Msalato, Jijini Dodoma kwa kushirikiana na Serikali ya Ujerumani kupitia *German Armed Forces Technical Advisory Group* (GAFTAG). Kwa sasa Mradi huu upo katika awamu ya pili inayohusisha ujenzi wa Jengo Kuu la Hospitali.

***Ushirikiano na Mamlaka za Kiraia Katika Shughuli Mbalimbali***

48. ***Mheshimiwa Spika,*** JWTZ imeendelea kushirikiana na Mamlaka za Kiraia katika shughuli mbalimbali ikiwemo; kutoa misaada wakati wa majanga na maafa, kushiriki katika utekelezaji wa ulinzi wa miradi ya kimkakati ikiwemo Reli ya Kiwango cha Kimataifa (SGR), Bwawa la Kufua Umeme wa Maji la Julius Nyerere (JNHPP), Mgodi wa Tanzanite, Mamlaka ya Bandari Tanzania (TPA), Kampuni ya Simu Tanzania (TTCL) na maeneo ya Viwanja vya Ndege.

49. ***Mheshimiwa Spika,*** vilevile, JWTZ imeendelea kushiriki katika shughuli za uokoaji wa raia na mali zao wakati na baada ya maafa na majanga, yakiwemo mafuriko yaliyotokea Mkoani Mtwara. Pia, JWTZ ilishiriki katika kuzima moto mkubwa uliotokea katika Hifadhi ya Mlima Kilimanjaro na kusafirisha misaada ya kibinadamu na kufanya uokozi kwa wahanga wa mafuriko nchini Malawi.

***Ushirikiano wa Kiulinzi na Nchi Nyingine***

50. ***Mheshimiwa Spika,*** JWTZ imeendelea kushirikiana na nchi rafiki katika masuala ya ulinzi na usalama katika maeneo mbalimbali ikiwemo; mafunzo, misaada ya kitaalam, zana na vifaa. Vilevile, JWTZ inashirikiana na Umoja wa Mataifa (UN), Umoja wa Afrika (AU), Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC), na Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC) katika mafunzo na ubadilishanaji wa wataalamu. Pia, JWTZ inaendelea kushirikiana na nchi rafiki katika kutoa mafunzo kwa Maafisa na Askari. Nchi hizo ni pamoja na; Algeria, Bangladesh, Canada, Ethiopia, Finland, Ghana, Hispania, India, Indonesia, Israeli, Jamhuri ya Watu wa China, Jordan, Marekani, Misri, Morocco, Nigeria, Oman, Pakistan, Sri Lanka, Jamaica, Sweden, Ufaransa, Uholanzi, Uingereza, Ujerumani, Umoja wa Falme za Kiarabu, Urusi, Uturuki, na Uswisi. Aidha, JWTZ imeendelea kushirikiana na nchi za Msumbiji na DRC katika kutoa mafunzo kwa Maafisa na Askari wa nchi hizo hapa nchini ili kuwajengea uwezo wa kukabiliana na matishio ya amani katika nchi zao.

51. Wizara kupitia Chuo cha Taifa cha Ulinzi (NDC) hutoa mafunzo ya usalama na stratejia kwa maafisa wa Vyombo vya Ulinzi na Usalama, pamoja na viongozi wa Umma. Pia, NDC imeendelea kutoa mafunzo hayo kwa washiriki kutoka nchi za Afrika Kusini, Bangladesh, Botswana, Burundi, China, Kenya, Malawi, Misri, Msumbiji, Namibia, Nigeria, Rwanda, Uganda, Zambia, na Zimbabwe.

***Ushiriki wa JWTZ Katika Shughuli za Ulinzi wa Amani***

52. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kupitia JWTZ imeendelea kushirikiana na Jumuiya za Kikanda na Kimataifa katika operesheni za ulinzi wa amani. JWTZ imeendelea kuwa na vikosi vya ulinzi wa amani katika nchi za Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo, Afrika ya Kati na Lebanon chini ya Misheni za Umoja wa Mataifa na inashiriki katika Operesheni ya kupambana na ugaidi nchini Msumbiji (SADC Mission in Mozambique - SAMIM). Vilevile, Jeshi lina maafisa wanadhimu kwenye operesheni za ulinzi wa amani nchini Sudan Kusini, Lebanon, Jamhuri ya Afrika ya Kati na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo.

53. Mheshimiwa Spika, ushiriki wa JWTZ katika operesheni za ulinzi wa amani chini ya Umoja wa Mataifa umeiwezesha nchi yetu kutimiza matakwa ya Umoja wa Mataifa na Jumuiya za Kikanda ya kushiriki katika ulinzi wa amani, kimataifa na kikanda. Vilevile, ushiriki huu unaendeleza Diplomasia ya Kijeshi, na unasaidia JWTZ kuongeza uwezo kwa kufanya kazi na nchi nyingine.

**Ushiriki wa JWTZ Katika Michezo**

54. ***Mheshimiwa Spika,*** JWTZ imeshiriki katika michezo mbalimbali ndani na nje ya nchi ikiwemo; Mashindano ya Dunia ya Michezo ya Majeshi yaliyofanyika Ujerumani, mwezi Julai 2022, Michezo ya Jumuiya ya Madola iliyofanyika Birmingham nchini Uingereza mwezi Agosti 2022, Mashindano ya Ngumi ya Ukanda wa Afrika yaliyofanyika nchini mwezi Agosti 2022, *East African Championship* yaliyofanyika Burundi mwezi Septemba 2022, Mashindano ya Gofu yaliyofanyika Lilongwe nchini Malawi mwezi Novemba 2022, michezo ya majeshi (BAMMATA) iliyofanyika Mkoani Mtwara mwezi Februari 2023, Mashindano ya Riadha yaliyofanyika nchini Japan (Osaka Marathon) na China (Yangzhou Jianzhen International Half Marathon) mwezi Februari na Aprili 2023 mtawalia.

55. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mashindano hayo, wanamichezo wetu wa JWTZ waliweza kupata ushindi na kuliletea Taifa letu medali.

Napenda kutumia fursa hii, kuwapongeza. Kipekee **Sajini Taji Seleman Kidunda** aliyetwaa ubingwa wa "**World Boxing Federation in Africa" (WBF); Sajini Alphonce Felix Simbu,** aliyepata medali ya shaba katika mbio za ***Osaka Marathon* na *Yangzhou Jianzhen International Half Marathon*; Praiveti Kassim Mbudikwe** na **Praiveti Yusuph Changarawe**, waliopata **medali ya shaba** kila mmoja katika mashindano ya ngumi ya Jumuiya ya Madola.

56. ***Mheshimiwa Spika,*** timu teule ya mpira wa kikapu iliyoshiriki mashindano ya Majeshi Duniani yaliyofanyika nchini Ujerumani mwezi Agosti 2022 ilishika **nafasi ya nne (4)** kati ya **Mataifa 19** yaliyoshiriki Mashindano hayo.

57. ***Mheshimiwa Spika,*** ushiriki huo umewezesha JWTZ kuimarisha mahusiano na ushirikiano kati yake na nchi rafiki na Vyombo vya Usalama. Aidha, kupitia shughuli za Baraza la Michezo ya Majeshi Duniani (CISM) JWTZ imeweza kujenga uhusiano baina yake na Jeshi la nchi ya Ujerumani ambapo Jeshi hilo limetupatia wakufunzi wa michezo ya mpira wa wavu, mpira wa kikapu na ngumi. Pia, Timu ya Mpira wa Miguu ya JKT Queens imealikwa kushiriki katika mashindano ya *World Military Women Football Championship* yatakayofanyika kuanzia tarehe 27 Juni, 2023 hadi 9 Julai, 2023 nchini Uholanzi. Vilevile, nchi yetu imepata fursa ya kuandaa Mkutano Mkuu wa Baraza la Michezo ya Majeshi Duniani ambao utafanyika Jijini Dar es Salaam mwezi Mei 2024.

58. ***Mheshimiwa Spika*****,** timu za Jeshi zimeshiriki katika mashindano yanayoandaliwa na Shirikisho la Mpira wa Miguu Tanzania (TFF) ambapo timu ya JKT Queens imefanikiwa kutwaa Ubingwa wa Ligi Kuu ya Wanawake Tanzania. Vilevile, JKT Tanzania iliyokuwa ikishiriki Ligi Daraja la Kwanza imefanikiwa kupanda daraja na msimu wa ligi 2023/24 itashiriki Ligi Kuu ya Tanzania Bara ambayo kwa sasa inajulikana kwa jina la *NBC Premier Legue*. Nazipongeza timu hizo kwa mafanikio hayo.

59. Wizara imeendelea kushirikiana na Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo katika kuibua vipaji na kuviendeleza kwa lengo la kuinua kiwango cha michezo nchini.

***Mapambano Dhidi ya Magonjwa Ambukizi na Yasiyoambukiza***

60. ***Mheshimiwa Spika,*** kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023, Wizara imeendelea kutekeleza mikakati ya kupambana na Virusi vinavyosababisha Upungufu wa Kinga Mwilini na Magonjwa Yasiyoambukiza. Huduma ya lishe kwa watumishi wenye maambukizi ya VVU imeendelea kutolewa. Hatua hizi zinachukuliwa kwa kuzingatia Mwongozo wa Kudhibiti VVU, UKIMWI na Magonjwa Sugu Yasiyoambukizwa Mahali pa Kazi wa mwaka 2014 uliotolewa na Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma. Aidha, katika Mwaka wa Fedha 2022/2023 Wizara kwa kushirikiana na Wizara ya Afya na TACAIDS imeendelea kutoa elimu na kuhamasisha upimaji wa hiari na uchangiaji damu.

***Utawala Bora***

61. ***Mheshimiwa Spika,*** katika hatua ya kudumisha dhana ya utawala bora, Wizara imeendelea kuimarisha ushirikishwaji wa watumishi kupitia vikao vya Baraza la Wafanyakazi. Aidha, Maafisa, Askari na Watumishi wa Umma hupata fursa ya kushiriki semina mbalimbali ambazo zimeongeza uadilifu na uwajibikaji katika utendaji kazi wa kila siku.

***Utunzaji wa Mazingira***

62. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi husika JWTZ imeendelea kushiriki katika utunzaji wa mazingira na kuhakikisha mazingira yanayozunguka maeneo ya Jeshi yanatunzwa kwa kuwa safi pamoja na kupanda miti. Vilevile, JWTZ imekuwa ikishiriki katika utunzaji wa mazingira kwa kufanya usafi katika maeneo yanayotoa huduma za kijamii ikiwemo hospitali. Wakati wa maadhimisho ya Mapinduzi Matukufu ya Zanzibar, JWTZ ilishiriki kupanda miti katika maeneo mbalimbali nchini ikiwemo Jijini Dodoma ambapo upandaji

miti uliongozwa na Mhe. Dkt. Philip Isdor Mpango, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

63. Wizara kupitia JWTZ imejipanga kutumia nishati ya gesi katika vikosi, vyuo na shule. Mpango uliopo kwa sasa ni kuweka miundombinu wezeshi kuwezesha azma hiyo kutekelezwa.

**Shughuli Zilizotekelezwa kwa Fedha za Maendeleo**

64. *Mheshimiwa Spika,* Fungu 57 - Wizara ya Ulinzi na JKT katika Mwaka wa Fedha 2022/2023 liliidhinishiwa kiasi cha Shilingi 160,000,000,000.00 kwa ajili ya kugharamia Shughuli za Maendeleo. Hadi kufikia mwezi Aprili 2023, kiasi cha Shilingi 82,800,291,199.95 kimepokelewa, sawa na asilimia 51.75 ya Bajeti iliyoidhinishwa. Fedha zilizopokelewa zimetumika kugharamia ununuzi na matengenezo ya zana na vifaa mbalimbali vya Kijeshi.

65. ***Mheshimiwa Spika,*** pia, fedha hizo zimetumika kugharamia; malipo ya awali ya mafunzo ya marubani na matengenezo ya Helikopta, ujenzi wa nyumba za makazi kwa ajili ya Maafisa na Askari katika Kikosi cha Jeshi Ubago - Unguja, ujenzi wa makazi ya Askari eneo la Ngara, ujenzi wa karakana ya kukarabati silaha ndogo – Mzinga, ujenzi wa *Taxiway*, *Apron* na karakana katika Shule ya Anga ya Kijeshi (SAK) Mkoani Tanga, marekebisho ya mfumo wa maji Makao Makuu ya Brigedi ya Mbuni – Arusha, Tathmini ya Hali ya Ulinzi na mafunzo ya Ufuatiliaji na Tathmini (U&T).

66. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea kutekeleza Mkakati wa Uhakiki, Upimaji na Uthamini wa Maeneo ya Jeshi wa Miaka Mitatu (2020/21 – 2022/23) ili kuhakikisha maeneo yote ya Jeshi yanapimwa na kupatiwa Hati Miliki na hivyo kuondoa migogoro iliyopo. Hadi sasa, Mkakati umetekelezwa kwa **asilimia 71.48** kwa kuhakiki, kupima na kufanya uthamini wa maeneo mbalimbali ya Jeshi nchini.

67. ***Mheshimiwa Spika,*** katika Mwaka wa Fedha 2022/23, maeneo yaliyolipwa fidia ni pamoja na Gurungu, Mtipa, Mkiwa, Mkwese na Choda Mkoani Singida; Kisakasaka na Chukwani Mkoa wa Mjini

Magharibi; Ras Nondwa Mkoani Kigoma; Itaga na Usule Mkoani Tabora; Funta Kihangaiko na Mkupuka Mkoani Pwani; Bulifani Misenyi Mkoani Kagera na Machenje Kongwa Mkoani Dodoma.

*68.* Nitoe rai kwa Waheshimiwa Wabunge na viongozi kuendelea kuwaelimisha wananchi kuacha kuvamia maeneo ya Jeshi kwani ni hatari kwa maisha yao na mali zao.

*69.* ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuimarisha miundombinu ya kambi za JKT ili kuongeza idadi ya vijana wanaopata mafunzo, **Shilingi 1,500,000,000.00** zimetumika kujenga mahanga kumi na tano (15) katika Kikosi cha Jeshi Mtabila, mahanga mawili (02) katika Kikosi cha Jeshi Bulombora na mahanga manne (04) na ghala la kuhifadhia chakula katika Kikosi cha Jeshi Rwamkoma.

*70.* ***Mheshimiwa Spika,*** Fungu 38 - NGOME katika Mwaka wa Fedha 2022/2023 liliidhinishiwa kiasi cha **Shilingi 56,367,636,000.00** kwa ajili ya kugharamia shughuli za maendeleo. Hadi kufikia mwezi Aprili 2023, Fungu 38 - NGOME limepatiwa kiasi cha **Shilingi 26,363,978,372.26** sawa na **asilimia 46.77** ya Bajeti iliyoidhinishwa. Fedha hizo zimetumika kugharamia; ujenzi wa makazi ya washiriki wa kozi ya NDC, ujenzi na ukarabati wa maghala ya kuhifadhia silaha, ununuzi wa risasi na milipuko, ununuzi na matengenezo ya zana na vifaa, ununuzi wa vipuri, sare za wanajeshi na mafunzo ya marubani wanafunzi.

*71.* ***Mheshimiwa Spika,*** Fungu 39 - JKT katika kipindi cha kuanzia Julai 2022 hadi Aprili 2023, limepatiwa kiasi cha **Shilingi 7,000,000,000.00** sawa na **asilimia 50.12** ya Bajeti iliyoidhinishwa. Kiasi hicho kimetumika kujenga na kukarabati miundombinu ya vikosi na makambi pamoja na kuendeleza skimu ya umwagiliaji katika Kikosi cha Jeshi cha Chita.

*72.* ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kupitia JKT imefanikiwa kutekeleza miradi mbalimbali kwa kutumia rasilimali za ndani ifuatavyo:

a. Kilimo cha Michikichi katika Kikosi cha JKT Bulombora Mkoani Kigoma;

b. Kilimo cha Mkonge katika vikosi vya JKT Maramba na Mgambo Mkoani Tanga;

c. Kilimo cha Kahawa katika vikosi vya JKT Itende Jijini Mbeya na Rwamkoma Mkoani Mara;

d. Kilimo cha Korosho katika mashamba ya vikosi vya JKT Nachingwea, Makutopora, Ruvu na Kibiti katika mikoa ya Lindi, Singida na Pwani, mtawalia. Aidha, Shamba la Korosho la Kikosi cha Ruvu ni Shamba Darasa;

e. Ujenzi wa miundombinu ya Skimu ya Umwagiliaji katika Kikosi cha Chita Mkoani Morogoro;

f. Ufugaji wa Samaki katika vikosi vya JKT Rwamkoma Mkoani Mara, Chita Mkoani Morogoro, na Ruvu Mkoani Pwani; na

g. Ufugaji wa Nyuki katika vikosi vya JKT Msange Mkoani Tabora, Kanembwa na Mtabila Mkoani Kigoma.

*73.* ***Mheshimiwa Spika*****,** naomba kutumia fursa hii kuishukuru Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na **Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan,** Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Amiri Jeshi Mkuu kwa kuendelea kuzipa kipaumbele shughuli za ulinzi kwa kutoa fedha kugharamia; operesheni za kupambana na ugaidi, ujenzi wa Makao Makuu ya Ulinzi wa Taifa – Kikombo Jijini Dodoma, kusafirisha wastaafu, madeni ya wazabuni, mafunzo na vifaa vya mifumo ya malipo na ununuzi wa magari ya makamanda na Wambata Jeshi.

**Mashirika Yanayosimamiwa na Wizara**

*74.* ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kupitia Mashirika ya Tanzania Automotive Technology Centre (TATC - NYUMBU), Mzinga na Shirika

la Uzalishaji Mali (SUMAJKT) imeendelea kutekeleza majukumu yake ifuatavyo;

**TATC - NYUMBU**

*75.* ***Mheshimiwa Spika,*** katika Mwaka wa Fedha 2022/2023, Shirika la TATC liliidhinishiwa jumla ya **Shilingi 20,445,970,300.00** kwa ajili ya kutekeleza Mpango wa Maendeleo wa Miaka Kumi (2021/22 – 2030/31) wa kuliimarisha Shirika**.** Hadi kufikia Aprili 2023, Shirika limepokea kiasi cha fedha **Shilingi 12,000,000,000.00** sawa na **asilimia 60.12** ya bajeti iliyoidhinishwa kwa ajili ya kutekeleza Mpango huo. Shughuli zilizotekelezwa ni:

a. Kujenga uwezo na kuendeleza utafiti na kuhawilisha teknolojia ya magari (kufanya *Reverse Engineering* ya pampu za magari ya Zimamoto na kufanya utafiti na kuzalisha *prototype* ya Magari ya Deraya);

b. Kuajiri na kuendeleza wataalamu katika utafiti na uhawilishaji wa teknolojia ya magari na mitambo;

c. Kununua mitambo kwa ajili ya Maabara ya Utafiti;

d. Kuanzisha karakana kuu ya kukalibu chuma na kiwanda cha *Metal Galvanization*;

e. Kuanzisha kiwanda cha kuunda na kuunganisha Magari; na

f. Kufanya ukarabati wa miundombinu ya milki.

*76.* ***Mheshimiwa Spika,*** TATC imefanikiwa kuunda jumla ya magari matatu (3) yenye hadhi ya viwango vya manispaa kwa ajili ya matumizi ya Jeshi la Zimamoto na Uokoaji na kukarabati magari 11 ya kuzimia moto yenye hadhi ya viwango vya manispaa.

***Shirika la Mzinga***

*77.* ***Mheshimiwa Spika,*** katika Mwaka wa Fedha 2022/2023, Shirika la Mzinga liliidhinishiwa jumla ya **Shilingi 4,000,000,000.00.** Hadi kufikia Aprili 2023, Shirika limepokea kiasi cha **Shilingi 3,805,911,630.00** sawa na **asilimia 95.15** ya Bajeti iliyoidhinishwa na kuweza kutekeleza shughuli za maendeleo mbalimbali, ikiwa ni pamoja na:

a. Ukarabati wa majengo na miundombinu ya kiwanda;

b. Ununuzi wa malighafi na uzalishaji wa Mazao ya Msingi;

c. Ununuzi wa vipuri vya mitambo na mashine; na

d. Ununuzi wa jenereta lenye *kilowatts* 1200 kwa ajili ya kutatua changamoto za umeme katika Kiwanda.

*78.* ***Mheshimiwa Spika***, pamoja na shughuli za msingi, Shirika limeendelea na utekelezaji wa shughuli mbalimbali kwa kutumia fedha za ndani ifuatavyo:

a. Ujenzi wa Hanga la Askari lenye vyumba 20;

b. Ujenzi wa Jengo la Utawala na Wagonjwa wa Nje, Jengo la Kuhifadhi Maiti katika Hospitali ya Mzinga;

c. Kusimika Mfumo wa Usimamizi wa Hospitali na ununuzi wa vifaa tiba katika Hospitali ya Mzinga;

d. Ujenzi wa ukumbi katika eneo la Magadu Club; na

e. Ujenzi wa madarasa matatu katika Chuo cha Ufundi Stadi Mzinga.

**SUMAJKT**

*79.* ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha kuanzia mwezi Julai 2022 hadi Aprili 2023, SUMAJKT imeendelea kutekeleza shughuli za uzalishaji mali, biashara na huduma kupitia miradi na kampuni zake tanzu. Kampuni hizo ni pamoja na; SUMAJKT Construction Co. Ltd, SUMAJKT Electric Co. Ltd, SUMAJKT Bottling Co. Ltd, SUMAJKT Guard Ltd, na SUMAJKT Cleaning and Fumigation Co. Ltd. Shughuli zilizotekelezwa ni pamoja na:

a. Miradi ya ujenzi ikiwemo; majengo ya Wizara na Taasisi za Serikali tisa (09) katika Mji wa Serikali Mtumba – Dodoma, ujenzi wa Ikulu Chamwino – Dodoma, ujenzi wa majengo ya ofisi mbalimbali za Serikali, Idara, Vyuo na Taasisi binafsi. Jumla ya miradi inayoendelea kutekelezwa kwa kipindi husika ni 210;

b. Miradi miwili (2) ya usambazaji wa umeme inayotekelezwa katika mikoa ya Morogoro na Shinyanga kupitia Mradi wa *Rural Energy Agency* (REA);

c. Kutoa huduma ya ushauri, ubunifu na usanifu majenzi, ambapo miradi 19 inaendelea kutekelezwa;

d. Kuzalisha maji ya *Uhuru Peak* ambapo katika kipindi husika Kiwanda kimeongeza mikondo miwili ya uzalishaji wa maji kwa ujazo wa mililita 350 hadi lita 1.6 na lita 13 hadi lita 18;

e. Kuuza matrekta, zana za kilimo, vipuri vya matrekta na kutoa huduma baada ya mauzo. Huduma hizo zinatolewa katika mikoa ya Morogoro, Dodoma, Simiyu, Manyara, Katavi, Ruvuma, Kagera, Geita, Kigoma na Pwani;

f. Kulima mpunga ekari 2000 na kuzalisha mbegu za mahindi ekari 700 katika shamba lililopo Mngeta, Mkoani Morogoro; na

g. Kutoa huduma ya Elimu kupitia Shule ya Sekondari Jitegemee na Shule ya Msingi na Sekondari Kawawa.

*80.* ***Mheshimiwa Spika,*** Viwanda vya kijeshi huzalisha bidhaa mbalimbali kwa ajili ya matumizi ya kijeshi na kiraia. Naomba nitoe wito kwa washirika mbalimbali wa maendeleo kushirikiana nasi katika sekta hii muhimu kwa ajili ya kukuza viwanda vyetu nchini. Pia, tunawakaribisha wawekezaji kuwekeza kwenye viwanda vya kijeshi ili kuwezesha uzalishaji wa zana na vifaa vya kijeshi na hivyo kuipunguzia Serikali gharama za kuagiza kutoka nje ya nchi.

## F: MPANGO NA MWELEKEO WA BAJETI KWA MWAKA WA FEDHA 2023/2024

*81.* ***Mheshimiwa Spika,*** katika Mwaka wa Fedha 2023/2024, Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa imelenga kutekeleza Mpango na Bajeti kwa kuzingatia miongozo ifuatayo; Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025, Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano (2021/22 – 2025/26), Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya Mwaka 2020, Malengo ya Maendeleo Endelevu 2030, Mpango Mkakati wa Wizara (2021/22 – 2025/26) na Mwongozo wa Maandalizi ya Mpango na Bajeti ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024.

*82.* ***Mheshimiwa Spika,*** naomba uniruhusu kuwasilisha Mpango na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024 ifuatavyo:

### Makadirio ya Makusanyo ya Maduhuli

*83.* ***Mheshimiwa Spika,*** katika Mwaka wa Fedha 2023/2024, Wizara inatarajia kukusanya maduhuli ya jumla ya **Shilingi 87,603,000.00** kutoka katika mafungu yake matatu, ambapo Fungu 38 – NGOME linatarajia kukusanya kiasi cha **Shilingi 22,000,000.00,** Fungu 39 – JKT linatarajia kukusanya kiasi cha **Shilingi 64,403,000.00** na Fungu 57 – Wizara inatarajia kukusanya kiasi cha **Shilingi 1,200,000.00** kama inavyoonekana katika **Jedwali Na. 4.**

**Jedwali Na. 4: Makadirio ya Makusanyo ya Maduhuli kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024**

| Na. | Fungu | Makadirio ya Maduhuli 2023/24 |
|---|---|---|
| 1. | 38 – NGOME | 22,000,000.00 |
| 2. | 39 – JKT | 64,403,000.00 |
| 3. | 57 – Wizara | 1,200,000.00 |
| | **Jumla** | **87,603,000.00** |

**Matumizi ya Kawaida na Maendeleo**

84. ***Mheshimiwa Spika,*** katika Mwaka wa Fedha 2023/2024, Serikali inatarajia kutenga fedha kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na Maendeleo ikiwa na jumla ya Shilingi 2,989,967,122,000.00 **ambapo kati ya fedha hizo, Shilingi 2,767,133,951,000.00** ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida, na **Shilingi 222,833,171,000.00** ni kwa ajili ya kugharamia shughuli za maendeleo.

Mchanganuo kwa kila Fungu ni kama ilivyoainishwa katika **Jedwali Na. 5.**

**Jedwali Na. 5: Mchanganuo wa Bajeti kwa Kila Fungu kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024**

| Na. | Fungu | Matumizi ya Kawaida | Matumizi ya Maendeleo | Jumla |
|---|---|---|---|---|
| 1. | 38 - NGOME | 2,273,738,750,000.00 | 48,867,636,000.00 | 2,322,606,386,000.00 |
| 2. | 39 - JKT | 468,397,562,000.00 | 13,965,535,000.00 | 482,363,097,000.00 |
| 3. | 57 - Wizara | 24,997,639,000.00 | 160,000,000,000.00 | 184,997,639,000.00 |
| | **Jumla** | **2,767,133,951,000.00** | **222,833,171,000.00** | **2,989,967,122,000.00** |

85. ***Mheshimiwa Spika,*** shughuli zinazokusudiwa kutekelezwa katika Mwaka wa Fedha 2023/2024 zitazingatia maeneo ya kipaumbele yafuatayo:

a. Kuliimarisha Jeshi kwa zana na vifaa vya kisasa, mawasiliano na rasilimali watu;

b. Kuimarisha miundombinu mbalimbali katika Kambi za Jeshi na mipakani;

c. Kuendelea kuweka mazingira mazuri ya utendaji kazi kwa Wanajeshi ikiwemo mafunzo, maslahi, huduma bora za afya na makazi;

d. Kuendelea kulijengea uwezo Jeshi la Kujenga Taifa kutoa mafunzo ya uzalendo, ukakamavu, umoja wa kitaifa na stadi za kazi kwa vijana wa Mujibu wa Sheria na wa Kujitolea;

e. Kuendelea kuimarisha Jeshi la Akiba;

f. Kuendeleza na kusimamia rasilimali za Jeshi ikiwemo miradi ya ujenzi hususan Makao Makuu ya Ulinzi wa Taifa;

g. Kuimarisha mashirika na taasisi za utafiti wa masuala ya kijeshi, ikiwemo uanzishaji wa viwanda katika sekta ya ulinzi (Defence industries) ili kuzalisha bidhaa kwa matumizi ya Kijeshi na Kiraia;

h. Kuimarisha ushirikiano na Umoja wa Mataifa (UN), Umoja wa Afrika (AU), Jumuiya za Kikanda na nchi nyingine katika nyanja za kijeshi na kiulinzi; na

i. Kuendelea kushirikiana na Mamlaka za Kiraia katika kukabiliana na majanga na dharura inapohitajika.

## G: SHUKRANI

86. ***Mheshimiwa Spika,*** naomba nitumie fursa hii kuwashukuru wale wote wanaonisaidia kuhakikisha Dira ya Wizara inafikiwa. Nawashukuru **Dkt. Faraji Kasidi Mnyepe,** Katibu Mkuu wa Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, **Jenerali Jacob** John Mkunda, **Mkuu wa Majeshi ya Ulinzi,** Luteni Jenerali Salum Haji Othman, Mnadhimu Mkuu wa Jeshi, **Meja Jenerali Rajabu Nduku Mabele,** Mkuu wa Jeshi la Kujenga Taifa, Wakuu wa Kamandi, Wakuu wa Mashirika, Wakuu wa Idara na Vitengo (Wizara ya Ulinzi na JKT), Wakuu wa Matawi (Makao Makuu ya Jeshi), Wakuu wa Idara (Makao Makuu ya Jeshi la Kujenga Taifa), Maafisa, Askari na Watumishi wa Umma waliopo Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa.

87. ***Mheshimiwa Spika,*** naomba nitumie fursa hii, kwa niaba ya Serikali kutoa shukrani kwa Serikali za nchi mbalimbali na washirika wa maendeleo kwa ushirikiano wanaoendelea kuipatia Wizara ninayoiongoza, ikiwa ni pamoja na; Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika, Jumuiya ya Afrika Mashariki, Canada, India, Jamhuri ya Watu wa China, Marekani, Ufaransa, Ujerumani na Uturuki. Aidha, tunazishukuru nchi rafiki kwa ushirikiano wao katika shughuli zetu za Ulinzi. Nchi hizo ni pamoja na Algeria, Bangladesh, Ethiopia, Finland, Ghana, Hispania, Indonesia, Israeli, Jamhuri ya Czech, Jordan, Misri, Morocco, Nigeria, Oman, Pakistan, Serbia, Sri Lanka, Sweden, Uholanzi, Uingereza, Umoja wa Falme za Kiarabu, Urusi, na Uswisi.

88. ***Mheshimiwa Spika,*** naomba pia kuwashukuru wananchi wote kwa ushirikiano wanaoutoa kwa Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania katika ulinzi wa nchi yetu. Ni matumaini yangu kuwa wataendelea kushirikiana na Jeshi katika kuhakikisha nchi yetu inaendelea kuwa na amani na usalama kwa kuwa ndiyo msingi wa maendeleo ya Taifa letu.

89. ***Mheshimiwa Spika,*** kwa namna ya kipekee, naomba kuwashukuru wananchi wa Jimbo la Karagwe kwa ushirikiano wanaonipatia. Ni matumaini yangu kuwa tutaendelea kushirikiana kwa manufaa ya Jimbo letu. Vilevile, napenda kuishukuru familia

yangu kwa upendo na uvumilivu wao, unaoniwezesha kutekeleza majukumu yangu.

90. ***Mheshimiwa Spika,*** napenda kukushukuru wewe binafsi na Wabunge wote kwa kunisikiliza. Hotuba hii, inapatikana pia katika tovuti ya Wizara ya Ulinzi na JKT ambayo ni *www.modans.go.tz.*

91. ***Mheshimiwa Spika,*** naomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WANAWAKE NA MAKUNDI MAALUM:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge hoja imeungwa mkono ahsanteni sana. Sasa nimwite Mwenyekiti wetu wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama kwa niaba yake anakuja Mheshimiwa Zahor Mohammed Haji. *(Makofi)*

**MHE. ZAHOR MOHAMMED HAJI - K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA MAMBO YA NJE, ULINZI NA USALAMA:** Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 118(9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023, naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama kuhusu utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kwa mwaka wa fedha 2022/2023, pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa mwaka wa fedha 2023/2024.

Mheshimiwa Spika, taarifa hii imegawanyika katika Sehemu Sita; ya kwanza ikiwa ni sehemu ya utangulizi, sehemu hiyo inatoa maelezo ya jumla kuhusu msingi na muundo wa taarifa.

Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Pili inafafanua matokeo ya ukaguzi wa miradi ya maendeleo uliofanyika kwa mujibu wa kanuni ya 117(1) ya Kanuni za Bunge na Sehemu ya Tatu hadi Nne zinafanya uchambuzi wa utekelezaji wa mipango na bajeti kwa

mwaka wa fedha 2022/2023 pamoja na kuchanganua makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara hii kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024.

Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Tano inaonesha Maoni na Ushauri wa Kamati kutokana na matokeo ya Uchambuzi. Aidha, Sehemu ya Sita na ya mwisho inakamilisha taarifa kwa kutoa shukurani na kulishauri Bunge kuhusu Hoja ya Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, juu ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hii kwa mwaka wa fedha 2023/2024.

Mheshimiwa Spika, msingi wa uchambuzi wa Kamati; msingi wa Kamati kuchambua makadirio ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa ni masharti ya kifungu cha 6(3) kikisomwa kwa pamoja na kifungu 7(1)(a) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Bunge. Aidha Kanuni ya 118(4) ya Kanuni za Bunge imeweka masharti yaliyotaka taarifa ya utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kuchambuliwa na Kamati kabla ya kujadiliwa na Bunge.

Mheshimiwa Spika, nafurahi kulijulisha Bunge lako Tukufu kwamba masharti hayo yamezingatiwa na kwamba naliomba Bunge hili liijadili Hoja ya Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa pamoja na taarifa hii.

Mheshimiwa Spika, mawanda ya taarifa; taarifa ya Makadirio ya Mapato na Matumizi yaliyochambuliwa inagusa Mafungu Matatu ya kibajeti ambayo ni Fungu Na. 38 - Ngome, Fungu Na. 39 - Jeshi la Kujenga Taifa, Fungu Na. 57 - Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kwa maana ya Wizara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kutambulisha mawanda ya taarifa naomba kuisoma taarifa hii kwa muhtasari ili kuendana na muda pasipo kuathiri mtiririko wa maudhui, hata hivyo umuhimu wa kumbukumbu naomba taarifa yote kama ilivyowasilishwa mezani mapema leo hii iingie kwenye Taarifa Rasmi za Bunge.

Mheshimiwa Spika, matokeo ya ukaguzi wa miradi ya maendeleo. Kwa kuzingatia masharti ya Kanuni ya 117 (1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Kamati ilitembelea na kukagua mradi wa ujenzi wa hanga la kuegesha Ndege za Jeshi Mkoani Dodoma, mradi huo ni sehemu ya miradi inayotekelezwa na Wizara hii.

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa lilitengewa kiashi cha shilingi bilioni 11 kwa ajili ya utekelezaji wa mradi wa Ujenzi wa hanga la kuegeshea ndege za Jeshi Jijini Dodoma, Dar es Salaam na Chato Mkoani Geita. Kamati ilipata fursa ya kutembelea mradi wa ujenzi wa hanga la kuhifadhia ndege za Jeshi, Dodoma. Kamati ilielezwa kuwa, mradi huo unatekelezwa na Mkandarasi M/S Simba *International Limited.*

Mheshimiwa Spika, naomba kuliarifu Bunge lako Tukufu kuhusu matokeo ya uchambuzi wa mradi huo ni kuwa kwa sasa hanga hili limekamilika kwa asilimia 93 ambapo kazi zilizobaki kukamilishwa kwa mradi huu kwa mujibu wa mkataba ni kuweka mfumo wa zimamoto, uwekaji wa ofisi *(partitioning)* na kumalizia sakafu.

Mheshimiwa Spika, maelezo ya kina kuhusu ukaguzi wa mradi huu yanapatikana katika sehemu ya pili ya taarifa ya Kamati.

Mheshimiwa Spika, uchambuzi wa taarifa ya utekelezaji wa mpango wa bajeti na uzingatiaji wa maoni ya kamati kwa mwaka wa fedha wa 2022/2023. Uchambuzi wa Kamati katika mapitio ya utekelezaji wa mpango wa bajeti ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kwa mwaka wa fedha 2022/2023, ulilenga kulinganisha makusanyo ya mapato na lengo la makusanyo hayo, upatikanaji wa fedha za matumizi kwa ajili ya shughuli zilizopangwa kutekelezwa, hususan fedha za matumizi mengineyo na upatikanaji wa fedha za Maendeleo ikilinganishwa na bajeti iliyoidhinishwa na Bunge kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023, kwa Mafungu yote Matatu ya Wizara.

Mheshimiwa Spika, kwa vile Kamati ilizingatia taarifa mbalimbali zilizowasilishwa mbele ya Kamati kwa kipindi cha Januari,

2023 na Machi, 2023 pamoja na majadiliano yaliyochangia upatikanaji wa taarifa muhimu na za ziada wakati wa vikao vya Kamati naomba kuwasilisha uchambuzi huo kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, mapitio ya utekelezaji wa ushauri wa Kamati. Wakati wa kuchambua mpango na makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara hii kwa mwaka wa fedha 2022/2023. Kamati ilishauri masuala mbalimbali yanayopaswa kufanyiwa kazi na Wizara hii, naomba kuliarifu Bunge lako kuwa, taarifa ya mtoa hoja ilionesha kwamba, Serikali imezingatia sehemu kubwa ya ushauri kama inavyoonekana katika Kiambatisho Na. 01 cha taarifa hii.

Mheshimiwa Spika, mfano wa ushauri uliozingatiwa ni kuhusu Serikali kupeleka askari wenye utaalamu unaohitajika katika Mashirika kimkakati ya Nyumbu na Mzinga.

Mheshimiwa Spika, pamoja na uzingatiaji mzuri wa ushauri, upo ushauri ambao unahitaji kufanyiwa kazi na Serikali. Mathalani, ushauri kuhusu Serikali kupitia Wizara ya Fedha kuandaa utaratibu mahsusi utakaowezesha upatikanaji wa fedha kwa ajili ya kufanya ukarabati wa nyumba za makazi ya wanajeshi pamoja na kukamilisha mchakato wa kuruhusu Jeshi kuwa na *Bonded Warehouse* yake.

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia Madaraka ya Bunge yaliyoainishwa katika Ibara ya 63 (2) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977, Kamati inaendelea kusisitiza kuwa ushauri ambao haujatekelezwa unapaswa kufanyiwa kazi na kuwa sehemu ya ratiba ya utekelezaji wa majukumu ya Wizara hii kwa mwaka wa fedha 2023/2024.

Mheshimiwa Spika, uchambuzi wa bajeti iliyoidhinishwa na Bunge kwa mwaka wa fedha 2022/2023. Kamati ilipitia taarifa ya utekelezaji wa mpango na Bajeti ya Wizara katika Kipindi cha Julai, 2022 hadi Februari, 2023, kwa kuchambua hali ya ukusanyaji wa mapato pamoja na upatikanaji wa fedha kutoka Hazina kwa kipindi hicho.

Mheshimiwa Spika, ukusanyaji wa maduhuli. Katika mwaka wa fedha 2022/2023 Wizara ilikadiria kukusanya maduhuli yenye jumla ya shilingi 87,603,000.00 kwa mafungu yote matatu. Makadirio haya yalikuwa zaidi ya lengo lililowekwa la makadirio ya makusanyo ya shilingi 85,103,000.00 kwa mwaka wa fedha 2021/2022.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa maelezo ya Wizara, hadi kufikia Februari, 2023 kiasi cha fedha za maduhuli kilichokuwa kimekusanywa kilikuwa shilingi 64,781,151.48 sawa na asilimia 73.95 ya lengo la mwaka lililopangwa. Kamati ilibaini kuwa kiasi kilichokusanywa ni pungufu kwa shilingi 22,828,348.58 sawa na asilimia 26 ikilinganishwa na makusanyo ya kipindi kama hicho kwa mwaka wa fedha 2021/2022 ambayo yalikuwa shilingi 87,676,496.06 ya lengo lililowekwa.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilibaini kuwa makusanyo hayo yamechangiwa na mafungu mawili ya Wizara ambapo Fungu 38 limekusanya asilimia 27 ya Fungu na Fungu 39 (JKT) limekusanya asilimia 37 ya kiasi kilichokusanywa. Aidha, Fungu 57 hadi kufikia mwezi Machi hakikuwa limekusanya kiasi chochote cha fedha.

Mheshimiwa Spika, vilevile Kamati ilifanya uchambuzi kwa kila Fungu na kubainisha mchanganuo wa makusanyo kwa mwaka wa fedha 2022/2023 kama inavyoonekana katika Jedwali Na. 01 na *graph* Na. 01 katika taarifa ya Kamati.

Mheshimiwa Spika, vilevile Kamati ilifanya uchambuzi na ulinganisho wa makusanyo yaliyopatikana kwa kila Fungu kufikia mwezi Februari 2023 na Makusanyo yaliyopatikana kwa kipindi kama hicho kwa mwaka 2021/2022 Kama inavyoonekana katika *graph* Na. 02 kwenye taarifa ya kamati.

Mheshimiwa Spika, baada ya kufanya uchambuzi wake, kamati imebaini yafuatayo: -

(i) Makusanyo katika Fungu 38 – Ngome yalikusudiwa kuchangia katika lengo la Wizara kwa asilimia 25 lakini katika utekelezaji Fungu hilo limechangia kwa asilimia 27 ya kiasi kilichokusanywa.

(ii) Makusanyo ya Fungu 39 yalikusudiwa kuchangia katika lengo la Wizara kwa asilimia 73.4 lakini hali halisi inaonesha kuwa makusanyo ya JKT yamechangia kwa asilimia 73 ya kiasi kilichokusanywa.

(iii) Makusanyo ya Fungu 57 – Wizara, yalikusudiwa kuchangia kwa asilimia 1.4 kwenye mapato yote ya Wizara, lakini hali halisi imeonesha Wizara haijakusanya mapato yoyote.

Mheshimiwa Spika, ulinganisho huo wa malengo ya makusanyo kwa kila Fungu ikilinganishwa na kiasi halisi kilichokusanywa, umeisaidia Kamati kubaini kuwa mwenendo wa makusanyo siyo mzuri kwani hakuna Fungu lililofikia lengo la kukusanya angalau asilimia 75 hadi kufikia mwezi Februari, 2023.

Mheshimiwa Spika, upatikanaji wa fedha kutoka Hazina. Baada ya kupokea taarifa ya wizara kuhusu utekelezaji wa bajeti kwa mwaka 2022/2023, Kamati ilitaka kujiridhisha kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kwa kufanya ulinganisho wa fedha zilizoidhinishwa na Bunge kwa ajili ya matumizi yote ya Wizara na kiasi cha fedha kilichotolewa hadi kufikia mwezi Februari, 2023.

Mheshimiwa Spika, vilevile katika kujiridhisha na uzito uliowekwa kwa wakati wa utoaji wa fedha kutoka Hazina kama uliendana na uzito uliokusudiwa na Bunge wakati wa kuidhinisha bajeti ya Wizara hii kwa mwaka wa fedha 2022/2023. Kamati ililinganisha uwiano wa bajeti za Mafungu hayo na uwiano wa fedha zilizopokelewa kwa Mafungu hayo. Ulinganisho huo unaonekanaka katika Jedwali Na. 02 na Na. 03 kwe taarifa ya kamati kupitia uchambuzi huo Kamati ilibaini mambo yafuatayo: -

(i) Hadi kufikia mwezi Februari, 2023 Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kwa Mafungu yote matatu ilipokea shilingi 1,787,960,094,970.55 sawa na asilimia 65.88 ya fedha zilizoidhinishwa.

(ii) Kati ya fedha zilizopokelewa shilingi 1,694,963,380,541.60 sawa na asilimia 94.8 ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na shilingi 92,996,714,428.91 sawa na asilimia 5.2 ni kwa ajili ya Bajeti ya Maendeleo.

(iii) Kati ya fedha zilizopokelewa Fungu 38 Ngome ilipokea asilimia 78.6, Fungu 39 JKT ilipokea asilimia 16.82 na Fungu 57 Wizara ilipokea asilimia 4.58. Kiasi cha fedha kilichopokelewa na Wizara hii kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo ni pungufu kwa shilingi 83,581,709,571.09 sawa na asilimia 47.3 ikilinganishwa na fedha zilizotolewa katika kipindi kama hicho kwa mwaka wa fedha 2021/2022 ambapo kwa kipindi kama hicho ilipokea shilingi 176,578,424,000.

(iv) Kati ya shilingi 92,996,714,424.91 zilizopokelewa kwa ajili ya miradi ya maendeleo, asilimia 18.28 ni kwa ajili ya Fungu 38, asilimia 7.52 ni kwa ajili ya Fungu 39 na asilimia 74.2 ni kwa ajili ya Fungu 57. Kati ya fedha zilizoidhinishwa kwa kila Fungu kwa ajili ya miradi ya maendeleo. Fungu 38 Ngome ilipokea shilingi 17,000,000,000 sawa na asilimia 30.16 ya shilingi 56,367,636,000 zilizoidhinishwa kwa ajili ya miradi ya maendeleo ya Fungu hilo.

(v) Fungu 39 JKT ilipokea shilingi 7,000,000,000 sawa na asilimia 51.24 ya shilingi 13,965,535,000 zilizoidhinishwa kwa ajili ya miradi ya maendeleo.

(vi) Fungu 57 Wizara, ilipokea shilingi 68,996,714,428.91 sawa na asilimia 43.12 ya shilingi 160,000,000,000 ya fedha zilizoidhinishwa kwa ajili ya miradi ya maendeleo kwa Fungu hilo.

Mheshimiwa Spika, uchambuzi huo unaonesha kuwa Serikali ilizingatia uzito uliotolewa na Bunge wakati wa kuidhinisha bajeti ya Wizara hii. Mathalani, Bunge liliidhinisha bajeti ya Fungu 38 ikiwa ni

asilimia 77.53 ya Bajeti yote ya Wizara na fedha zilizopokelewa na Fungu hilo ni asilimia 78.6 ya fedha zote zilizopokelewa na Wizara hadi kufikia mwezi Februari, 2023.

Mheshimiwa Spika, Fungu 39 liliidhinishiwa asilimia 15.69 ya bajeti yote ya Wizara na fedha zilizopokelewa na Fungu hilo hadi kufikia Februari, 2023 ni asilimia 16.82 ya fedha zote zilizopokelewa na Wizara, Fungu 51 ilitengewa asilimia 6.78 ya bajeti yote ya Wizara, hadi kufikia Februari, 2022 ilikuwa imepokea asilimia 4.58 ya fedha zote zilizopokelewa na Wizara.

Mheshimiwa Spika, kwa mwenendo huu, Kamati inaipongeza Serikali kutoa uzito stahiki kwa Bajeti ya Ngome na Jeshi la Kujenga Taifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pamoja na mtiririko huo mzuri wa upatikanaji wa fedha, Kamati haijaridhishwa na mtiririko wa fedha za maendeleo kwa Mafungu yote ya Wizara hii ambapo hadi kufikia mwezi Februari, 2023 Fungu 38 Ngome lilikuwa limepokea asilimia 30.16 tu ya fedha zilizoidhinishwa, Fungu 39 JKT lilikuwa limepokea asilimia 51.24 ya fedha zilizoidhinishwa na Fungu 51 Wizara lilikuwa limepokea asilimia 43.12 ya fedha iliyoidhinishwa kwa ajili ya miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Spika, Wizara hii ina majukumu mazito na muhimu kwa nchi, hivyo kutokutolewa kwa fedha za miradi ya maendeleo kwa wakati kunaathiri mipango ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, uchambuzi wa mpango wa bajeti na makadirio ya mapato na matumizi kwa mwaka wa fedha 2023/2024. Mpango wa utekelezaji wa majukumu ya Wizara kwa mwaka wa fedha 2023/2024

Mheshimiwa Spika, ili kujiridhisha na makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara hii kwa mwaka wa fedha 2023/2024. Kamati ilipitia majukumu makuu ya Wizara na kubaini kuwa makadirio ya

mapato na matumizi yanayopendekezwa yanalenga kuimarisha utendaji kazi na ufanisi wa Wizara katika utekelezaji wa majukumu hayo kulingana na dira na dhima ya Wizara.

Mheshimiwa Spika, lengo hili limepangwa kufikiwa kwa kutekeleza majukumu sita, likiwemo kuliongezea uwezo wa kimedani Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania kwa kulipatia vifaa na zana bora, mafunzo na mazoezi, kuboresha mazingira ya kufanyia kazi ikiwemo makazi na kuimarisha upatikanaji wa huduma stahiki kwa mahitaji ya msingi kwa wanajeshi na watumishi wa umma pamoja kuwapa viijana wa Kitanzania mafunzo ya awali ya kijeshi na stadi za kazi ili kuwajengea ukakamavu, uzalendo, umoja wa kitaifa na uwezo wa kujitegemea.

Mheshimiwa Spika, uchambuzi wa Kamati umeonesha kuwa, majukumu yaliyopangwa yatawezesha kufikiwa kwa malengo sita ya Wizara hii kwa ufanisi zaidi endapo Serikali itazingatia mpango na makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara kwa kutoa fedha zitakazoidhinishwa na Bunge kwa ukamilifu na kwa wakati kwa kuzingatia mpango kazi wake.

Mheshimiwa Spika, uchambuzi wa makadirio ya mapato kwa mwaka 2023/2024. Kwa mwaka wa fedha 2023/2024, Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, kwa mafungu yote matatu Fungu Na. 38, Fungu Na. 39 na Fungu Na. 57 inategemea kukusanya mapato ya jumla ya shilingi 87,603,000. Kiasi hiki ni sawa na kiasi kilichopangwa kukusanywa katika mwaka wa fedha 2022/2023, mchanganuo wa lengo hilo la makusanyo na sura ya mchanganuo wake inaonekana katika Jedwali Na. 03. Na Jedwali Na. 04 ya taarifa ya Kamati.

Mheshimiwa Spika, kwa uchambuzi huo, Kamati imebaini mambo yafuatayo: -

(i) Lengo la makusanyo kwa mafungu yote ya Wizara hii ni sawa na lengo la makusanyo kwa mwaka wa fedha unaoishia 2022/2023

(ii) Fungu 38 Ngome linategemewa katika makusanyo kwa kiasi cha asilimia 25.11

(iii) Fungu 39 JKT linategemewa katika makusanyo kwa kiasi cha asilimia 73.52.

(iv) Fungu 57 Wizara linategemewa kwa makusanyo kwa kiasi cha asilimia 1.37.

Mheshimiwa Spika, kwa maelezo hayo ni matumaini ya Kamati kuwa Wizara imeweka lengo linalofikika kwa kuzingatia changamoto zilizojitokeza katika ukusanyaji wa maduhuli kwa mwaka wa fedha 2022/2023.

Mheshimiwa Spika, uchambuzi wa makadirio ya matumizi. Maelezo yaliyotolewa na Wizara mbele ya Kamati yalibainisha kuwa katika mwaka wa fedha 2023/2024, bajeti ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa inayoombwa kwa Mafungu yote matatu ni shilingi 2,893,846,897,000. Kati ya fedha hizo shilingi 2,671,013,726,000 sawa na asilimia 92.3 ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na shilingi 222,833,171,000 sawa na asilimia 7.7 ni kwa ajili ya miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Spika, ili kukidhi mantiki ya masharti ya Kanuni ya 117 (2) ya Kanuni za Bunge, Kamati ilifanya uchambuzi wa makadirio hayo kwa kupitia kasma, vifungu na mafungu yote ikilinganishwa na Bajeti iliyoidhinishwa na kutekelezwa katika mwaka wa fedha 2022/2023, katika uchambuzi wake, Kamati imebaini mambo yafuatayo: -

(i) Bajeti ya Wizara hii kwa mwaka wa fedha 2023/2024 imeongezeka kwa shilingi 180,059,491,547 ikilinganishwa na bajeti ya mwaka wa fedha 2022/2023. Tofauti hiyo ni ongezeko la 6.63%. Kamati inaipongeza Serikali kwa kuzingatia ushauri wa Kamati wa kuongeza kiwango cha bajeti ya Wizara hii na vyombo vyake vyote inavyovisimamia;

(ii) Kiasi cha fedha kinachoombwa kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo kimepungua kwa shilingi 7,500,000,000 ambayo ni sawa na 3.3% ikilinganishwa na kiwango kilichotengwa katika mwaka wa fedha 2022/2023. Fedha hizi zimepungua katika Fungu 38 (Ngome) kwa asilimia 13.3 ambapo katika Fungu 39 (JKT) na Fungu 57 (Wizara) hakuna tofauti;

(iii) Kati ya shilingi 222,833,171,000 zinazoombwa kwa ajili ya kugharamia shughuli za Maendeleo, 22% ni kwa ajili ya Fungu 38 - Ngome, 6% ni kwa ajili ya Fungu 39- JKT na 27% ni kwa ajili ya Fungu 57- Wizara.

Mheshimiwa Spika, naomba Bunge lako Tukufu lipokee maelezo hayo yatakayosaidia majadiliano kuhusu hoja iliyowasilishwa na Waziri wa Ulinzi, Jeshi la Kujenga Taifa kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara yake kwa mwaka ujao wa fedha.

Mheshimiwa Spika, kutokana na uchambuzi kama nilivyoeleza, Kamati inayo maoni yanayojenga msingi wa ushauri nitakaotoa. Naomba kubainisha maoni hayo kama ifuatavyo:-

(i) Utoaji wa fedha za miradi ya maendeleo katika Wizara hii kwa mtiririko uliopangwa ni jambo linapaswa kupewa kipaumbele kuendelea na malengo yaliyokusudiwa wakati Bunge linaidhinisha fedha hii;

(ii) Kukosekana kwa *bonded warehouse* ya Jeshi kunasababisha Jeshi kutumia gharama kubwa katika kuhifadhi mizigo Bandarini;

(iii) Baadhi ya vifaa na mashine kwa ajili ya matumizi ya jeshi vimekuwa vikitozwa Kodi mbalimbali kwa mujibu wa Sheria. Hali hii husababisha jeshi kutumia fedha nyingi kulipa kodi wakati vifaa hivyo ni kwa ajili ya matumizi ya jeshi katika kutekeleza majukumu yake kwa mujibu wa Katiba na Sheria;

(iv) Uzingatiaji wa ushauri wa Kamati kuhusu Sera ya Ulinzi wa Taifa kwa kipindi tofauti, umefikia hatua ya kuhitaji kuwekwa katika utekelezaji. Hivyo, ukamilishaji wa Sera ya Ulinzi wa Taifa ni jambo linalopaswa kupewa kipaumbele katika mwaka wa fedha 2023/2024;

(v) Kuimarisha mipaka yetu ili kudhibiti mianya ya njia zisizo rasmi ni suala linalopaswa kuendelea kupewa kipaumbele. Aidha, katika kudhibiti mianya ya mipaka inayoweza kutumiwa isivyostahili, Serikali iendelee kuboresha utaratibu wa jambo hilo;

(vi) Maeneo mengi ya Wizara hii hayajapimwa na kupata Hati. Hali hii huchangia kuwavutia wananchi kufanya shughuli zao katika maeneo hayo na baadaye kuibuka kwa migogoro isiyo na sababu; na

(vii) Nyumbu na Mzinga ni mashirika ya kimkakati. Uboreshaji wa miundombinu na teknolojia kwa mashirika haya ili uwe na tija ni vema ikama ya watumishi ikazingatiwa kwa kuzingatia malengo yaliyowekwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kutokana na maoni hayo, Kamati inashauri yafuatayo:-

(i) Serikali iendelee kutoa kipaumbele na kuipa uzito unaostahili wa kibajeti miradi ya Wizara ili kupata tija iliyokusudiwa kwa maslahi mapana ya wananchi na na Taifa kwa ujumla; *(Makofi)*

(ii) Serikali ione umuhimu wa kutoa fedha za maendeleo kwa Fungu 38 - Ngome kwa mtiririko uliopangwa. Aidha, Serikali itoe kwa ukamilifu fedha zote za maendeleo ambazo bado hazijatolewa kwa Fungu 57 - Wizara na Fungu 39 - JKT ili kutoathiri utekelezaji wa shughuli zilizopangwa;

(iii) Mamlaka ya Mapato *(TRA)* pamoja na Mamlaka nyingine zinazohusika ziidhinishe maombi ya Jeshi kutumia *Bonded*

*Warehouse* zake. Kufanya hivyo kutasaidia jeshi kuepuka gharama kubwa inazotumia kuhifadhi mizigo bandarini *(demurrage charges);*

(iv) Serikali ifanye mapitio ya Sheria za Kodi zinazotoza vifaa vya jeshi kodi ili kuondoa utaratibu huo na kuweka utaratibu mzuri wa kutoa msamaha kwa vifaa vyote vinavyoingizwa kwa ajili ya matumizi ya Jeshi. Naomba kurudia hapa. Serikali ifanye mapitio ya Sheria za Kodi zinazotoza vifaa vya jeshi kodi ili kuondoa utaratibu huo na kuweka utaratibu mzuri wa kutoa msamaha kwa vifaa vyote vinavyoingizwa kwa ajli ya matumizi ya jeshi; *(Makofi)*

(v) Katika mwaka wa fedha 2023/2024 Serikali ikamilishe upatikanaji wa Sera ya Taifa ya Ulinzi *(The National Defence Policy)* kwa umuhimu wake kwa Taifa kama ambavyo imekuwa ikishauriwa vipindi tofauti tangu Bunge la Tisa;

(vi) Serikali iendelee kuchukua hatua madhubuti za kuimarisha miundombinu ya kiulinzi na kudhibiti mianya ya njia zisizo rasmi katika mipaka yetu. Kufanya hivyo kutawezesha kudhibiti vitendo visivyo na afya kwa Taifa;

(vii) Wizara iongeze kasi ya utekelezaji wa mkakati wa kupima na kupata Hati za maeneo yote ambayo hayajapimwa. Kufanya hivyo kutawezesha maeneo ya Wizara kutambulika rasmi na hivyo kuepuka migogoro isiyo na lazima na wananchi;

(viii) Uimarishaji wa Mashirika ya Mzinga na Nyumbu uende sambamba na kuongeza rasilimaliwatu kwa kuzingatia mahitaji ya Mashirika hayo. Kufanya hivyo kutaimarisha utendaji wa kazi za mashirika hayo na hivyo kufikia malengo yaliyokusudiwa; na

(ix) Wizara iendelee kutekeleza maoni na mapendekezo ya Kamati yaliyotolewa katika vipindi mbalimbali ambayo hayajatekelezwa hususan katika Bajeti za miaka mitatu iliyopita ya 2020/2021, 2021/2022 na 2022/2023.

Mheshimiwa Spika, mwisho, napenda kukushukuru kwa kunipa nafasi kwa ajili ya kuwasilisha Taarifa hii. Aidha, kipekee nawashukuru Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama ambao maoni, ushauri na ushirikiano wao umewezesha kukamilika kwa taarifa hii. Naomba majina yao yaingie katika Taarifa Rasmi za Bunge.

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Wajumbe wa Kamati, napenda kutumia fursa hii kumshukuru Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, Mheshimiwa Innocent Bashungwa, Mbunge kwa ushirikiano wake mzuri katika kipindi chote cha utekelezaji wa majukumu ya kikanuni ya Kamati. Aidha, namshukuru Katibu Mkuu Dkt. Faraji Mnyepe pamoja na Watendaji wote wa Wizara kwa ushirikiano wao.

Mheshimiwa Spika, vilevile napenda kumshukuru Katibu wa Bunge Ndg. Nenelwa J. Mwihambi, *ndc*. kwa kuratibu vyema shughuli za Kamati na Bunge. Aidha, nawashukuru Kaimu Mkurugenzi wa Idara ya Kamati za Bunge Ndg. Michael Chikokoto, Mkurugenzi Msaidizi Ndg. Gerald Magili na Makatibu wa Kamati, Ndugu Omary Magwinza na Bi. Victoria Mizengo wakisaidiwa na Bi. Rehema Kimbe kwa kuratibu vyema shughuli za Kamati na kuhakikisha Taarifa hii inakamilika kwa wakati.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo, sasa naliomba Bunge lako Tukufu lipokee Taarifa hii na likubali kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024 kama yalivyowasilishwa na mtoa hoja.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. Naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**24 MEI, 2023**

**TAARIFA YA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA MAMBO YA NJE, ULINZI NA USALAMA KUHUSU UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YA WIZARA YA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA (FUNGU 38, 39, 57) KWA MWAKA WA FEDHA 2022/2023; PAMOJA NA MAONI YA KAMATI KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NAMATUMIZI YA WIZARA HIYO KWA MWAKA WA FEDHA 2023/2024 – KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

## SURA YA KWANZA

### 1.0 UTANGULIZI

**Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa Kanuni ya 118 (9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023, naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama kuhusu utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023, pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024 na kuliomba Bunge lako Tukufu liipokee Taarifa hii na kuikubali, kisha kuidhinisha Bajeti ya Wizara hiyo.

**Mheshimiwa Spika**, msingi wa taarifa hii ni majukumu ya Kamati kwa mujibu wa Kifungu cha 6 (3) na Kifungu cha 7 (1) (a), cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Bunge pamoja na masharti ya Kanuni ya 118 (4) ya Kanuni za Bunge. Kwa mujibu wa Kanuni hizo, kabla ya taarifa ya utekelezaji na Makadirio ya Matumizi ya Wizara ya Ulinzi na JKT, kujadailiwa Bungeni, zilipaswa kuchambuliwa na Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama. Naomba kulijulisha Bunge lako tukufu kuwa uchambuzi huo ulifanyika tarehe 22 Machi, 2023 baada ya ziara za ukaguzi wa miradi ya maendeleo inayotekelezwa chini ya Wizara hii kama ilivyoelekeza Kanuni ya 117 (1) hadi 117 (2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge.

**Mheshimiwa Spika,** kwa madhumuni ya kuweka bayana mawanda ya Taarifa hii, nitangulie kulikumbusha Bunge hili kuwa Wizara ya Ulinzi na JKT inajumuisha Mafungu Matatu (3) ya Kibajeti yafuatayo: -

a) Fungu 38 - Ngome;

b) Fungu 39 - Jeshi la Kujenga Taifa; na
c) Fungu 57 – Wizara

**Mheshimiwa Spika**, ili kuliwezesha Bunge lako Tukufu kufuatilia ipasavyo utekelezaji wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023, pamoja na kuishauri vema Serikali kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024, Taarifa hii imegawanyika katika Sehemu Kuu sita (6) zifuatazo: -

Sehemu ya kwanza; ikiwa ni sehemu ya utangulizi; Sehemu hiyo inatoa maelezo ya jumla kuhusu msingi na muundo wa Taarifa. Sehemu ya Pili inafafanua matokeo ya ukaguzi wa miradi ya Maendeleo uliofanyika kwa mujibu wa Kanuni ya 117 (1) ya Kanuni za Bunge. Na sehemu ya tatu hadi ya nne zinafanya uchambuzi wa Utekelezaji wa mipango na Bajeti kwa mwaka wa fedha 2022/2023 pamoja na kuchanganua Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hii kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024.

**Mheshimiwa Spika,** Sehemu ya tano inaonesha Maoni na Ushauri wa Kamati kutokana na matokeo ya Uchambuzi. Aidha, sehemu ya sita na ya mwisho inakamilisha taarifa kwa kutoa shukurani na kulishauri Bunge kuhusu Hoja ya Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, juu ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hii kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024.

## SURA YA PILI

## 2.0 MATOKEO YA UKAGUZI WA MIRADI YA MAENDELEO

**Mheshimiwa Spika**, kwa kuzingatia masharti ya Kanuni ya 117 (1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Kamati ilitembelea na kukagua Mradi wa Ujenzi wa Hanga la kuegesha Ndege za Jeshi Mkoani Dodoma. Mradi huo ni sehemu ya miradi inayotekelezwa na Wizara hii.

**Mheshimiwa Spika,** Sehemu ya Taarifa hii inaeleza mambo makuu mawili yafuatayo: -

a) Muhtasari wa maelezo ya miradi iliyotembelewa na kukaguliwa katika Mwaka wa Fedha 2022/2023; na

b) Uchambuzi wa taarifa ya utekelezaji wa miradi hiyo.

**Mheshimiwa Spika**, Lengo la sehemu hii ni kuliwezesha Bunge kufuatilia hali ya utekelezaji na upatikanaji wa Fedha ilizo ziidhinisha na kupata mantiki ya uamuzi wake wakati wa kujadili makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara hii.

## 2.1 Muhtasari wa Maelezo kuhusu Mradi wa Maendeleo uliokaguliwa

**Mheshimiwa Spika**, maelezo kuhusu mradi uliokaguliwa ni kama ifuatavyo: -

### 2.1.1 Mradi wa ujenzi wa Hanga la kuegesha Ndege za Jeshi - Dodoma

**Mheshimiwa Spika,** Wizara ya Ulinzi na JKT ilitengewa kiasi cha **Shilingi 11,000,000,000** kwa ajili ya utekelezaji wa mradi wa Ujenzi wa Hanga la Kuegeshea Ndege za Jeshi Jijini Dodoma, Dar es Salaam na Chato mkoani Geita. Kamati ilipata fursa ya kutembelea mradi wa ujenzi wa Hanga la Kuhifadhia Ndege za Jeshi, Dodoma. Kamati ilielezwa kuwa, mradi huo unatekelezwa na Mkandarasi M/S Simba International Limited.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilielezwa kuwa Mradi wa Ujenzi wa Hanga la Kuegesha Ndege za Jeshi, Dodoma ulianza kujengwa tarehe 01 Agosti, 2021 na ulitarajiwa kukamilika tarehe 18 Machi, 2023.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inaipongeza Serikali kwa kuona umuhimu wa kujenga Hanga la kuhifadhi Ndege za Jeshi katika uwanja wa Dodoma. Hatua hii ni muhimu kwani inaliwezesha Jeshi kuhifadhi ndege zake kwa usalama zaidi.

### *2.2 Matokeo ya Ukaguzi*

**Mheshimiwa Spika**, baada ya muhtasari wa mradi wa maendeleo uliokaguliwa, sasa naomba kuliarifu Bunge lako Tukufu kuhusu matokeo ya ukaguzi wa mradi huo kuwa kwa sasa Hanga hili limekamilika kwa asilimia 93; ambapo kazi zilizobaki kukamilisha mradi huu kwa mujibu wa Mkataba ni mfumo wa zimamoto, uwekaji wa ofisi *(partitioning)* na umaliziaji (*finishing)* wa sakafu.

### *2.3 Maoni ya Jumla kuhusu Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023*

**Mheshimiwa Spika**, kutokana na matokeo ya ziara za ukaguzi wa miradi ya maendeleo, Kamati ina maoni kuwa, Serikali iendelee kutoa kipaumbele na kuipa uzito unaostahili kibajeti miradi ya Wizara hii kutokana na umuhimu wake.

## SURA YA TATU

### 3.0 UCHAMBUZI WA TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA MPANGO WA BAJETI NA UZINGATIAJI WA MAONI YA KAMATI KWA MWAKA WA FEDHA 2022/2023

**Mheshimiwa Spika,** uchambuzi wa Kamati katika Mapitio ya Utekelezaji wa Mpango wa Bajeti ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023, ulilenga kulinganisha Makusanyo ya Mapato na lengo la Makusanyo hayo, upatikanaji wa fedha za matumizi kwa ajili ya shughuli zilizopangwa kutekelezwa, hususan fedha za Matumizi Mengineyo na upatikanaji wa fedha za Maendeleo ikilinganishwa na bajeti iliyoidhinishwa na Bunge kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023, kwa mafungu yote Matatu ya Wizara.

**Mheshimiwa Spika**, vilevile Kamati ilizingatia taarifa mbalimbali zilizowasilishwa mbele ya Kamati kwa kipindi cha Januari, 2023 na Machi, 2023 pamoja na majadiliano yaliyochangia upatikanaji wa taarifa muhimu na za ziada wakati wa vikao vya Kamati.

**Mheshimiwa Spika,** naomba kuwasilisha uchambuzi huo kama ifuatavyo: -

### *3.1 Mapitio ya utekelezaji wa ushauri wa Kamati*

**Mheshimiwa Spika,** wakati wa kuchambua Mpango na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hii kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023, Kamati ilishauri masuala mbalimbali yanayopaswa kufanyiwa kazi na Wizara hii. Naomba kuliarifu Bunge lako kuwa, taarifa ya mtoa hoja ilionesha kwamba, Serikali imezingatia sehemu kubwa ya ushauri kama inavyoonekana katika **Kiambatisho Na. 1** cha Taarifa hii.

Mfano wa ushauri uliozingatiwa ni kuhusu Serikali kupeleka askari wenye utaalamu unaohitajika katika Mashirika kimkakati ya NYUMBU na MZINGA. Kamati imeridhishwa na namna serikali ilivyozingatia na kutekeleza ushauri huu.

**Mheshimiwa Spika**, pamoja na uzingatiaji mzuri wa ushauri, upo ushauri ambao unahitaji kufanyiwa kazi na Serikali. Mathalani, ushauri kuhusu Serikali kupitia Wizara ya Fedha kuandaa utaratibu mahsusi utakaowezesha upatikanaji wa fedha kwa ajili ya kufanya ukarabati wa nyumba za makazi ya Wanajeshi pamoja na kukamilisha mchakato wa kuruhusu Jeshi kuwa na "*Bonded Warehouse*" yake.

**Mheshimiwa Spika**, kwa kuzingatia Madaraka ya Bunge yaliyoainishwa katika Ibara ya 63 (2) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977, Kamati inaendelea kusisitiza kuwa ushauri ambao haujatekelezwa unapaswa kufanyiwa kazi na kuwa sehemu ya ratiba ya utekelezaji wa majukumu ya Wizara hii kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024.

### *3.2 Uchambuzi wa Bajeti iliyoidhinishwa na Bunge kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023*

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilipitia Taarifa ya utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Wizara katika Kipindi cha Julai, 2022 hadi Februari, 2023 kwa kuchambua hali ya ukusanyaji wa mapato pamoja na upatikanaji wa fedha kutoka Hazina kwa kipindi hicho.

#### 3.2.1 Ukusanyaji wa Maduhuli

**Mheshimiwa Spika,** katika Mwaka wa Fedha 2022/2023, Wizara ilikadiria kukusanya maduhuli yenye jumla ya **Shilingi 87,603,000.00** kwa Mafungu yote matatu (3). Makadirio haya yalikuwa zaidi ya lengo lililowekwa la Makadirio ya makusanyo ya **Shilingi 85,103,000.00** kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022.

**Mheshimiwa Spika,** kwa mujibu wa maelezo ya Wizara, hadi kufikia Mwezi Februari, 2023 kiasi cha fedha za maduhuli kilichokuwa kimekusanywa kilikuwa **Shilingi 64,781,151.48** sawa na **asilimia 73.95** ya lengo la mwaka lililopangwa. Kamati ilibaini kuwa kiasi kilichokusanywa ni pungufu kwa **Shilingi 22,821,848.52** sawa na **asilimia 26** ikilinganishwa na makusanyo ya kipindi kama hicho kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022 ambayo yalikuwa **Shilingi 87,679,496.06** ya lengo lililowekwa.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilibaini kuwa makusanyo hayo yamechangiwa na Mafungu mawili ya Wizara ambapo; Fungu 38 (Ngome) limekusanya **asilimia 27** na Fungu 39 (JKT) limekusanya **asilimia 73** ya kiasi kilichokusanywa.

Aidha, Fungu 57 (Wizara) hadi kufikia Mwezi Machi halikuwa limekusanya kiasi chochote cha Fedha.


**Mheshimiwa Spika**, vilevile Kamati ilifanya uchambuzi kwa kila Fungu na kubainisha mchanganuo wa makusanyo kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023 kama inavyoonekana katika **Jedwali Na. 01** na **Grafu Na. 01** hapa chini.

**Jedwali Na. 1: Mchanganuo wa Makadirio na Makusanyo ya Mapato**

| FUNGU | MAKADIRIO | MAKUSANYO | % YA JUMLA YA LENGO | % YA JUMLA YA MAKUSANYO |
|---|---|---|---|---|
| 38 - Ngome | 22,000,000.00 | 17,281,151.48 | 25 | 27 |
| 39 - JKT | 64,403,000.00 | 47,500,000.00 | 73.4 | 73 |
| 57 - Wizara | 1,200,000.00 | 0.00 | 1.4 | 0.00 |

Chanzo: Randama ya Wizara 2022/2023


**Grafu Na. 1: Ulinganisho wa lengo na Makusanyo halisi ya Mapato**




**Chanzo: Randama ya Wizara 2022/2023**

**Mheshimiwa Spika**, vilevile Kamati ilifanya uchambuzi na ulinganisho wa Makusanyo yaliyopatikana kwa kila Fungu kufikia Mwezi Februari, 2023 na Makusanyo yaliyopatikana katika kipindi kama hicho katika Mwaka 2021/2022 kama inavyoonekana katika **Grafu na 2** hapa chini:-

**Grafu Na. 2: Ulinganisho wa Makusanyo 2021/2022 na 2022/2023**




| | FUNGU 38 NGOME | FUNGU 39 JKT | FUNGU 57 WIZARA |
|---|---|---|---|
| 2021/2022 | 31,405,466.00 | 54,292,000.00 | 1,982,030.06 |
| 2022/2023 | 17,281,151.48 | 47,500,000.00 | 0.00 |

*Chanzo: Randama za Wizara 2021/2022 na 2022/2023*

**Mheshimiwa Spika**, Baada ya kufanya Uchambuzi wake, Kamati imebaini kuwa:-

i) **Makusanyo katika Fungu 38 – Ngome** yalikusudiwa kuchangia katika lengo la Wizara kwa **asilimia 25** lakini katika utekelezaji Fungu hilo limechangia kwa **asilimia 27** ya kiasi kilichokusanywa.

ii) **Makusanyo ya Fungu 39 –JKT** yalikusudiwa kuchangia katika lengo la Wizara kwa **asilimia 73.4,** lakini hali halisi imeonesha

kuwa makusanyo ya JKT yamechangia kwa **asilimia 73** ya kiasi kilichokusanywa.

iii) **Makusanyo ya Fungu 57 – Wizara**, yalikusudiwa kuchangia kwa **asilimia 1.4** kwenye mapato yote ya Wizara, lakini hali halisi imeonesha Wizara haijakusanya mapato yoyote.

**Mheshimiwa Spika,** ulinganisho huo wa malengo ya makusanyo kwa kila Fungu ikilinganishwa na kiasi halisi kilichokusanywa, umeisaidia Kamati kubaini kuwa mwenendo wa makusanyo si mzuri kwani hakuna Fungu lililofikia lengo la kukusanya angalau **asilimia 75** hadi kufikia Mwezi Februari, 2023.

### 3.2.2 Upatikanaji wa Fedha Kutoka Hazina

**Mheshimiwa Spika,** Baada ya kupokea Taarifa ya Wizara kuhusu utekelezaji wa Bajeti kwa Mwaka 2022/2023, Kamati ilitaka kujiridhisha kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kwa kufanya ulinganisho wa fedha zilizoidhinishwa na Bunge kwa ajili ya matumizi yote ya Wizara na kiasi cha Fedha kilichotolewa hadi kufikia Mwezi Februari, 2023.

**Mheshimiwa Spika**, vilevile katika kujiridhisha na uzito uliowekwa wakati wa utoaji wa fedha kutoka Hazina kama uliendana na uzito uliokusudiwa na Bunge wakati wa kuidhinisha Bajeti ya Wizara hii kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023, Kamati ililinganisha uwiano wa Bajeti za Mafungu hayo na uwiano wa fedha zilizopokelewa kwa Mafungu hayo. Ulinganisho huo unaonekanaka katika **Jedwali Na. 02** na **03** hapa chini.

**Jedwali Na. 2: Ulinganisho wa fedha zilizoidhinishwa na zilizopokelewa miongoni mwa Fungu 38, Fungu 39 na Fungu 57**

| Fungu | Fedha zilizoidhinishwa | Asilimia ya fedha zilizoidhimish wa kiuwiano | Fedha zilizopokele wa | Asilimia ya fedha zilizopokele wa | Asilimia ya fedha zilizopokele wa kiuwiano |
|---|---|---|---|---|---|

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| 38 | 2,104,091,139,453 | 77.53 | 1,405,231,972,409.8 | 66.78 | 78.6 |
| 39 | 425,829,176,000 | 15.69 | 300,887,636,984.62 | 70.66 | 16.82 |
| 57 | 183,867,090,000 | 6.78 | 81,840,485,576.13 | 44.5 | 4.58 |
| | **2,713,787,405,453.00** | **100** | **1,787,960,094,970.6** | | **100** |

**Chanzo: Randama ya Wizara 2022/2023**

**Jedwali Na. 3: Ulinganisho wa fedha za maendeleo zilizoidhinishwa na zilizopokelewa miongoni mwa Fungu 38, Fungu 39 na Fungu 57**

| Fungu | Fedha zilizoidhinishwa | Asilimia ya fedha zilizoidhinishwa kiuwiano | Fedha zilizopokelewa | Asilimia ya fedha zilizopokelewa | Asilimia ya fedha zilizopokelewa |
|---|---|---|---|---|---|
| 38 | 56,367,636,000.00 | 24.47 | 17,000,000,000.00 | 30.16 | 18.28 |
| 39 | 13,965,535,000.00 | 6.06 | 7,000,000,000.00 | 51.24 | 7.52 |
| 57 | 160,000,000,000.00 | 69.47 | 68,996,714,428.91 | 43.12 | 74.2 |
| | **230,333,171,000.00** | **100** | **92,996,714,428.91** | | **100** |

Kupitia uchambuzi huo Kamati ilibaini mambo yafuatayo: -

i) Hadi kufikia Mwezi Februari, 2023 Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kwa Mafungu yote matatu imepokea **Shilingi 1,787,960,094,970.55** sawa na **asilimia 65.88** ya fedha zilizoidhinishwa.

ii) Kati ya fedha zilizopokelewa Shilingi **1,694,963,380,541.60** sawa na asilimia **94.8** ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na **Shilingi 92,996,714,428.91** sawa na **asilimia 5.2** ni kwa ajili ya Bajeti ya Maendeleo.

iii) Kati ya fedha zilizopokelewa; Fungu 38 (Ngome) limepokea **asilimia 78.6**, Fungu 39 (JKT) limepokea **asilimia 16.82** na Fungu 57 (Wizara) limepokea **asilimia 4.58.** iv) Kiasi cha fedha kilichopokelewa na Wizara hii kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo ni pungufu kwa **Shilingi 83,581,709,571.09** sawa na **asilimia 47.3** ikilinganishwa na Fedha zilizotolewa katika kipindi kama hicho katika Mwaka wa Fedha 2021/2022 ambapo kwa kipindi kama hicho ilipokea shilingi **176,578,424,000.**

v) Kati ya **Shilingi 92,996,714,428.91** zilizopokelewa kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo, **asilimia 18.28** ni kwa ajili ya Fungu 38 (Ngome), **asilimia 7.52** ni kwa ajili ya Fungu 39 (JKT) na **asilimia 74.2** ni kwa ajili ya Fungu 57 (Wizara).

vi) Katika Fedha zilizoidhinishwa kwa kila Fungu kwa ajili ya miradi ya maendeleo, Fungu 38 (Ngome) limepokea **Shilingi 17,000,000,000** sawa na **asilimia 30.16** ya Shilingi **56,367,636,000** zilizoidhinishwa kwa ajili ya miradi ya maendeleo ya Fungu hilo.

vii) Fungu 39 (JKT) lilipokea **Shilingi 7,000,000,000** sawa na **asilimia 51.24** ya **Shilingi 13,965,535,000** zilizoidhinishwa kwa ajili ya miradi ya maendeleo ya Fungu hilo;

viii) Fungu 57 (Wizara) limepokea **Shilingi 68,996,714,428.91** sawa na **asilimia 43.12** ya **Shilingi 160,000,000,000** ya fedha zilizoidhinishwa kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo kwa Fungu hilo.

**Mheshimiwa Spika**, uchambuzi huo unaonesha kuwa Serikali ilizingatia uzito uliotolewa na Bunge wakati wa kuidhinisha Bajeti ya Wizara hii. Mathalani, Bunge liliidhinisha bajeti ya Fungu 38 (Ngome) ikiwa ni **asilimia 77.53** ya Bajeti yote ya Wizara na fedha zilizopokelewa na Fungu hilo ni **asilimia 78.6** ya fedha zote zilizopokelewa na Wizara hadi kufikia Mwezi Februari, 2023;

Fungu 39 liliidhinishiwa **asilimia 15.69** ya bajeti yote ya Wizara na fedha zilizopokelewa na Fungu hilo hadi kufikia Februari, 2023 ni **asilimia 16.82** ya fedha zote zilizopokelewa na Wizara; na Fungu 51 ilitengewa **asilimia 6.78** ya bajeti yote ya Wizara, hadi kufikia Februari 2022 ilikuwa imepokea **asilimia 4.58** ya fedha zote zilizopokelewa na Wizara.

Kwa mwenendo huu, Kamati inaipongeza Serikali kutoa uzito stahiki kwa Bajeti ya Ngome na Jeshi la Kujenga Taifa.

**Mheshimiwa Spika,** pamoja na mtiririko huo mzuri wa upatikanaji wa fedha, Kamati haijaridhishwa na mtiririko wa fedha za maendeleo kwa Mafungu yote ya Wizara hii ambapo hadi kufikia Mwezi Februari, 2023 Fungu 38 (Ngome) lilikuwa limepokea **asilimia 30.16** ya fedha zilizoidhinishwa, Fungu 39 (JKT) lilikuwa limepokea **asilimia 51.24** ya fedha zilizoidhinishwa na Fungu 51 (Wizara) lilikuwa limepokea **asilimia 43.12** ya fedha iliyoidhinishwa kwa ajili ya miradi ya maendeleo.

**Mheshimiwa Spika,** kutokutolewa kwa fedha za miradi ya maendeleo kwa wakati kunaathiri mipango ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo.

## SURA YA NNE

## 4.0 UCHAMBUZI WA MPANGO WA BAJETI NA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2023/2024

### *4.1 Mpango wa Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024*

**Mheshimiwa Spika,** ili kujiridhisha na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hii kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024, Kamati ilipitia majukumu makuu ya Wizara na Kubaini kuwa makadirio ya mapato na matumizi yanayopendekezwa yanalenga kuimarisha utendaji kazi na ufanisi wa Wizara katika utekelezaji wa majukumu hayo kulingana na Dira na Dhima ya Wizara.

**Mheshimiwa Spika,** lengo hili limepangwa kufikiwa kwa kutekeleza majukumu sita likiwemo kuliongezea uwezo wa kimedani Jeshi la ulinzi la Wananchi wa Tanzania kwa kulipatia vifaa na zana bora; mafunzo na mazoezi, kuboresha mazingira ya kufanyia kazi ikiwemo makazi na kuimarisha upatikanaji wa huduma stahiki na mahitaji ya msingi kwa Wanajeshi na Watumishi wa Umma pamoja kuwapa Viijana wa kitanzania mafunzo ya awali ya kijeshi na stadi za kazi ili kuwajengea ukakamavu, uzalendo, umoja wa kitaifa na uwezo wa kujitegemea.

**Mheshimiwa Spika**, uchambuzi wa Kamati umeonesha kuwa, majukumu yaliyopangwa yatawezesha kufikiwa kwa malengo sita (6) ya Wizara hii kwa ufanisi zaidi endapo Serikali itazingatia Mpango na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara kwa kutoa Fedha zitakazoidhinishwa na Bunge kwa ukamilifu na kwa wakati kwa kuzingatia mpango kazi wake.

### *4.2 Uchambuzi wa Makadirio ya Mapato kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024*


**Mheshimiwa Spika,** kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024, Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kwa Mafungu yote matatu (38, 39 na 57) inategemea kukusanya mapato ya jumla ya **Shilingi 87,603,000** Kiasi hiki ni sawa na kiasi kilichopangwa kukusanywa katika Mwaka wa Fedha 2022/2023.
Mchanganuo wa lengo hilo la Makusanyo na Sura ya mchanganuo wake inaonekana katika **Jedwali Na. 04.** na **Chati Na. 03** hapa chini:-

**Jedwali Na. 4: Mchanganuo wa Makadirio ya Maduhuli kwa mwaka 2023/2024**

| Fungu | Makadirio | Asilimia ya lengo la Wizara |
|---|---|---|
| Fungu 38 - Ngome | 22,000,000.00 | 25.11 |
| Fungu 39 - JKT | 64,403,000.00 | 73.52 |
| Fungu 57 - Wizara | 1,200,000.00 | 1.37 |
| **JUMLA** | **87,603,000.00** | **100** |

***Chanzo: Randama ya Wizara 2023/2024***

**Chati Na. 1: Mchanganuo wa asilimia ya Makadirio ya Maduhuli kwa mwaka 2023/2024**




***Chanzo: Randama ya Wizara 2023/2024***

**Mheshimiwa Spika**, kwa uchambuzi huo, Kamati imebaini mambo yafuatayo: -

i) Lengo la makusanyo kwa Mafungu yote ya Wizara hii ni sawa na lengo la Makusanyo kwa Mwaka wa Fedha unaoishia yaani 2022/2023;

ii) Fungu 38 (Ngome) linategemewa katika Makusanyo kwa kiasi cha **asilimia 25.11;**

iii) Fungu 39 (JKT) linategemewa katika Makusanyo kwa kiasi cha **asilimia 73.52;** na

iv) Fungu 57 (Wizara) linategemewa kwa makusanyo kwa kiasi cha **asilimia 1.37.**

**Mheshimiwa Spika**, kwa maelezo hayo, Kamati inaamini kuwa Wizara imeweka lengo linalofikika kwa kuzingatia changamoto zilizojitokeza katika ukusanyaji wa maduhuli kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023.

### *4.3 Uchambuzi wa Makadirio ya Matumizi*

**Mheshimiwa Spika**, maelezo yaliyotolewa na Wizara mbele ya Kamati yalibainisha kuwa katika Mwaka wa Fedha 2023/2024, Bajeti ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa inayoombwa kwa Mafungu yote matatu ni **Shilingi 2,893,846,897,000.** Kati ya fedha hizo

**Shilingi 2,671,013,726,000** sawa na **asilimia 92.3** ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na **Shilingi 222,833,171,000** sawa na **asilimia 7.7** ni kwa ajili ya miradi ya maendeleo.

**Mheshimiwa Spika**, ili kukidhi mantiki ya Masharti ya Kanuni ya 117 (2) ya Kanuni za Bunge, Kamati ilifanya uchambuzi wa makadirio hayo kwa kupitia Kasma *(Items),* Vifungu *(Subvotes)* na Mafungu *(Votes)* yote ikilinganishwa na Bajeti iliyoidhinishwa na kutekelezwa katika Mwaka wa Fedha 2022/2023. Katika uchambuzi wake, Kamati imebaini mambo yafuatayo:-

i) Bajeti ya Wizara hii kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024imeongezeka kwa Shilingi **180,059,491,547** ikilinganishwa na bajeti ya Mwaka wa Fedha 2022/2023. Tofauti hiyo ni ongezeko la **asilimia 6.63.** Kamati inaipongeza Serikali kwa kuzingatia ushauri wa Kamati wa kuongeza kiwango cha Bajeti ya Wizara hii na vyombo vyake vyote inavyovisimamia;

ii) Kiasi cha fedha kinachoombwa kwa ajili ya Miradi yaMaendeleo kimepungua kwa **Shilingi 7,500,000,000** ambayo ni sawa na **asilimia 3.3** ikilinganishwa na kiwango kilichotengwa katika Mwaka wa Fedha 2022/2023. Fedha hizi zimepungua katika Fungu 38 (Ngome) kwa **asilimia 13.3.** ambapo katika 39 (JKT) na Fungu 57 (Wizara) hakuna tofauti;

iii) Kati ya Shilingi **222,833,171,000** zinazoombwa kwa ajili ya kugharamia shughuli za Maendeleo, **asilimia 22** ni kwa ajili ya Fungu 38 - Ngome, **asilimia 6** ni kwa ajili ya Fungu 39- JKT na **asilimia 72** ni kwa ajili ya Fungu 57- Wizara.

**Mheshimiwa Spika**, naomba Bunge lako Tukufu lipokee maelezo hayo yatakayosaidia majadiliano kuhusu hoja iliyowasilishwa na Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara yake kwa Mwaka ujao wa Fedha.

## SURA YA TANO

## 5.0 MAONI NA USHAURI WA KAMATI

**Mheshimiwa Spika,** kutokana na uchambuzi kama nilivyoeleza, Kamati inayo maoni yanayojenga msingi wa ushauri utakaotolewa. Naomba kubainisha maoni hayo kama ifuatavyo:-

### *5.1 Maoni ya Kamati*

i) Utoaji wa fedha za miradi ya maendeleo katika Wizara hii kwa mtiririko uliopangwa ni jambo linapaswa kupewa kipaumbele stahili ili kuendana na malengo yaliyokusudiwa wakati Bunge linaidhinisha fedha kwa ajili hiyo.

ii) Kukosekana kwa "*Bonded werehouse*" ya Jeshi kunasababisha Jeshi kutumia gharama kubwa katika kuhifadhi mizigo Bandarini.

iii) Baadhi ya vifaa na mashine kwa ajili ya matumizi ya Jeshi vimekuwa vikitozwa Kodi mbalimbali kwa mujibu wa Sheria. Hali hiyo husababisha Jeshi kutumia fedha nyingi kulipa kodi wakati vifaa hivyo ni kwa ajili ya matumizi ya Jeshi katika kutekeleza majukumu yake ya ulinzi kwa mujibu wa Katiba na Sheria za nchi.

iv) Uzingatiaji wa ushauri wa Kamati kuhusu Sera ya Ulinzi wa Taifa kwa kipindi tofauti umefikia hatua ya kuhitaji kuwekwa katika utekelezaji. Hivyo, Ukamilishaji wa Sera ya Ulinzi wa Taifa ni jambo linalopaswa kupewa kipaumbele katika Mwaka wa Fedha 2023/2024.

v) Kuimarisha Mipaka yetu ili kudhibiti mianya ya njia zisizo rasmi ni suala linalopaswa kuendelea kupewa kipaumbele. Aidha, katika kudhibiti mianya ya mipaka inayoweza kutumiwa isivyostahili, Serikali iendelee kuboresha uratibu wa jambo hilo.

vi) Maeneo mengi ya Wizara hii hayajapimwa na kupata Hati. Hali hii huchangia kuwavutia wananchi kufanya shughuli zao katika maeneo hayo na badaye kuibuka kwa migogoro kuhusu umiliki.

vii) NYUMBU na MZINGA ni mashirika ya kimkakati. Uboreshaji wa miundombinu na teknolojia kwa Mashirika haya ili uwe na tija ni vema Ikama ya Watumishi ikazingatiwa kwa kuzingatia malengo yaliyowekwa.

### *5.2 Ushauri wa Kamati*

**Mheshimiwa Spika**, kutokana na maoni hayo, Kamati inashauri yafuatayo:-

i) Serikali iendelee kutoa kipaumbele na kuipa uzito unaostahili wa kibajeti miradi ya Wizara ili kupata tija iliyokusudiwa kwa maslahi mapana ya wananchi na na Taifa kwa ujumla.

ii) Serikali ione umuhimu wa kutoa fedha za maendeleo kwa Fungu 38 - Ngome kwa mtiririko uliopangwa. Aidha, Serikali itoe kwa ukamilifu fedha zote za maendeleo ambazo bado hazijatolewa kwa Fungu 57 - Wizara na Fungu 39 (JKT) ili kutoathiri utekelezaji wa shughuli zilizopangwa.

iii) Mamlaka ya Mapato (TRA) pamoja na Mamlaka nyingine zinazohusika ziidhinishe maombi ya Jeshi kutumia *Boundedwere House* zake. Kufanya hivyo kutasaidia Jeshi kupunguza muda wa mizigo yake kukaa kuepuka gharama kubwa inazotumia kuhifadhi mizigo Bandarini *(demurrage charges na storage charges)*.

iv) Serikali ifanye mapitio ya Sheria za Kodi zinazotoza vifaa vya Jeshi ili kuweka utaratibu mzuri wa kutoa msamaha kwa vifaa vyote vinavyoingizwa kwa ajili ya matumizi ya Jeshi kuliko utaratibu uliopo sasa.

v) Katika Mwaka wa Fedha 2023/2024 Serikali ikamilishe upatikanaji wa Sera ya Taifa ya Ulinzi (*The National Defence Policy*) kwa umuhimu wake kwa Taifa kama ambavyo imekuwa ikishauriwa vipindi tofauti tangu Bunge la Tisa.

vi) Serikali iendelee kuchukua hatua madhubuti za kuimarisha miundombinu ya kiulinzi na kudhibiti mianya ya njia zisizo rasmi katika

mipaka yetu. Kufanya hivyo kutawezesha kudhibiti vitendo visivyo na afya kwa Taifa.

vii) Wizara iongeze kasi ya utekelezaji wa mkakati wa kupima na kupata Hati za maeneo yote ambayo hayajapimwa. Kufanya hivyo kutawezesha maeneo ya Wizara kutambulika rasmi na hivyo kuepuka migogoro isiyo na lazima na wananchi.

viii) Uimarishaji wa Mashirika ya MZINGA na NYUMBU uende sambamba na kuongeza rasilimaliwatu kwa kuzingatia mahitaji ya Mashirika hayo. Kufanya hivyo kutaimarisha utendaji kazi wa Mashirika hayo na hivyo kufikia malengo yaliyokusudiwa.

ix) Wizara iendelee kutekeleza Maoni na Mapendekezo ya Kamati yaliyotolewa katika vipindi mbalimbali ambayo hayajatekelezwa hususan katika Bajeti za miaka mitatu iliyopita ya 2020/2021, 2021/2022 na 2022/2023.

## SURA YA SITA

## 6.0 HITIMISHO

**Mheshimiwa Spika**, napenda kukushukuru kwa kunipa nafasi kwa ajili ya kuwasilisha Taarifa hii. Aidha, kipekee nawashukuru Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama ambao maoni, ushauri na ushirikiano wao umewezesha kukamilika kwa taarifa hii. Naomba majina yao kama yalivyo katika Taarifa hii yaingie katika Taarifa Rasmi za Bunge (Hansard): -

1. Mhe. Vita Rashid Kawawa, Mb - Mwenyekiti
2. Mhe. Vincent Paul Mbogo, Mb - M/Mwenyekiti
3. Mhe. Abdi Hija Mkasha, Mb - Mjumbe
4. Mhe. Ali Juma Mohamed, Mb - Mjumbe
5. Mhe. Bupe Nelson Mwakang'ata, Mb - Mjumbe
6. Mhe. Cosato David Chumi, Mb - Mjumbe
7. Mhe. Daniel Tlemai Awack, Mb - Mjumbe
8. Mhe. Dr. Alfred James Kimea, Mb - Mjumbe
9. Mhe. Edwin Enosy Swalle, Mb - Mjumbe

10. Mhe. Fakharia Shomar Khamis, Mb - Mjumbe
11. Mhe. Felister Deogratius Njau, Mb - Mjumbe
12. Mhe. Grace Victor Tendega, Mb - Mjumbe
13. Mhe. Jafari Wambura Chege, Mb - Mjumbe
14. Mhe. Joseph Anania Tadayo, Mb - Mjumbe
15. Mhe. Joseph Michael Mkundi, Mb - Mjumbe
16. Mhe. Maulid Saleh Ali, Mb - Mjumbe
17. Mhe. Minza Simon Mjika, Mb - Mjumbe
18. Mhe. Muharami Shabani Mkenge, Mb - Mjumbe
19. Mhe. Mwinyikondo Rajab Mustafa, Mb - Mjumbe
20. Mhe. Neema Lugangira, Mb - Mjumbe
21. Mhe. Nicholaus G. Ngassa, Mb - Mjumbe
22. Mhe. Zahor Mohammed Haji, Mb - Mjumbe

**Mheshimiwa Spika,** kwa niaba ya Wajumbe wa Kamati napenda kutumia fursa hii kumshukuru Waziri wa Ulinzi na JKT Mhe. Innocent L. Bashungwa (Mb) kwa ushirikiano wake mzuri katika kipindi chote cha utekelezaji wa majukumu ya Kikanuni ya Kamati. Aidha, namshukuru Katibu Mkuu Dkt. Faraji Mnyepe pamoja na Watendaji wote wa Wizara kwa ushirikiano wao.

**Mheshimiwa Spika,** Vilevile napenda kumshukuru Katibu wa Bunge Ndg. Nenelwa J. Mwihambi, *ndc* kwa kuratibu vyema shughuli za Kamati na Bunge. Aidha, nawashukuru Kaimu Mkurugenzi wa Idara ya Kamati za Bunge Ndg. Michael Chikokoto, *ndc*. Mkurugenzi Msaidizi Ndg. Gerald Magili na Makatibu wa Kamati hii Ndugu Omary Magwinza na Bi. Victoria Mizengo wakisaidiwa na Bi. Rehema Kimbe kwa kuratibu vyema shughuli za Kamati na kuhakikisha Taarifa hii inakamilika kwa wakati.

**Mheshimiwa Spika,** baada ya maelezo hayo, sasa naliomba Bunge lako Tukufu liipokee Taarifa hii na likubali kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024 kama yalivyowasilishwa na Mtoa Hoja.

**Mheshimiwa Spika**, naunga mkono hoja na naomba kuwasilisha.

**Vita Rashid Kawawa, Mb**
**MWENYEKITI ULINZI NA USALAMA**
**KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA MAMBO YA NJE,**
24 Mei, 2023

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Zahor Mohammed Haji kwa niaba ya Mwenyekiti. Waheshimiwa Wabunge, hayo ndiyo mambo ambayo Kamati imepata nafasi ya kuyatazama na sasa imewasilisha kwetu ili tuyatumie hayo kuishauri Serikali.

Waheshimiwa Wabunge, mnaozungumza na simu, nilishatoa maelezo kuhusu matumizi ya simu humu ndani. Ukitaka kuongea na simu, toka nje ili uwape nafasi Wabunge kusikiliza yanayosemwa humu ndani. Milango iko sehemu nyingi. Kama kuna sababu, tutafanya semina ya kuwaeleza mahali pa kutokea ili usione ni mbali. Hakuna kiti ambacho kiko mbali na mlango. Bunge letu limekaa vizuri kabisa kukupa nafasi Mheshimiwa Mbunge kuzungumza na wapiga kura, kuzungumza na viongozi wakiwa wana jambo la haraka la kukwambia, lakini usizungumze na simu Bungeni. Usizungumze na simu Bungeni. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunaanza uchangiaji. Tunaanza na Mheshimiwa; sasa huyu sijui kama hata ameshafika kwenye kiti chake. Tunaanza na Mheshimiwa Zahor Mohammed Haji, atafuatiwa na Mheshimiwa Fakharia Shomar Khamis, Mheshimiwa Rashid Abdalla Rashid ajiandae. Ama ungehitaji dakika chache za kupumzika Mheshimiwa?

**MHE. ZAHOR MOHAMMED HAJI:** *Yes Madam*.

**SPIKA:** Haya, ahsante sana. Basi yeye nitamwita baadaye ili apumue kidogo. Mheshimiwa Fakharia Shomar Khamis atafuatiwa na Mheshimiwa Rashid Abdalla Rashid na Mheshimiwa Ahmed Ally Salum ajiandae.

**MHE. FAKHARIA SHOMAR KHAMIS:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Kwanza sina budi kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijaalia afya na uzima kusimama mbele ya Bunge lako tukufu. Vilevile nampongeza Mheshimiwa Waziri kwa usomaji wake mzuri pamoja na Mheshimiwa Zahor pamoja na watendaji wote wa Wizara ya Ulinzi na viongozi waliokuja wastaafu wa ulinzi na viongozi wanaoendelea na majukumu yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sina budi kwanza kuishukuru Wizara na SUMA - JKT kwa ujenzi wa Ikulu yetu nzuri, ya kileo ya kufahari, kwa pesa za kodi za Watanzania. Jengo linapendeza na wamelijenga kizalendo, lazima tuwapongeze. Mtu akifanya kitu kizuri ana haki ya kupongezwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nitazungumzia ujenzi wa hanga la kuegesha ndege za jeshi. Kwa kweli walipewa Shilingi bilioni 11 na walitakiwa wajenge Dar es Salaam, Dodoma, pamoja na Chato Mkoa wa Geita. Wamejitahidi na kampuni iliyopewa *M/S Simba Limited* imefanya kazi nzuri. Tumekwenda kulitembelea la Dodoma liko katika hali nzuri na hata Kamati imeeleza hapo mbele kwamba wamejitahidi na lazima na wao pia kampuni ipongezwe na Wizara tuipongeze kwa kusimamia. Ingawa walianza mwaka 2021 wakatakiwa kumaliza mwanzoni mwa 2023, lakini hawajachelewa, kazi imekamilika, hongereni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nakuja kwenye suala la ukusanyaji wa maduhuli. Ukusanyaji wa maduhuli kwa kweli kidogo wameshuka, lakini siyo sana na ilikuwa Ngome - Fungu 38, JKT - Fungu 39 pamoja na Wizara - Fungu 57 kwa pamoja zipatikane Shilingi bilioni 87.6, lakini kwa kweli hawakufikia lengo. Wamefikia Shilingi bilioni 85.1. Siyo mbaya, lakini hawakufika lengo.

Mheshimiwa Spika, kimsingi labda tuangalie pesa walizokuwa wakilipwa na Wizara ya Fedha zilikuwa chache tuseme ikawa ndiyo sababu, kwa sababu na Wizara ya Fedha safari hii imewabinya. Maombi ya fedha walizokuwa wakiwapa siyo waliyoomba. Wanasahau kama hiki ni chombo cha ulinzi, kinahitaji pesa. Usalama

wetu na ulinzi wa mipaka yetu iko chini ya dhamana yao, na mtu hawezi kufanya kazi kama hana pesa. Sasa Waziri wa Fedha hili awe analiangalia. Makisio ya ulinzi yawe hayapungui, yanapelekwa kama wanavyoomba na matokeo yake tunayaona kwa sababu wanajeshi wetu ni wazalendo, wanafanya kazi zinavyopangwa kwa mujibu wa taarifa wanazozileta. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusu sera ya ulinzi wa Taifa *(defense policy)*. Hii sera bado haijafanya kazi kwa sababu hatuoni hizo *missions* na *visions* zao walizozipanga na wanashindwa kutokana na kwamba hii sera haijatolewa tukajua. Unajua tu kwamba wameambiwa wafanye siku nyingi toka Bunge la Tisa. Wanasema hivi, Serikali ya Zanzibar bado haijatoa maoni yake, wadau; lakini Serikali ya Mapinduzi Zanzibar tayari ilishatoa maoni na wadau tayari walishatoa maoni. Sasa kinachochelewesha nini hii sera haifanyi kazi? Bila ya sera huwezi kufanya kazi. Sera ndiyo itakayokupa mwongozo ukaweza kufanya kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri atuambie amekwama wapi? Kuna tatizo gani? Hii sera hadi hii leo mambo yote umeshapata, majukumu itakuwa yote umeshapata, kwa nini mpaka hii leo haijafanya kazi? Tunaomba Mheshimiwa Waziri utakapokuja utuambie umekwama wapi? Kama utataka upate msaada kwenye Kamati au kwenye Serikali tutajua vipi tunakuisaidia Kamati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nazungumzia kwamba Wizara iongeze kasi ya utekelezaji wa mkakati na kupata hatimiliki za maeneo. Unajua maeneo ya jeshi kwa sasa na tunakoelekea siyo makubwa ya hivyo, yanahitaji kuongezwa, na nafasi hamna kwa sababu mshabanwa na wananchi wamejenga mpaka karibu na kambi. Mliambiwa mkae na Wizara ya ardhi ili mweze kuelewana, vipi mtaondoa, vipi mtapima, kwa sababu kuna kambi nyingine mpaka hii leo hazina hatimiliki.

Mheshimiwa Spika, ingawa leo wamezungumza hapa kwamba Kambi ya Chukwani tumeshalipwa, lakini ziko nyingi tu. Kuna Mtoni, kuna Ubago, zipo nyingi tu ambapo bado nina hakika

hazina hatimiliki. Hiyo ni kwa upande wa Zanzibar. Sikwambii kwa upande wa Pemba, sikwambii kwa upande wa Mikoani. Naomba hili Mheshimiwa Waziri mliangalie mweze kujua kwamba ni vipi mtaweza kuvuka ili tusigombane na wananchi, tusigombane na Taifa na mweze kuwa na makambi yenu ambayo mnayamiliki na yawe hayana matatizo.

Mheshimiwa Spika, kwa haya machache, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Waheshimiwa Wabunge, kabla hatujaendelea, nimeletewa ujumbe hapa. Kuna wageni wa Mheshimiwa Noah Lemburis Saputu Mollel, hawa ni Makatibu Waenezi wa CCM kutoka Arumeru Magharibi. Karibuni sana Bungeni. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, nilikuwa nimeshamtaja Mheshimiwa Rashid Abdalla Rashid, atafutiwa na Mheshimiwa Ahmed Ally Salum, na Mheshimiwa Prof. Patrick Alois Ndakidemi ajiandae.

**MHE. RASHID ABDALLA RASHID:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipatia nafasi hii ya kuchangia Wizara yetu hii ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa. Kwanza, nampongeza Mheshimiwa Waziri kwa hotuba yake nzuri fupi ambayo imejaa mambo yote ambayo yanahusu masuala ya kijeshi. Kipekee nawapongeza watendaji wake ambao wameandaa hotuba hii kwa kweli wamefanya kazi nzuri na wameisoma na tumeifahamu vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nianze kwa upande wa Jeshi la Wananchi wa Tanzania, kwa kuwashukuru sana kwa kuwapatia eneo wananchi wa Kimbini Kengeja, eneo ambalo linamilikiwa na Jeshi lakini kuwaruhusu wananchi kufanya shughuli zao pale kwa masharti ambayo wananchi wanayatimiza ya kutojenga, kutouza ili wafanye shughuli za kilimo na za kijamii tu, na wananchi kweli hakuna mgogoro na jeshi wanafanya shughuli zao kama kawaida, na yale masharti na matakwa ambayo wamepewa na jeshi wanayafuata.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nikwambie kwamba wananchi wa Kengeja Mwambe wanashukuru sana jeshi la wananchi kwa kuwapatia eneo hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Zanzibar tuna *school* mbili ambazo zinamilikiwa na jeshi. Kuna *School* ya Nyuki iliyopo kisiwa cha Unguja na na *School* ya *Ally Khamis Camp* iliyopo Vitongoji Chakechake Pemba. *School* hii ya *Ally Khamis Camp* ni miongoni mwa *school* zinazofanya vizuri sana kwa upande wa Pemba na hata kwa Zanzibar. Inafanya vizuri kwa upande wa msingi, na pia inafanya vizuri kwa upande wa sekondari. Nilikuwa naomba tu hata Mheshimiwa Waziri, najua hana muda mrefu katika Wizara hii, lakini afanye jitihada za makusudi za kufika Kisiwani Pemba na kwenda kuikagua *school* hii aone jinsi watoto wanavyofanya vizuri katika masomo yao na ukakamavu ambao wanao, na matokeo bora ambayo wanayapata katika kila mwaka kwenye mitihani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia Mheshimiwa Waziri atambue kwamba, skuli hii ina changamoto ya mabweni ya wanafunzi wa kike na wa kiume, ili wanafunzi wafanye vizuri lazima wapate mahali pazuri pa kusomea. Ningeomba Mheshimiwa Waziri atenge fedha kwa ajili ya ujenzi wa mabweni katika skuli ile ili watoto waendelee kufanya vizuri na kulijengea heshima Jeshi la Wananchi, lakini pia na Taifa kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, katika Kambi ya Jeshi la Wananchi katika eneo la Uwanja wa Ndege, makazi yao kwa kweli siyo mazuri. Wanajeshi wale wanafanya kazi kwa uzalendo mkubwa sana kama lilivyo Jeshi lenyewe, na yale maadili yao ambayo wanayo, lakini kwa kweli yale majengo yaliyoko katika eneo lile la uwanja wa ndege hayaridhishi kabisa. Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri nikuombe kwamba, katika bajeti yako siyo kambi kubwa sana lakini ni ulinzi mkuba kwa uwanja wetu wa ndege hasa kwamba, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar sasa hivi miongoni mwa miradi yake mikubwa ni kuutanua uwanja wetu wa ndege wa Pemba ili ndege kubwa ziweze kutua. Sasa kwa *style* ile ya nyumba zile au ofisi zile au kambi ile ya jeshi kwa kweli, haileti picha nzuri.

Mheshimiwa Spika, naomba Mheshimiwa Waziri utakapofanya safari yako upite huko uone. Najua kwamba, Jeshi lina maadili, hawawezi kila taarifa wakazitoa, lakini hili kwa sababu wanatulinda nasi tulioko humu tunawatetea, ni vema ile kambi nayo ikafanyiwa ukarabati mzuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo alilieleza katika ukurasa wa 14 la kuendelea kutoa huduma za afya kwa Maafisa, wapiganaji na wananchi kwenye maeneo mbalimbali ya nchi yetu. Ninakiri kwamba, katika kisiwa chetu cha Pemba kuna hospitali kubwa ya Jeshi ambayo inatuhudumia wananchi wengi, lakini hospitali hii ina upungufu wa vifaatiba. Ameeleza hapa kwamba, wanao mpango wa kununua vifaatiba, kaviorodhesha, ukiangalia katika ukurasa wa 14 utavikuta. Nimuombe Mheshimiwa Waziri na ile Hospitali ya Jeshi ya Vitongoji tunaomba na wao wapelekewe vifaa hivi ili huduma zile za tiba tuweze kuzipata vizuri pale Jeshini na kwa nidhamu nzuri ambayo tunaipata kutoka Jeshini.

Mheshimiwa Spika, kuna jambo jingine ambalo Jeshi la Wananchi Tanzania kwa upande wa Zanzibar limefanya ni jambo kubwa sana na ni jambo la kushukuru sana. Jeshi hili wamefanya uwekezaji mkubwa katika eneo la Migombani, miongoni mwa uwekezaji ambao wameufanya ni ujenzi wa kituo cha mafuta pale maeneo ya Migombani, kituo ambacho kinatoa huduma masaa 24 pamoja na huduma za kifedha ambapo wananchi wa Zanzibar wanaamini kwamba, *time* yoyote ambayo unahitaji kupata huduma pale Jeshini unazipata. Kwa hiyo, tuwashukuru na tunawapongeza sana kwa kazi hii kubwa ambayo wameifanya, ni uwekezaji mkubwa na wanaendelea kujenga maduka mengi na makubwa ya kisasa kabisa.

Mheshimiwa Spika, kwa sababu, kengele tayari ya kwanza imeniashiria huko na umeshanionesha, hata niombe dakika moja nizungumzie kidogo tu kwa upande wa JKT. Kwa upande wa JKT nao wanafanya vizuri na wanachukua vijana wetu hawa wa kujitolea, wanawajengea uzalendo na ujasiriamali. Ninaomba sana

kwamba, katika kuwajengea ujasiriamali huu basi lazima kule JKT wajipange kwa vifaa ili watoto wetu wanapotoka kule, mbali ya kutegemea ajira hizi kupitia vyombo vya ulinzi na usalama na wao wakitoka waweze kujiajiri na wasikae tu mitaani na kusubiri kazi hizi za ulinzi. Vinginevyo hawa watu wamefundishwa uzalendo, wanaweza kutumia silaha vizuri, ndiyo sasa mara tunakuja kukuta hawa watu wanatumia silaha mitaani vibaya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Ahmed Ally Salum, atafuatiwa na Mheshimiwa Profesa Patrick Aloyce Ndakidemi, Mheshimiwa Zahor Mohamed Haji ajiandae.

**MHE. AHMED A. SALUM:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi. Kwanza kabisa naunga mkono hoja yetu hii ya Wizara ya Ulinzi. Imesomwa na Mheshimiwa Waziri, yuko vizuri, yuko sahihi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kabla sijaendelea Amiri Jeshi Mkuu, Mama yetu Mama Samia, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kama Amiri Jeshi Mkuu wa Jeshi letu la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania nimshukuru sana kwa kazi anayoifanya. Amani ya nchi ina mambo mengi katika kuhakikisha amani inakuwepo katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Moja katika kazi kubwa kabisa inayofanyika ni pamoja na Mama kutengeneza au kujenga au kuwa na mahusiano mazuri kabisa na nchi zote za Afrika ikiwemo nchi zilizotuzunguka. Hiyo yote ni sehemu moja katika kuona kwamba, Watanzania wanaishi kwa amani kufungua fursa za nchi, wakishirikiana na Jeshi letu la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pili ni pia, nimshukuru Mkuu wetu wa Majeshi, *CDF General* Nkunda kwa kazi kubwa anayoifanya pamoja na timu yake nzima, Luteni *General* Salim Othman, ma-Meja *Generals* wote, ma-*Brigadier Generals* wote, ma-Kanali wote, ma-

Meja wote kwa kazi kubwa wanayoifanya kwa ajili ya amani ya Jamhuri yetu ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, amani ina mambo mengi na moja katika eneo ambalo wanatusababishia, ukiacha Mungu mwenyewe, amani ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ni Mungu mwenyewe ametupa zawadi kwamba, Tanzania ni moja katika nchi chache Afrika au duniani ambazo mpaka sasa hivi zina amani na tunaishi kwa raha. Kama ni wafanyabiashara, kama ni wafanyakazi, na namna yoyote ile tuko kwenye amani kubwa sana. Moja katika sababu kubwa kabisa ni Jeshi ambalo wanafanya kazi kubwa ya kuhakikisha amani inakuwepo katika Jamhuri yetu ya Muungano wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, taharuki niliwahi kusikia huko Kusini, kuna wakati ilitokea taharuki hapa na pale, kazi kubwa ilifanywa na Jeshi letu la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kuna vijana kule wanakaa *24/7* wanakaa kwenye mapori mazito yale kuhakikisha wako tayari kujitoa muhanga, wako tayari kupoteza maisha yao kwa ajili ya amani ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Hapa tunapokaa tunaona Bunge hili, Bunge hili linakaa kwa sababu ya amani ya Jeshi hili la Jamhuri ya Muungano wakiongozwa na *General* Nkunda katika kuhakikisha kwamba, hata Kusini kule taharuki iliyokuwepo Kusini kule amani inakuwepo. Hata wananchi wa Mtwara amani ipo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa hivi kuna vijana wetu wako hata Msumbiji wanakwenda kutoa ushirikiano mkubwa sana kwenye Jeshi la Msumbiji ili kushirikiana na Jeshi ambalo liko hapa Tanzania kuhakikisha eneo lile ambalo liko Kusini kule linaendelea kuwa na amani. Amani katika nchi yetu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika kambi zile ambazo ziko Kusini, zote ni Watanzania vijana wako zaidi ya 1,500 ndani ya Msumbiji wakitoa ushirikiano, wakitoa mafunzo na Watanzania wanajeshi wanashirikiana pale kuona kwamba amani inakuwepo.

Mheshimiwa Spika, ninamuomba tu Mheshimiwa Waziri, *operation* kama hii ni gharama kubwa sana, Jeshi hili linafanya kazi kwa weledi, kwa uzoefu, kwa uzalendo, nikuombe tu kwamba kama kuna namna ambayo kuna mapungufu ya kulihudumia Jeshi hili kwenye aina hii ya *operation* peke yake huku Kusini, hebu jaribu kuona kwa sababu bado mwezi mmoja, hotuba yako na hotuba ya Kamati imeelezea kwamba, bado kuna fedha wanahitaji ili kukamilisha mambo yao waliyojipangia katika maendeleo yao. Bado sasa hivi ni kama mwezi mmoja mpaka kufikia Tarehe 30 mwezi wa Sita, kuna tatizo gani, kama ni Waziri wa Fedha yuko hapa, mkahakikishe kwa muda huu fedha ambazo zimebaki wakapewa, lakini *specifically* Mheshimiwa Waziri utakapokuja kuhitimisha hoja yako hapa itapendeza sana, sina mashaka na wewe kabisa Mheshimiwa Waziri wa Ulinzi, lakini kama watakuwa na mipango ya muda mfupi, muda wa kati na muda mrefu, kuboresha Jeshi la Tanzania kutoka tulikotoka tulipo hapa sasa hivi tukawa katika Jeshi bora Afrika na Tanzania. Kwa maana ya kwamba, kubadilisha mitambo, kubadilisha zana, kuwa na mawasiliano, Jeshi likawa la kisasa zaidi.

Mheshimiwa Spika, *specifically* kwenye *operation* hii nimuombe Mheshimiwa Waziri kama kuna uwezekano waongezewe fedha angalao hata kama bilioni 150, *specifically* naongelea kwa ajili ya *operation* hii ya Kusini mwa Tanzania. Sasa utakapokuja kuhitimisha hapa Mheshimiwa Waziri, kama utakuwa na namna ambayo utaiweza sisi Wabunge tuko hapa na tuko tayari kukuunga mkono. Kama utakuwa na mipango mizuri tutakuunga mkono wala hatuna shida na wala sina mashaka kabisa na wewe pamoja na Serikali ya Mheshimiwa Mama Samia Suluhu Hassan. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri ameongea hapa kwa maana sasa wamekubaliana kwamba tutaingia *partnership* na *private sector* katika kuliendeleza Jeshi. Niliwahi kuongea na niliwahi kushiriki Bunge hili wakati ule, mwaka juzi kwenye bajeti na nikasema Jeshi letu la Tanzania wana uwezo mkubwa mno wa kutengeneza silaha ndogondogo, wana uwezo mkubwa mno wa kutengeneza hata risasi, wana uwezo mkubwa mno wa kutengeneza hata

magari, lakini pale ambapo kutakuwa na mpango mzuri wa kushirikiana na sekta binafsi, iwe nje ya nchi iwe ndani ya nchi, uwezo huo upo. Hawa wenzetu wamewezaje?

Mheshimiwa Spika, kuna nchi hapa jirani wanajipambanua hivi, lakini sisi ndiyo tuliowafundisha, tuliowaweka pale na tuliwasababisha wakakaa vizuri. Leo wanakuwa na mipango mizuri kuliko hapa, haiwezekani! *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nimuombe Mheshimiwa Waziri awe na mipango hiyo. Na uwezo mkubwa kabisa, Jeshi la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania wapo wasomi wazuri, Jeshi la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania wana uwezo mkubwa sana, wamo ma-*engineer* wazuri sana, ni suala tu la kukaa, kuwa na mipango, tunafanyaje, unahitaji fedha, kama kuna *private sector* inakuja, lete Bungeni tupitishe waende wakatengeneze hayo mambo ambayo watakuwa wamejipangia. Tukianza kutengeneza silaha, tukawa na risasi, tukawa na mambo yote hayo, hata magari, hata zana, hatuwezi kushindwa, lakini tukawa na mpango wa muda mrefu tunakuwa tunajihakikishia kabisa kwamba, tunaweza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nchi kama *Egypt* leo wanatengeneza silaha nyingi tu, wanatengeneza risasi nyingi tu, tunashindwaje sisi? Tanzania ina historia kubwa ya kuleta uhuru Kusini mwa Afrika, tunashindwaje sisi? Leo hapa nchi jirani hapa tuna mawasiliani mazuri. Jeshi la Tanzania lina historia nzuri sana Afrika, Jeshi la Tanzania lina historia nzuri sana kuleta uhuru nchi zote za Kusini mwa Afrika, tunashindwaje kufanya hivyo, ni suala la mipango tu.

Mheshimiwa Spika, mimi sina mashaka na uongozi wa Jeshi wako vizuri sana, tukiamua kwa pamoja, mkiamua kama Wizara kwa pamoja tutoke kwenye Jeshi lililopo sasa hivi *standard* hii tuihuishe ipande kabisa liwe Jeshi la kisasa, wawe na mitambo ya kisasa, wawe na mawasiliano ya kisasa, yaani liwe Jeshi la kidijitali kutoka kwenye Jeshi la analogia ambalo tunalo sasa hivi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ushauri wangu, ukishakuwa na mipango ya kati, mipango ya muda mrefu, Jeshi hili litakuwa Jeshi moja zuri sana. Bahati nzuri sana heshima ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa nchi za Afrika ni kubwa mno. Suala la kuwa na amani mimi sina matatizo kwa sababu amani ipo, lakini unapokuwa na jeshi zuri ni *back up* ya kuwa na amani ndani ya nchi na hata nchi jirani wanajua kabisa Tanzania pale Jeshi ni zuri hakuna sababu ya kuleta fyokofyoko, tukileta fyokofyoko tunafyatuliwa. Kwa hiyo, suala la kuwa na Jeshi imara ni moja ya *back up* kubwa sana kusababisha amani ndani ya nchi, Ukiachana na Mama Samia anavyohangaika kutengeneza diplomasia nchi za Afrika na duniani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuboresha maslahi ya wanajeshi na hasa hawa ambao wanaingia kwenye *operations* za moja kwa moja, kuwepo na mipango mahsusi kabisa hawa ambao wanakwenda kuhatarisha maisha yao kwa ajili ya nchi yetu, hawa ambao wanakaa kule kwa ajili ya nchi yetu, hawa hebu tuone maslahi yao yamekaaje kwa maana ya maslahi yao, kwa maana ya zana za kisasa…

**SPIKA:** Kengele ya pili imeshagonga Mheshimiwa.

**MHE. AHMED A. SALUM:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. Naunga hoja mkono, ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Profesa Patrick Aloyce Ndakidemi, atafuatiwa na Mheshimiwa Zahor Mohammed Haji, Mheshimiwa Vedastus Manyinyi Mathayo ajiandae.

**MHE. PROF. PATRICK A. NDAKIDEMI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa fursa na nianze kwa kuunga mkono hoja.

Mheshimiwa Spika, nianze kwa kumpongeza sana Waziri wetu wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, Mheshimiwa Innocent Bashungwa, Katibu Mkuu Dkt. Faraji Mnyepe, Mkuu wa Majeshi Generali Jacob John Mkunda na Mnadhimu Mkuu wa Jeshi Luteni

Jenerali Salim Haji Othman pamoja na Mkuu wa JKT Meja Jenerali Rajab Mabele na Makamanda wote nchi hii kwa kazi nzuri mnayofanya, hongereni sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia nimpongeze Rais wetu Dkt. Samia Suluhu Hassan, ambaye ni Amiri Jeshi Mkuu kwa jinsi alivyoipa kipaumbele sekta ya ulinzi kwenye Taifa letu. Tunamshukuru sana Rais wetu kwa hilo kwa sababu, tunaona hata bajeti ya Wizara ya Ulinzi imeongezeka kwa 6.9 *percent.* Hiyo inaonesha dhamiri njema ya Rais wetu kwenye kuboresha ulinzi katika nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Jeshi letu la Wananchi ni Jeshi imara sana na ni Jeshi bora, linaongozwa kwa misingi ya uzalendo, utii na nidhamu ya hali ya juu. Amani tunayoringia hapa nchini kama Watanzania inatokana na uimara wa Jeshi letu. Jeshi letu liko imara na sisi Watanzania tunafurahia sana uwepo wao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kama Taifa nchi yetu imeshafanya mambo mengi sana ambayo nitataja kwa haraka haraka mambo machache. Kwanza kabisa ilishiriki kwenye vita vya kukomboa Mataifa ya Kusini mwa Afrika. Pili, ikafundisha Majeshi ya Vyama vya Ukombozi katika nchi hizi ambazo tulizikomboa. Tatu, kikubwa kuliko vyote, tulimtandika nduli Iddi Amini na kumsambaratisha moja kwa moja, ile vita ilikuwa nzuri na ni nchi ambayo iliweza kuliondoa Jeshi la nchi nyingine madarakani moja kwa moja na kulisambaratisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vilevile Jeshi letu limeshiriki katika *operations* mbalimbali hapa duniani kwenye kulinda amani, kikubwa pia, limeshiriki katika shughuli mbalimbali za kuokoa watu, kwa mfano, Mheshimiwa Waziri amesema juzi walikuwa huko Malawi, hapa nchini wala hatusemi. Kule kwangu Kilimanjaro walikuja wakazima ule moto kule mlimani, sisi tunawshukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa ujumla Jeshi letu ni la Wananchi kwelikweli na siyo mchezo. Ukiangalia kona zote nilizotaja wanafanya mambo ambayo yanaonekana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa katika mchango wangu leo nitajikita kwenye vijana wanaojiunga na JKT, wale wa kujitolea, kwa miaka miwili na wanapoondoka ni nini kinatokea, nitashauri ni nini kifanyike kama makamanda mtanisikiliza.

Mheshimiwa Spika, Jeshi letu la Kujenga Taifa lina lengo la kulea vijana wetu na wanawafundisha vitu vingi sana, ikiwepo umoja, uzalendo, mbinu za kuzalisha mali na mafunzo ya ulinzi, hawa vijana wamepatiwa hivyo vitu, vijana hawa huchaguliwa kwa kuangalia walivyofaulu, kwa mfano, kama wewe ni darasa la saba una cheti, unachaguliwa, wanaenda mpaka *form six* na ukishinda masuala ya ukakamavu unaingia Jeshini.

Mheshimiwa Spika, wanapoingia kambini vina wetu huwa wanafundishwa na makamanda ambao wamesoma, Jeshi letu lina wasomi wazuri sana kwenye sekta mbalimbali, wanafundishwa na watu wenye *degree* na *diploma.* Mafunzo wanayopata kule Jeshini yanakwenda kwenye ulinzi wa Taifa, uzalendo, kilimo, ufugaji, ujenzi, useremala, ufugaji nyuki, ufugaji mifugo na ujasiriamali kwa ujumla hata biashara wanafundishwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa katika stadi nilizotaja hapo juu huwa zinatolewa kwa nadharia na vitendo kwa hiyo, hawa vijana wanafundishwa darasani na kwa vitendo na wakitoka pale wanakuwa wameiva vizuri kabisa, lakini baada ya mafunzo ya miaka miwili vijana wetu hawa hurudi uraiani, niwe mkweli, wengi wao huwa hawafanikiwi kuendelea, kwa mfano walivyokuwa kwenye kilimo hawaajiriwi kwenye sekta za kilimo, hawaendi kwenye sekta za mifugo na kwenye ajira za Serikali. Tunalishukuru sana Jeshi la Polisi, Magereza, Zimamoto, Uhamiaji na Jeshi la Wananchi Tanzania, huwachukua hawa vijana walio na cheti cha Jeshi na kuwapa kazi. Huwapa kipaumbele cha kuwaajiri, lakini wale

waliosoma kilimo na vitu vingine haiwasaidii, haionekani inawasaidia mahali popote pale. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninafikiria sasa ni wakati ambapo jeshi letu lichukue ushauri wa kushirikiana na mamlaka zinazotoa vyeti vingine. Kwa mfano, nimeona Waziri amesema wana ushirikiano mzuri sana na Wizara ya Kilimo na Mifugo. Washirikianenao sasa watangeneze mitaala inayofaa iwe kwenye *National Qualification Framework* ili hawa vijana wanapotoka pale wanapofundishwa na Wanajeshi wetu ambao wamesoma, amefundishwa uzalendo yuko vizuri, apate diploma au cheti. Ni kitu kirahisi sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kule Jeshini kuna kitu ambacho kimeshatokea kwenye Kambi yetu ya Monduli, pale Arusha. Wanashirikiana vizuri sana na chuo cha, taasisi ya *Accounts* ya Arusha *(Institute of Accounts Arusha)* na wanatoa *degree* ya Shahada ya Kwanza ya Sayansi za Kijeshi, hapo wamefanikiwa. Sasa ninashauri JKT ibadilike tuwatafute hawa watu kama ni *VETA,* mtu wa darasa la saba apate cheti, kama ni mtu wa *NACTE* apate diploma, na kadhaika hata ikiwezekana *degree* wapate. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wanapotoka hawa vijana wetu wakimaliza haya mafunzo ambayo nimeyataja kwenye hizi sekta ambazo wanawafundisha kule, wakiwa na cheti cha *diploma* au *certificate* au *degree* kutoka Jeshini, nakuhakikishia tutawapigania kama mpira wa kona kuwapa kazi. Kwa sababu watakuwa wamefundishwa ukakamavu, uzalendo na hakuna mtu atakayemkimbia mtu ambaye amepata mafunzo kupitia kwa hawa makamanda wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo nihitimishe kwa kusema kwamba naomba hili jambo lipewe kipaumbele ili hii *effort* ambayo vijana wanatumia miaka miwili isiishie pale ambapo wamepata vile vyeti tu vya Jeshi, wapewe na hizi *qualifications* nyingine ili waweze kusaidia Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Zahor Mohammed Haji, atafuatiwa na Mheshimiwa Vedastus Manyinyi Mathayo, Mheshimiwa Ussi Salum Pondeza ajiandae.

**MHE. ZAHOR MOHAMMED HAJI:** Mheshimiwa Spika, naomba nikushukuru kwa kunipa nafasi.

Mheshimiwa Spika, kwa kuanza naomba nimshukuru Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Amiri Jeshi Mkuu wa Majeshi ya Ulinzi, kubwa kwa kuendelea kuiunga mkono Wizara hii pamoja na vyombo vyetu vyote kwa sababu yeye ndiye kiongozi wa majeshi haya na ndio mkuu wa ulinzi wa Taifa hili.

Mheshimiwa Spika, lakini pia naomba kumshukuru Mheshimiwa Waziri pamoja na timu yake yote kwa sababu mara zote wamekuwa wakishirikiana vizuri na Kamati yetu ili kuhakikisha kwamba Kamati zinafanya majukumu yake kwa mujibu wa Kanuni zetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa mimi naomba kuchangia mambo machache sana, nikiamini kwamba Serikali itaweza kutusikia, kutusikiliza na kutekeleza. Kwanza naomba niwashukuru kwa sababu Serikali imeamua kuongeza asilimia kama moja nukta kitu hivi kwa ajili ya shughuli za Wizara yetu hii. Lakini ninaomba kuomba zaidi, tena kwa heshima kubwa sana.

Mheshimiwa Spika, huko nyuma niliwahi kusema kwamba Jeshi ni chombo cha utafiti, Jeshi ni chombo cha ulinzi. Chombo hiki kinatulinda angani, kinatulinda ardhini, kinatulinda baharini na mipakani. Sasa pamoja na kwamba Serikali yetu inafanya jitihada kubwa za kuwaongezea uwezo, bado naiomba Serikali iendelee kutafakari kwa kina sana, kwa sababu kazi kubwa ya Jeshi letu ni kulinda mipaka yetu, *period. (Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo ninaomba sana, pamoja na kwamba Serikali imefanya kazi ya kuongeza lakini bado kwa sababu

Jeshi hili halina pa kulia, Jeshi hili sehemu ambayo itaomba ipatiwe nyenzo za kufanyia kazi ikiwemo utafiti ni Bunge lako hili. Kwa hiyo ninaomba sana, kwa niaba ya Kamati yangu, lakini kwa niaba ya Bunge hili, tuombe sana Serikali itusikie na ituelewe kwamba tunahitaji Jeshi la kisasa, ambalo tutaliwezesha ili kazi yake iwe moja tu, ya kulinda mipaka yetu ili kuhakikisha kwamba Tanzania inaendelea kubaki kuwa salama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, la pili, wakati tunasoma taarifa yetu pale, tulizungumzia hoja ya kuliwezesha Bunge. Moja miongoni mwa kuliwezesha Bunge Jeshi letu hili ni kuhakikisha kwamba linapata vitendea kazi lakini vilevile na sisi tunaendelea kusaidia kuhakikisha kwamba halitumii fedha nyingi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Jeshi letu linapata gharama kubwa kwenye kulipa kodi. Sasa mimi naomba niliombe Bunge lako, na naomba niiombe Wizara, kwamba sasa wakati umefika wa kuhakikisha kwamba Jeshi letu linapatiwa msamaha wa asilimia 100 kwa vifaa vyake vyote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa sababu kama sikosei tunatafsiri vifaa vya Jeshi kwamba ni silaha, kwa maana ya risasi na mizinga; hapana, tunakosea. Huko nyuma Jeshi letu lilikuwa na msamaha *fully* kwa vifaa vyake vyote inavyotumia. Inawezekana yalitokea mapungufu kwa watu wachache, lakini tumeliadhibu Jeshi kwa kutokuona kwamba hata uzi wa askari ni silaha. Sasa ombi langu, naiomba Serikali, hasa Wizara ya Fedha, ituletee mabadiliko ya sheria ili kuhakikisha kwamba Jeshi tunalipa msamaha kwa vifaa vyake vyote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa sababu kuitoza kodi Wizara ya Ulinzi ni sawasawa na kutoa pesa mfuko wa kushoto ukaweka kulia ukitegemea tija; haipo. Lakini pili, Jeshi hili ndilo linalotulinda, mimi sioni sababu ya kuwa na wasiwasi na chombo chetu halafu ukawapa nafasi baadhi ya watu pale bandarini wanakwenda kuchungulia Jeshi wameleta nini. Siyo kazi yetu vifaa vyetu kuchunguliwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo kama vifaa vyetu vimeletwa kama Jeshi, ombi langu, kwa sababu ndio wanaotulinda, tumewaruhusu na tumewapa fedha ya kununua vifaa hivyo, hatuna sababu ya kuendelea kuwatoza kodi Jeshi. Ombi langu, watuletee sheria tuibadilishe, tena iletwe kwa hati ya dharura ili tuipitishe hapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba kuendelea kwenye pointi yangu nyingine, kwamba pamoja na Serikali kuendelea kujitahidi bado naomba tuendelee kwa sababu sisi ndio tunaosimamia Wizara hii pamoja na nyingine mbili; bado tunahitajika kuhakikisha kwamba Jeshi letu hili, hasa kwenye suala la kuewezesha makazi yao na vifaa vyao, bado. Kwa sababu wenzetu hawa wanafanya kazi kubwa, ninaomba sana Serikali iendelee kuona namna gani tutaliongezea Bunge Jeshi letu hili ili makazi yao na vifaa vyao viendelee kuwa vya kisasa kama inavyotakiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwisho kabisa, sisi sote hapa ni wastaafu watarajiwa. Sote hapa kwa njia moja au nyingine ama tutastaafu kwa muda ukifika au tutastaafishwa na Mungu kwa sababu hatma ya kufa pia ipo. Sasa ninaomba basi, wale wenzetu wote ambao wamestaafu au wale ambao wametangulia mbele ya haki lakini wao wenyewe au wale warithi wao bado hawajapatiwa yale mafao yao, ninaomba sana, kwa sababu umepoteza mzazi au mlezi halafu yale mafao unapata usumbufu. Si kwa sababu Jeshi hawapati, hapana, ni kwa sababu bado Wizara ya Fedha haijatekeleza hoja ya kuwapa fedha ili waweze kuwalipa waliostaafu na waliofiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo naomba wenzetu hawa, hasa Wizara ya Fedha, wajue kwamba Jeshi ni chombo cha kujitolea. Sisi kama Serikali, kama Taifa, hatuna cha kuwalipa Jeshi ambao wametoa roho zao na nafasi zao kwa ajili yetu. Ninaomba sana tuwathamini, tuwalinde, kuwalinda wao ni pamoja na kulinda haki zao na waliowaacha ili waweze kujenga Taifa hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Vedastus Manyinyi Mathayo, atafuatiwa na Mheshimiwa Ussi Salum Pondeza, Mheshimiwa Grace Victor Tendega ajiandae.

**MHE. VEDASTUS M. MATHAYO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kunipa nafasi ili na mimi niweze kuchangia katika hii Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa.

Mheshimiwa Spika, kwanza nitumie nafasi hii kumpongeza Amiri Jeshi Mkuu na Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, mama yetu Samia Suluhu, ambaye ndiye kiongozi wetu Mkuu.

Mheshimiwa Spika, lakini nampongeza na Mheshimiwa Waziri, *CDF* wetu pamoja na vikosi vyetu vya ulinzi na usalama kwa kazi kubwa na nzuri ambayo mnaifanya kuhakikisha kwamba nchi yetu inakuwa tulivu na inaendelea kuwa salama.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, mimi ninayo maombi mawili na ushauri mmoja tu kwa ufupi. Ombi la kwanza linahusiana na wananchi wangu wa Kata ya Buhare kwenye Mtaa wa Mgalanjago**.** Wale wananchi kwenye hili eneo vilevile kuna eneo la Jeshi; lakini mnamo mwaka 2008 Jeshi liliweza kuongeza eneo ambalo walimega kwenye maeneo ambayo wananchi wangu walikuwa wanjipatia riziki, pale walikuwa wanafanya shughuli zao, na wakawa wameahidi kwamba watalipwa fidia. Sasa mchakato huo umeendelea kusema kweli mpaka sasa hawajapata fidia.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri, hawa watu wako kama 26 na barua yao ninayo hapa, naomba mhudumu aje aichukue akupatie hapo ili tuweze kuhakikisha kwamba basi hawa ndugu zetu wa Buhare ambao wanahitaji wapate hiyo fidia yao waweze kupata fidia ili waweze kuendelea na maisha yao kama kawaida.

Mheshimiwa Spika, la pili vilevile ni ombi ambalo bahati nzuri nilishakufikishia Mheshimiwa Waziri. Sasa nikuombe basi, kwamba kule eneo la Bukanga mnamo mwaka 1979 tulipata bahati ya kuwa na ulinzi pale, Jeshi lilichukua maeneo pale kwa hiyo wakahamia pale. Lakini katika yale maeneo waliyokuwa wamehamia, kumbe wakati wanapewa walipewa maeneo ambayo ni makubwa na mengine hawakuyafahamu.

Mheshimiwa Spika, kilichotokea ni kwamba wao kwa sababu hawakuyafahamu, wale wananchi waliishi katika baadhi ya maeneo. Sasa miaka imekwenda, Jeshi hawajui kama ni ya wale lakini na wale wananchi wanajua ni maeneo yao.

Mheshimiwa Spika, kilichokuja kutokea miaka mitatu iliyopita watu wa *MUWASA* wakaja kuomba eneo la kujenga tenki la maji, sasa sisi kama wahusika wa eneo hilo tukawapa ili wajenge tenki la maji. Wakati wanaendelea ku-*demarcate* maeneo haya ndiyo wakagundua kwamba lile ni eneo la Jeshi. Tayari kuna familia au kaya zaidi ya 60 zimeshakaa pale; nadhani hilo linahitaji sana busara ya Serikali ili iweze kwenda na kuona kwamba wale watu tunawafanyaje, kwa sababu Jeshi hawakufahamu na wale wananchi nao hawakufahamu.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri, ombi langu, nadhani hilo nilishakufikishia, kwamba hebu twende wote pale Musoma uende ukaangalie hali halisi halafu tushauriane tuone kwamba ni kwa kiasi gani tunaweza kuwasaidia wale wananchi ambao wamekaa kwenye hilo eneo ambalo ni pamoja na huruma ya Serikali kuwapatia ili waendelee kuishi basi maisha yao yaweze kuendelea salama.

Mheshimiwa Spika, baada ya hiyo, mengine mawili madogo, ninapenda tu kufahamu lile Shirika letu la Nyumbu ambalo ndiyo lilikuwa shirika lililoanza kuwa linatengeneza magari, siku hizi hatulisikii kabisa. Kwa hiyo ninapenda kupata tu maelezo kwamba hivi lile shirika letu limekufa au bado linaendelea.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hilo, niseme la mwisho ambalo ni ushauri wangu, kwamba tunatambua na huwa tunaona hata kule kwetu wakitangaza tu kwamba sasa kuna nafasi za Jeshi, JKT, wako vijana zaidi ya 1,000 wanakwenda pale kwenye ofisi ya mkuu wa wilaya kwa ajili ya kuanza kujiandikisha na kuhakikisha kwamba wanapambana ili wapate nafasi ile.

Mheshimiwa Spika, kinachotokea ni kwamba wale vijana watakaochukuliwa hata katika nchi nzima unakuta wanakaa mwaka au miaka miwili baadaye baadhi yao ndio wanapata nafasi ya kwenda katika vyombo vingine au katika majeshi mengine. Lakini vijana wengi baada ya miaka miwili tafsiri yake ni kwamba wanarudi nyumbani.

Mheshimiwa Spika, sasa wakirudi nyumbani, wale vijana bahati nzuri walishajifunza ukakamavu, walishajifunza ulinzi na mambo mengi ya kuwafanya waendeleze maisha yao, lakini kwa bahati mbaya sana sasa wanarudi kule hawana kazi ya kufanya. Kwa hiyo mimi nilidhani kwamba kuna haja kubwa ya Serikali kuangalia kwamba vijana hawa ni rasilimali kubwa ambao wakitumiwa vizuri kwanza wanaweza kusaidia sana kuendelea kuijenga nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo mimi nilidhani sasa hata kwenye mpango kama huu wa *BBT,* huu wa kilimo, ni kwa nini Serikali isitoe fedha za kutosha ikawapa JKT ili wale vijana watakapomaliza yale mafunzo badala ya kuwatupa nyumbani wapewe maeneo ya kujiendeleza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, na tena bahati nzuri kwa sababu wao walishafanya mazoezi, ni vijana wakakamavu, wanaweza wakapewa kama mkopo hata kama ni kilimo hicho, wakapata fedha na baadaye wakarudisha ili wale wengine wanaokuja, *intake* inayofuata, nao waweze kusaidika na mpango huo.

Mheshimiwa Spika, na kwa kufanya hivyo tunadhani kwamba kwanza itasaidia sana kupunguza tatizo la ajira, lakini vilevile

itasaidia sana kujenga uchumi wa nchi kwa sababu nchi nyingi zinazotuzunguka, majirani zetu, ukienda Kenya, Uganda, Rwanda na Burundi, wote wana mahitaji makubwa ya chakula. Sasa kwa sababu maeneo tunayo, vijana tunao, ardhi tunayo, kumbe tunaweza kuleta ajira kwa vijana wetu lakini vilevile tukawa tumesaidia uchumi wa nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo nadhani hili ni vizuri Wizara lakini na Serikali ingelipa kipaumbele, kwa sababu moja wapo ya majukumu makubwa ya Serikali yoyote ile ni kuhakikisha kwamba watu wake wanapata ajira. Kwa hiyo hiyo nayo ni *avenue* nyingine ambayo tunadhani tunaweza tukawasaidia vijana wetu.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Ussi Salum Pondeza, atafuatiwa na Mheshimiwa Grace Tendega, Mheshimiwa Nicholaus George Ngassa ajiandae.

**MHE. USSI SALUM PONDEZA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Nitumie nafasi hii kwanza kukushukuru wewe kwa kunipa nafasi hii kuchangia leo hii katika Bajeti yetu hii ya Ulinzi.

Mheshimiwa Spika, vilevile nitumie nafasi hii kumpongeza Amiri Jeshi Mkuu wa Jeshi letu hili la Wananchi wa Tanzania, mama yetu Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan. Vilevile nitumie nafasi hii kumpongeza pia Rais wetu wa Zanzibar kwa majukumu yake na ushirikiano ambao anautoa katika kuhakikisha amani inaendelea kutawala katika nchi yetu, lakini katika kushauriana na Amiri Jeshi Mkuu ambaye ni mama yetu Samia Suluhu Hassan katika kutekeleza yale majukumu ya amani na ulinzi katika nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, nitumie nafasi hii sasa kukupongeza wewe Waziri kwa jinsi ambavyo unafanya kazi katika nafasi hii muda mchache lakini jinsi gani umetufikisha hapa na umelifikisha hapa

Jeshi letu hili katika kuongoza. Nakushukuru sana na tunakupongeza sana Mheshimiwa Waziri.

Mheshimiwa Spika, mimi leo hapa nataka nitoe ushauri ambao nahisi ukiuchukua ikikupendeza itatusaidia sana katika Jeshi letu.

Mheshimiwa Spika, ushauri wangu wa kwanza ni katika kuhakikisha nafasi zile za ajira zinapotokea uliendeshe Jeshi kama ilivyo katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, yaani nafasi za ajira zinapotoka, umesema katika hotuba yako, nimekusikia, lakini unavyosema wewe na inavyochukuliwa haiko hivyo. Nina ushahidi, ukihitaji nitakupa, jinsi gani ambavyo hata mgawanyo wa ajira unapotoka katika Serikali yetu hi ya Muungano, tuna asilimia 79 kwa 21, lakini mgawanyo hauko hivyo, kama ambavyo washauri wako au watendaji wako labda wanakuelezea unakwenda sawa, lakini hauko sawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo lingine, nimekuwa nikisimama mara nyingi nikiuliza maswali yangu kuhusu Wizara yako, ni jambo la mipaka ya makambi ya Jeshi. Hili umelizungumza kuwa mmeanza, umetuonesha mpaka picha kuwa mnapima. Lakini kiuhalisia mipaka bado ni jambo moja ambalo linasumbua sana baina ya wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, na wananchi siyo kama Jeshi hawalipendi, Jeshi wanalipenda kwa sababu ni Jeshi lao na linafanya kazi vizuri, lakini sasa inapofika mipaka wakijenga tokea asili yao ilivyokuwa Jeshi wanasema sisi mpaka hapa, lakini hakuna mwenye hati. Jeshi tatizo kubwa ambalo lipo, lina makambi mengi hayana hati miliki, lakini wananchi wapo ambao wana hati lakini Jeshi kwa heshima yake au kwa nguvu zake ambazo ipo na tumeipa sisi, na ndivyo tunavyopenda Jeshi letu liwe lina nguvu, basi huwa linafanya mpaka mwisho wanavyotaka wao.

Mheshimiwa Spika, kuna jambo lingine ambalo nataka pia nikushauri. Kiwanda chetu cha Nyumbu kinafanya mambo mengi,

lakini yote kwa yote, fedha hakipati kwa muda, lakini na Serikali haitoi fedha kukiimarisha Kiwanda chetu cha Nyumbu kuhusu vifaa vyetu vinavyoweza kutengenezwa pale.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo nataka nishauri, leo hapa sina haja ya kushika shilingi ya Mheshimiwa Waziri, kazi yangu kubwa ni kumshauri yale ambayo nahisi ana mapungufu katika Wizara yake ila na ni kuboresha ili jeshi letu liendelee kuwa bora. SUMA JKT wamefanya kazi nzuri na wamefanya kazi kubwa katika nchi yetu hii lakini tatizo lao nalo kama Kiwanda cha Nyumbu bajeti wanaomba na pesa wanazoomba hawazipati kwa wakati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, namwomba Waziri, tukiziimarisha taasisi zetu mbili hizi Nyumbu na SUMA JKT tukiwapa fedha ambazo wanataka na kwa wakati basi zita-*create* hata ajira ambazo tumesema zipo rasmi na ambazo sio rasmi, basi wana uwezo wa ku-*create,* kwa sababu wamefanya mambo mengine ambayo sitaki niyarudie wachangiaji wengine wamesema hapa, mpaka Ikulu yetu ambayo tunajisifia sasa hivi kubwa, nzuri, lakini imefanywa chini ya usimamizi wa SUMA JKT na ni vitu ambavyo vinawezekana, lakini wakiwezeshwa ndio itaonekana. Sasa ni jukumu la Waziri.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo nataka labda nimshauri Waziri na ushauri wangu sio jambo kubwa sana, jinsi ambavyo zinavyotoka nafasi zile za vyeo, majengo, basi yatoke kwa uwiano na yatoke kwa wakati, lakini sana vyeo. Kuna maafisa ambao wanatoka kwenye JWT lakini wanafanya kazi katika SMZ ambao wamechukuliwa kwa ajili na wao ni Watanzania kama sisi, lakini unapofika wakati wa kuwa na wao wafikiriwe kwenye vyeo, kidogo wanasahaulika. Ningependa hili nalo Mheshimiwa Waziri alichukue kwa sababu yote hii inatokana na nini? Jeshi letu hili la Muungano linafanya kazi huku na huku. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ushauri wangu wa mwisho, ikimpendeza Mheshimiwa Waziri, Jeshi lina hospitali ya Bububu kule Zanzibar ambayo ndio hospitali kubwa na hospitali ya viongozi wa ngazi ya juu na ya mwisho ikitokea wamepata matatizo au wana shida

yoyote hata Mawaziri kama huyu akija, basi hospitali yao ya mwanzo huwa ni ya Bububu ambayo ni ya Jeshi, lakini ukiingalia hali yake sio nzuri kabisa, ina hali mbaya inahitaji ukarabati mkubwa na vifaatiba, vile vile na hata yale majengo yake hayako sawa, yaani ukiangalia hadhi yake na ya Jeshi letu la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na hospitali ile haviko sawa. Kwa hiyo, ushauri wangu nafikiri nitakuwa nimechangia pale ambapo Waziri anahitaji mchango wa sisi kama Wabunge, naomba leo mchango wangu uwe huu.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono asilimia mia moja. Ahsante sana kwa kunipa nafasi. *(Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge nilikuwa nimeshamtaja Mheshimiwa Grace Victor Tendega, lakini kabla hajachangia kuna wageni ambao walishatangazwa hapa. Viongozi wa Chama Cha Mapinduzi, Wilaya ya Karagwe wako sehemu gani mlikuwa mmeshatangazwa kabla hamjakuja. Mwenyekiti anaitwa Pascal Rwamgata, karibuni sana. *(Makofi)*

Wapo pia viongozi wa Halmashauri ya Wilaya ya Karagwe wakiongozwa na Mwenyekiti wa Halmashauri hiyo, Wallace Mashada. Karibuni sana. *(Makofi)*

Yupo pia Mgeni wa Mheshimiwa Wanu Ameir na yeye alishatangazwa na alikuwa hayupo, Salha Azizi. Karibu sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, wapo wageni ambao wamekuja kwa ajili ya mafunzo, Walimu na Walezi 70 wa Umoja wa Wamiliki wa *Day Care Centre* kutoka Jijini Dodoma. Karibuni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge jambo lingine la marekebisho kwenye Taarifa Rasmi za Bunge, wakati wakisomwa Wakuu wa Majeshi ya Ulinzi Wastaafu, tangazo lilikuwa linasomeka Jenerali George Mwita Waitara kama Mkuu wa Majeshi wa Sita, nimeletewa ujumbe hapa hilo jina linapaswa kuwa George Marwa Waitara, kwa

hiyo neno Mwita hapo liondoke liwekwe Marwa. Kwenye Taarifa Rasmi za Bunge hilo lirekebishwe.

Mheshimiwa Grace Victor Tendega, atafuatiwa na Mheshimiwa Nicholaus George Ngassa na Mheshimiwa Cosato David Chumi ajiandae.

**MHE. GRACE V. TENDEGA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa fursa nichangie katika bajeti hii. Nianze kwa kumpongeza Waziri, kwa kweli nampa pongezi kubwa kwa sababu ya usikivu na uvumilivu na utendaji kazi katika Wizara hiyo, hongera sana. Pia nampongeza Katibu Mkuu Doctor Faraji Mnyepe kwa kazi kubwa anayofanya pamoja na watendaji wote katika Wizara hii. Watendaji hawa wanafanya kazi kwa weledi mkubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nianze na Jeshi la Wananchi Tanzania, napenda kuwapongeza pia nao kwa utendaji mkubwa wa kazi zao uliotukuka na kwa gharama ya uhai wao. Hapa tulipo tunapumua na tuna starehe kabisa, lakini wenzetu wapo kazini wanafanya kazi bila kuchoka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kipekee nimpongeze Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. Samia Suluhu Hassan ambaye ndiye Amir Jeshi Mkuu kwa kutufanya tuwe na amani hii katika nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pamoja na pongezi hizo na utendaji wote wa Jeshi wanaoufanya, lakini kwa kweli fedha wanayopata ya maendeleo ni kidogo. Laiti wangepata fedha nyingi za maendeleo wangefanya vitu vikubwa sana. Tumetembelea maeneo mengi ambayo wanafanyia kazi, wanafanya kazi kubwa, kwa weledi mkubwa na kazi zao zinaonekana ukilinganisha na maeneo mengine ambayo tunakwenda. Kwa hiyo, niiombe Serikali iweze kutoa fedha wamepata asilimia 30.11 tu ya fedha za maendeleo. Kwa hiyo wangepata asilimia mia moja wangeweza kufanya kazi

kubwa Hivyo, niombe Serikali itoe fedha kwa asilimia mia moja bila kuleta mzaha kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jeshi letu ili liendane na ubora hasa kama ubora wa kimataifa, lazima bajeti yao inayotengwa, iliyoidhinishwa itolewe kwa wakati na itolewe kikamilifu. Ikitolewa hivyo, wanajeshi wetu watafanya kazi kwa uhakika, lakini pia Serikali ihakikishe kwamba maslahi ya wanajeshi wetu wanapata bila changamoto zozote.

Mheshimiwa Spika, kwa mfano tunaona kuna wanajeshi ambao wanaenda kwenye kozi mbalimbali sasa wanakwenda kule wanatoa fedha zao mfukoni za mshahara, ningependa kama ingekuwa Jeshi linapata asilimia mia moja fedha za maendeleo, hawa wangeweza kulipiwa kwa sababu kuna kozi ambazo ni za kuongeza teknolojia na mambo mengine ambayo ni ya kiubunifu ambayo wanatakiwa waweze kulipiwa. Kwa hiyo Serikali isifanye masihara katika kutoa fedha hizo.

Mheshimiwa Spika, niende katika mashirika yetu ya kimkakati, Nyumbu pamoja na Mzinga. Mashirika haya ni mashirika ya kimkakati yapo. Tumeona Nyumbu juzi tu hapa yametengeneza magari ya zimamoto na magari haya yamekuwa ni magari mazuri kabisa. Dunia yenyewe inatuona tumetengeneza magari ya zimamoto kwa fedha zetu hapa ndani. Sasa hawa Nyumbu wakiweza kupewa fedha za kutosha, wakiweza kupewa teknolojia za kisasa, wanaweza wakatengeneza vitu vingi vikiwemo vipuri mbalimbali wakauza ndani ya nchi na hata nje ya nchi. Wanaweza wakashirikiana na shirika la reli, wakasaidiana kuona wanatengeneza vipuri mbalimbali vikasaidia katika kupunguza mapato ambayo tunakwenda kununua katika nchi nyingine, tunatumia fedha za nje badala ya kutumia fedha zetu.

Mheshimiwa Spika, Nyumbu ilitoa mafunzo katika Nchi ya Uganda na Rwanda, lakini wenzetu wameshatupita,wako mbali kwa sababu ya kutekeleza azma ambayo Baba wa Taifa alikuwa anaitaka, kwa hiyo tuombe Serikali mweze kuchukulia kwa uzito,

shirika hili linaweza likatutoa likatupeleka mbali sana kwa kutengeneza vifaa mbalimbali vya kisasa na hii itatusaidia kuweza ku-*serve* fedha za ndani badala ya kutumia fedha za nje kwenda kununua labda chuma nje, tunaweza tukasaidia Jeshi letu likapata Mchuchuma na Liganga wakaweza kuona kuna kitengo gani wawape ili waweze kuvuna chuma kile kikatumika kwenye Shirika la Nyumbu ambalo litasaidia katika kuleta masuala mbalimbali ya kimaendeleo.

Mheshimiwa Spika, pia kuna changamoto ya ikama ya watumishi. Kuna watumishi wapo lakini kuna wale ambao ni hitaji katika shirika hilo ambao wana sifa ambazo zinatakiwa katika shirika hilo. Nimwombe Mheshimiwa Waziri na niiombe Serikali waweze kupeleka watumishi wa kutosha katika shirika hilo ili waweze kufanya kazi kwa ufanisi mkubwa, kwa sababu wanafanya kazi kwa weledi mkubwa. Ukifika pale unashangaa ni Tanzania ama sio Tanzania, ni kweli kabisa kwa kweli wenzetu wanajitoa, wanafanya kazi kwa weledi lakini tuwape fedha, Serikali wapeleke fedha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nikienda katika suala la JKT; Jeshi la Kujenga Taifa ni jeshi ambalo linaweza likatusaidia sana kututoa katika hali ya kiuchumi hasa tukishirikiana na vijana. Nimpongeze Mheshimiwa Waziri kwa mawazo ya kuona kwamba vijana wanatakiwa kusimamiwa kimaadili na mambo mengine yoyote, lakini bila fedha bado ni changamoto. JKT wametengewa asilimia sita tu ya fedha za maendeleo, itafanya nini? Tumeona wanajenga majengo mazuri. Tumeona wanashindwa hata kupeleka vijana JKT wengi kwa kukosa fedha za kuwahifadhi pale. Kuna vijana wengi wanatamani kwenda Jeshi la Kujenga Taifa hapa Wabunge wengi tunapigiwa simu kutoka huko, tunaomba vijana waende, lakini Mkuu wa Jeshi anashindwa awaweke wapi, hakuna hata sehemu ya kuwaweka. Kwa hiyo fedha zikienda, fedha nyingi za maendeleo tunaweza tuka-*accommodate* vijana wengi kwenda katika Jeshi hilo lakini wakafanya kazi nyingi za kilimo, za kiuchumi na za kuleta maendeleo katika Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo nimwombe Mheshimiwa Waziri aangalie kabisa kwamba *target* kubwa katika fedha ya Wizara JKT inachangia asilimia 73.3, hizo ndio fedha zinazochangiwa na JKT. Pale ambapo wanachangia fedha nyingi na Serikali ione namna ya kuwekeza zaidi ili kuweza kuongeza fedha nyingi Zaidi, kama tutawekeza kwa Jeshi la kujenga Taifa. Nimwombe Mheshimiwa Waziri aweze kufanya hivyo kwa Jeshi letu la Kujenga Taifa.

Mheshimiwa Spika, tumeona kwamba katika Jeshi la Kujenga Taifa kuna miradi ya kilimo ambayo inafanywa, lakini wanashindwa kuitekeleza kwa ukosefu wa fedha. Changamoto kubwa ni hiyo ya ukosefu wa fedha. Kwa hiyo niombe Serikali, Wizara ya Fedha wapeleke fedha kwa Wizara hii, hatuwezi kuwa salama bila ulinzi wa nchi hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa nafasi hii. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Nicholaus George Ngassa atafuatiwa na Mheshimiwa Cosato David Chumi na Mheshimiwa James Kimei ajiandae.

**MHE. NICHOLAUS G. NGASSA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi pia kuchangia Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa. Kwanza naunga mkono hoja ya Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, lakini pia naunga mkono Taarifa ya Kamati ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama.

Mheshimiwa Spika, duniani kote unapopima uwezo wa taasisi kwa maana ya uthabiti na uimara, basi kuna uhusiano wa moja kwa moja na uimara na uthabiti wa mkuu wa taasisi husika. Kwa mantiki hii nichukue nafasi hii kumpongeza Amir Jeshi Mkuu na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan kwa maboresho mbalimbali ambayo anayafanya kwenye Jeshi letu pamoja na vyombo vya ulinzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa kiwango kikubwa ili vyombo vya Ulinzi na Majeshi yaweze kufanya vizuri unahitajika uwekezaji mkubwa

sana katika teknolojia, katika rasilimali watu lakini pia na rasilimali fedha. Mheshimiwa Rais amechukua jitihada mbalimbali katika kuhakikisha Majeshi yetu yanafanya kazi vizuri na ndio maana tunaona Taifa letu liko imara na liko salama. Asubuhi nilikuwa namtania kaka yangu Lusinde, namwambia kuna mataifa Wabunge hawatembei mtaani wanazurura tu bila ulinzi au bastola kiunoni, lakini sisi Tanzania tuko imara kwa sababu ya ulinzi na usalama. Nampongeza sana Mheshimiwa Rais. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia nampongeza Mheshimiwa Waziri na Wataalam wake wote Wizarani, nampongeza Afande *CDF* Mkuu wa Majeshi, Majenerali na Makamanda na watumishi wote wa Jeshi pamoja na Wizara. Kazi nzuri wanayoifanya lakini pia na Makamanda wetu walioko maeneo mbalimbali duniani kwa ajili ya kuhakikisha wanaweka usalama mbalimbali kwa maana ya *peace keeping mission* na *peace building mission*. Wanajitolea unapoingia katika viwanja vya mapambano maana yake umeweka rehani usalama na uhai wako. Tunawapongeza sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba nichangie baadhi ya maeneo asubuhi hii katika hotuba hii ya Waziri kuhusu Wizara ya Ulinzi. Eneo la kwanza ningependa kuchangia ushiriki wa Jeshi letu kwenye usanifu na usimamizi wa miradi ya kitaifa na miradi ya kimkakati. Tunaamini kabisa Jeshini ni sehemu ya kwanza katika suala la *strategy,* mikakati na ulinzi. Serikali ningewashauri waongeze wigo wa ushiriki wa Jeshi letu katika usanifu wa miradi hii hususan miradi mikubwa ya kimkakati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimpongeze Waziri wa Ulinzi na Waziri wa Nishati hivi karibuni niliwaona wamekaa wakijadiliana kuhusu suala la kuimarisha ulinzi kwenye Mradi wa Bwawa letu la Umeme. Hii ni hatua nzuri wakati mwingine wawe wanashirikishana kwenye miradi mikubwa kama Serikali ya kimkakati. Miradi kama Liganga na Mchuchuma ambayo kwa sasa ndio *move* ya Taifa letu, wahakikishe wanashirikisha Jeshi letu kuanzia hatua za awali na Jeshi letu limejaliwa wataalam wengi, lina ma-*engineer* wa kila aina, lakini

lina watu wazalendo ambao watafanya kazi kwa maslahi ya Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hoja ya pili ambayo ningependa kuchangia mchana huu ni suala la Kamandi ya Jeshi la Akiba. Hili ni kama vile limesahaulika kidogo, naomba Wizara na Serikali waongeze nguvu katika kamandi hii. Tumekuwa tukitoa mafunzo kwa askari mgambo, lakini baada ya mafunzo tunajikuta tunawaacha mtaani kwa maana ya *notion* kwamba ni Jeshi la Akiba. Hawa watu waingizwe kwenye mfumo rasmi wa kiserikali, waweze kuwa-*monitor* kwa ukaribu, lakini pia waangalie namna ya kuweza kuwasaidia kwa namna yoyote, mbeleni wawe na mipango hata ya kuimarisha bima za afya ili waweze kuwa tayari gado, wakiwa *fit,* hata inapotokea dharura yoyote watakapowahitaji basi wanaungana na Majeshi yetu katika *operation* mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Sheria ya Jeshi, *Military Act* ukijaribu kuangalia hawa watu kunapotokea tafrani, hadhi yao ni sawa na askari wetu ambao wako kazini. Kwa hiyo na wenyewe katika kipindi ambacho ni cha amani na utulivu, basi tujaribu kuangalia namna ambavyo tunaweza tuka wa-*accommodate* na waka-*feel* kwamba ni sehemu ya Jeshi letu la Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo ningependa kuchangia mchana huu ni ujenzi wa anga za ndege za Jeshi ambalo Mheshimiwa Fakharia aliliongelea, niwasisitize tu na kuwaomba Serikali wakamilishe ni anga za kisasa na kubwa ambazo zinaweza zika-*accommodate* ndege zetu hususan hii ya Dodoma ambapo kwa sasa ni makao makuu, tungependa kuona hivi karibuni imeanza kufanya kazi ili tuweze kuimarisha ulinzi wa Taifa letu na Makao Makuu ya Nchi yetu. Kama tunavyojua tumezindua Ikulu yetu kwa sasa ya Chamwino, basi na Jeshi liwe kamili kamili kabisa kwa lolote ambalo litakuwa tayari kwa ajili ya kukabiliana nalo.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo ningependa kuchangia ni Mradi wa Nyumbu *TATC-Tanzania Automotive*

*Technology Centre* ni kituo cha Jeshi kwenye teknolojia, tunaomba Serikali na Wizara waongeze fedha. Kamati tulipita pale tukaona maendeleo yaliyokuwepo mwaka jana na mwaka huu kuna *improvement* kubwa, tuwatie moyo, waendelee kupambana. Naamini kwamba Jeshini ukiwekeza teknolojia Zaidi, basi tutasonga mbele, utafiti utafanyika kwa kiwango kikubwa, lakini tutabuni mambo makubwa ambayo yatakuwa yanatusaidia katika ulinzi na usalama wa Taifa letu na kupiga hatua mbele katika *level* ya teknolojia.

Mheshimiwa Spika, jambo la mwisho ambalo ningependa kulichangia na kulisisitiza ambalo baadhi ya Waheshimiwa wamelichangia ni kuhusu msamaha wa kodi kwenye vifaa vya Jeshi. Mheshimiwa Waziri ajaribu kukaa na Waziri wa Fedha hili jambo walione ili itakapokuja Sheria ya Fedha tuliangalie kwa mapana. Haiwezekani tukawa na Jeshi ambalo tumeliamini kulinda mipaka ya nchi, tumeweka usalama wetu mikononi mwa Jeshi letu, lakini inapokuja kwenye *clearance* ya vifaa tunaanza kuwa na kigugumizi. Ni aibu sana, tulifanyie kazi, sisi tumeamua kulisemea Jeshi kwa kuwa linafanya uzalendo wa Taifa letu, linatulinda usiku na mchana na sisi kama Taifa tumebaki imara.

Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Cosato David Chumi atafuatiwa na Dkt. Alfred James Kimea na Mheshimiwa Elibariki Immanuel Kingu ajiandae.

**MHE. COSATO D. CHUMI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia siku ya leo katika Wizara yetu. Nianze kwa kumshukuru na kumpongeza sana Mheshimiwa Rais ambaye ndiye Amir Jeshi Mkuu wa Taifa letu na mara kadhaa nimesema hapa Mheshimiwa Rais kama mwanadiplomasia namba moja amekuwa akiitendea haki nafasi yake kwa sababu tumeendelea kuwa Taifa ambalo linaaminika katika ulinzi wa amani duniani, katika ulinzi wa amani katika nchi mbalimbali za kiafrika. Hii ni kutokana na

kazi nzuri ambazo Mheshimiwa Rais anazifanya kuendelea kutuheshimisha katika Jumuiya ya kimataifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia nitumie nafasi hii kumshukuru na kumpongeza Mheshimiwa Waziri, kama jina lake lilivyo Innocent yuko *very innocent,* msikivu na Kamati tunafanya nae kazi vizuri sana pamoja na Katibu Mkuu Faraji Mnyepe na viongozi wa Jeshi kwa maana Mkuu wa Majeshi ya Ulinzi Jenerali Jacob Mkunda, pamoja na Mnadhimu Mkuu wa Jeshi Luteni Jenerali Salum Haji Othuman ambae mara nyingi tumekuwa nae kwenye vikao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ukiona nchi imetulia kama alivyosema Mheshimiwa Ngasa, tunafanya shughuli zetu, tunashiriki kazi za Bunge, wakulima wanaenda mashambani, wananchi wangu Mafinga wanaenda kuchana mbao na kadhalika, maana yake wako watu hawalali usingizi. Kati ya watu ambao hawalali usingizi ni pamoja na wenzetu wa Jeshi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, huwa namwambia mtu, ukimwona Mwanajeshi vyovyote alivyo wewe mheshimu tu, awe na maji ya kunde kama mimi, kimo cha kati kama mimi vyovyote alivyo mheshimu tu, kwa sababu wanafanya kazi ya kutukuka ya kukesha. Sisi hatuwezi kujua tutakwenda huko masokoni, tutakwenda kunywa soda na kadhalika, tutakwenda kwenye ibada tutakwenda kufanya kila kitu lakini kuna watu ambao wanakesha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa sababu hii kama alivyosema Mheshimiwa Fakharia, kazi ambayo imefanyika pale Ikulu ni mojawapo wa mfano kwamba, vyombo vyetu vikiaminiwa na kuwezeshwa vinaweza vikafanya maajabu makubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nitoe ushauri ambao nimetoa nadhani kama mara tatu mfululizo. Kama ambavyo umeona ile kazi ya Ikulu ya kuheshimisha, nenda Chita utaenda kuona maajabu, kwa wale ambao wamefika wanaweza kujionea jinsi ambavyo kilimo cha mpunga kinafanyika kwa weledi mkubwa sana. Ndiyo maana mara

nyingi nashauri na nimesema hata mwaka jana, hii nchi yetu mimi nilisikitika na lazima niseme ukweli, Waziri wa Viwanda na Biashara anatoa vibali tuagize mchele tani 90,000 Tanzania, kuna vitu Hapana! Sasa, namna ya kusema hapana ni nini? Tuwekeze JKT, nilisema mwaka jana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tuwezesheni JKT na kupitia SUMA JKT, wape *target* tu miaka miwili uone kama utaagiza mafuta ya kula kutoka nje ya nchi hii, uone kama utatoa vibali vya kuagiza mchele kutoka nje. Tumefanya mambo mangapi kwa majaribio? Hebu tufumbe macho tukipe mkopo, tukiwezeshe, tuone maajabu.

**MHE. FELISTA D. NJAU:** Mheshimiwa Spika, taarifa.

**SPIKA:** Mheshimiwa Cosato Chumi, kuna taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Felista Njau.

**TAARIFA**

**MHE. FELISTA D. NJAU:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Nataka nimpe mchangiaji taarifa kwamba kwa ukosefu wa fedha JKT wana hekari 12,500 lakini mwaka huu imekuwa ni pori na miundombinu iko ardhini, kwa hiyo wamekosa fedha wangekuwa na fedha wangeweza kwenda mbele. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Cosato Chumi, unaipokea taarifa hiyo?

**MHE. COSATO D. CHUMI:** Mheshimiwa Spika, naipokea taarifa hiyo kwa mikono miwili na huyu kama Mjumbe wa Kamati nadhani amenielewa.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ninachotaka niseme ni nini? Kama Taifa kijiografia tunayo nafasi ya kunufaika na kuneemeka kutokana na *geographical position,* sasa miongoni mwa watu wanaoweza kutusaidia ni hivi vyombo, lakini hawawezi kutusaidia kama hatuviwezeshi ipasavyo. Ushauri wangu ni kwamba tuviwezeshe hivi vyombo na tuwape fedha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, suala la pili na hili napenda kwa dhati ya moyo wangu nikushukuru wewe binafsi. Mimi na baadhi ya wenzangu tulienda JKT mwaka jana, hapa ndipo ambapo nataka nitoe ushauri na nisisitize. Kumekuwepo nafasi haba za vijana kwenda JKT wanaomaliza Kidato cha Sita, mara nyingi pengine kwa kukosa uelewa tunaona kama vile JKT imewanyima nafasi vijana, Hapana! Hawana vitendeakazi, hawana *facilities.* Kwa hiyo, nashauri Wizara ya Fedha tuwawezeshe JKT wajenge mahanga ya kutosha ili kusudi vijana wengi waende JKT.

Mheshimiwa Spika, zamani nilidhani JKT ni maguvu tu, lakini tulienda pale unakaa darasni wakati mwingine mpaka saa nne usiku, unafundishwa uzalendo, kuna vitu vingi. Kwa nafasi hii ninashauri na pengine ushauri huu unaweza usipokelewe vizuri sana, hata Watumishi wa Umma wanapoajiriwa kama ambavyo tunafanya semina elekezi, waende JKT hata mwezi mmoja. mimi nakwambia tutaona mabadiliko makubwa sana katika nchi yetu, kwa maana ya *mindset,* tabia, utendaji na uzalendo kwa ujumla. Simaanishi waliopo kwamba siyo wazalendo lakini itawaongezea uzalendo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa kumalizia yapo mambo mawili. Jana tumejadili Wizara ya Uchukuzi hapa na tumesema mambo muhimu ambayo tunatakiwa tufanye katika kuboresha bandari yetu. Wenzetu hawa wakileta vifaa tayari wamekwisha jenga *bonded warehouse,* tunaomba na tunaishauri Serikali waruhusiwe wakishachukua vifaa vyao vya Jeshi wakavihifadhi kwenye *bonded warehouse* wakati taratibu zingine zinaendelea, tusivi – *expose* pale.

Mheshimiwa Spika, jambo la pili ni la kisheria, tuniomba Serikali ilete sheria ili kusidi vile vifaa vya wenzetu visitozwe kodi. Kwa sababu kama alivyosema Mheshimiwa Zahor, ukisema tu ni *military equipment* mwingine anadhani ni vile vifaru tu hata buti ni kifaa cha Jeshi. Kwa hiyo, niombe sana kama naeleweka hii tuone haya mambo mawili. Moja, hili la kwanza nadhani ni *administrative* tu

kwamba *bonded warehouse* zao wanazo zitumike kuhifadhia vifaa vyao na hilo la *TRA*.

Mheshimiwa Spika, jambo la mwisho ni la wastaafu. Mimi napokea maombi kutoka Mafinga, sasa kidogo inanichanganya maana ni Mjumbe wa Kamati, nimepokea *recently* wakati tumeshamaliza Vikao vya Kamati, nikiwauliza wastaafu waliokuwa Wanajeshi kwanza wanaomba kwamba ile pensheni yao wanadhani kwa kuwa walistaafu wakiwa katika vyeo vya chini na wengine walilazimika kustaafu labda kutokana na maradhi kwa hiyo ile pesheni yao ni nyembamba kidogo. Kwa hiyo, wana ombi Serikali iwaangalie wastaafu pia kuwafikishia kwa wakati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa kumalizia niliona hapa timu ya JKT, imepanda Ligi Kuu, mimi ni mwanamichezo nampongeza sana Kocha Ndugu Malale Hamsini pia na JKT Queen ya wanawake Kocha Ali Ali kwa kuchukua ubingwa wa Ligi Kuu ya Wanawake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo nakushukuru sana, naunga mkono hoja na Mungu akubariki sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Dkt. Alfred James Kimea, atafuatiwa na Mheshimiwa Elibariki Immanuel Kingu, Mheshimiwa Jesca Msambatavangu ajiandae.

**MHE. DKT. ALFRED J. KIMEA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii na mimi kuweze kuchangia kwenye bajeti ya Wizara hii.

Mheshimiwa Spika, awali ya yote napende kumpongrza Rais wetu Mama Samia Suluhu Hassan, ambae ndiye Amiri Jeshi Mkuu na Kiongozi mkubwa wa Majeshi haya yote, niendelee kumpongeza kwa kazi kubwa ambayo anaifanya kuhakikisha nchi yetu inaendelea kuwa salama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia ninatumia fursa hii kumpongeza Kiongozi wa Wizara hii Waziri wetu Mheshimiwa Innocent Bashungwa, kwa kazi kubwa ambayo anaifanya pia tumpongeze Katibu Mkuu, Ndugu yetu Dkt. Faraji Mnyepe kwa kazi kubwa ambayo anaifanya na kwa ushirikiano wake mkubwa ambao anautoa kwa Kamati na Watanzania kwa ujumla. Niwapongeza pia Majemedari na Makamanda wote ndani ya nchi hii ambao wanafanya kazi kubwa kuhakikisha nchi yetu inaendelea kuwa salama.

Mheshimiwa Spika, nina mambo machache sana ya kuchangia leo, jambo la kwanza, jambo hili limezungumzwa na Wabunge wengi, naomba Waziri wa Fedha apate kutuambie anafanya nini juu ya suala hili la changamoto ya kikodi.

Mheshimiwa Spika, tunafahamu kazi kubwa ambayo Jeshi letu linafanya, tuwasaidie hawa watu waendelee kuifanya kazi yao vizuri kwa kuwapatia msamaha wa kodi asilimia 100. Waziri wa Fedha, akae chini na Wizara hii wapate ku–*define* vifaa vya kijeshi ni nini? Vifaa vya kijeshi siyo bunduki au risasi peke yake. Kitu chochote kinachoagizwa na Jeshi letu hivyo ni vifaa vya kijeshi. Hivyo, Wabunge tunaomba ndugu zetu hawa wapatiwe msamaha wa asilimia 100. Wabunge wengi wamezungumza sitaki kuongea sana kwenye *detail* kwa sababu najua Waziri wa Fedha atakuwa amekwishachukua atalifanyia kazi.

Mheshimiwa Spika, suala la pili, limeongelewa na ndugu yangu Chumi hapa mwisho. Hawa ndugu zetu ili kuhakikisha vifaa vyao havikai bandarini muda mrefu, wametengeneza *bonded warehouse* zao lakini *TRA* bado Inawakatilia kupeleka vifaa vyao kwenye *bonded warehouse* zao wakiwa wanaendelea na *process* za *clearing*.

Mheshimiwa Spika, tunaomba watu wa *TRA* waweze kutoa *go ahead* Jeshi letu likapate kutumia *bonded warehouse* zao kuhifadhi mizigo yao wakiwa wanafanya *process* za kufanya *clearing*. Vifaa vyao kukaa kwa muda mrefu pale kwanza ni aibu kwa Taifa letu,

kwa watu ambao wanajitoa kwa Taifa hili kuweza kuzuia mizigo yao halafu iko pale bandarini.

Mheshimiwa Spika, mwisho, muda mwingine huwa hatufahamu wanaagiza vitu gani kwa matumizi gani? Siku moja tutakuja kukimbiana pale bandarini inawezekana kuna vitu havistahili kukaa kwa muda mrefu pale kwenye bandari yetu, waruhusuni watu hawa kwa kuwa ni ngumu kuweza kumwelezea kila mtu kitu gani kiko kwenye ma - *container* yao kwa ajili ya *issue* za kiusalama, waruhusiwe wawe na *bonded warehouse* zao vifaa vyao vikija vyote vihifadhiwe huko kama mnataka watu wenu wa *TRA* wawe huko *clearing* ifanyike vifaa vyao vikiwa kwenye maghala yao na siyo ndani ya bandari yetu pia itapunguzia mzigo bandari yetu ambayo tunataka iwe ya kisasa na ihudumie mambo mengine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwenye suala la kikodi ninaamini kabisa Waziri wa Fedha leo katika kuhitimisha ataliongelea suala hili na atatuhakikishia kwamba moja, kutakuwa na msamaha wa asilimia 100 lakini pili, wataruhusu Jeshi letu liweke vifaa kwenye *bonded warehouse* zao. Hivyo ni vitu viwili ambavyo nilitaka kuchangia.

Mheshimiwa Spika, jambo la mwisho pia limeongelewa na watu wengi ni Shirika la Nyumbu. Naomba niongelee kwa uchache Shirika hili la Nyumbu. Kwanza, napenda kuipongeza Serikali hasa viongozi wetu waasisi wa Taifa hili kwa kuwa na maono haya makubwa ya kuwa na shirika hili. Nahisi watu wengi hawafahamu ndoto za Rais wetu wa Kwanza kuanziasha shirika hili. Alikuwa anatamani siku moja Tanzania iwe inajitosheleza kwenye masuala ya magari, vifaa vya kijeshi, kila kitu kifanyike ndani ya nchi yetu, lakini changamoto ya Serikali yetu baada ya hapo hatukuwa *committed* kwenye shirika lile. Ninaiomba Serikali iwe *Committed* ili shirika hili liende mbali zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda kuwapongeza viongozi wa Shirika hili. Shirika hili limejiongezea uwezo mkubwa sana, ukifika pale utaona mambo makubwa ambayo yanafanywa kwenye shirika lile.

Wanatengeneza magari ya Kijeshi, wanatengeneza magari ya zima moto, wanatengeneza vifaa vya nyumbani, majiko na vitu vingine lakini kikubwa zaidi wanatengeneza hadi vifaa vya kilimo ambapo nchi yetu inatamani kupeleka suala la kilimo mbali zaidi.

Mheshimiwa Spika, Serikali iwe *committed* iwapeleke fedha mimi ninaamini kabisa nchi yetu itafika mbali sana tukiamua kuwekeza kwenye shirika hili. *(Makofi)*

**MHE. ALI JUMA MOHAMED:** Mheshimiwa Spika, taarifa.

**SPIKA:** Nani mtoa taarifa? Mheshimiwa Ali Mohamed.

**TAARIFA**

**MHE. ALI JUMA MOHAMED:** Mheshimiwa Spika, napenda nimpe taarifa mchangiaji anaeendelea kwamba licha ya changamoto mbalimbali na mafanikio ambayo yanatokea nchini kutokana na Jeshi letu, lakini Jeshi letu limekuwa likiijengea sifa sana nchi yetu ya Tanzania hasa pale linaposhiriki katika *mission* mbalimbali za Kimataifa. Hii imepelekea kupata sifa kwenye Jumuiya ya Kimataifa, sasa ikiwa Jumuiya ya Kimataifa inathamini sana Jeshi letu, kwa nini Serikali yetu ishindwe kutoa uwezo wa kifedha kwa ajili ya Jeshi letu? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Kimea, unaipokea taarifa hiyo?

**MHE. DKT. ALFRED J. KIMEA:** Mheshimiwa Spika, ninaipokea taarifa kwa mikono yote miwili. Kwa hiyo, ninachotaka kusisitiza hapa Serikali yetu iwe *committed* kwenye shirika hili ninaamini kabisa tutaenda mbali.

Mheshimiwa Spika, tukiamua kwenye nchi hii kwamba: (i) Magari yote ya zima moto yasiagizwe kutoka nje ya nchi, yatengenezwe kwenye shirika hili. (ii)Magari yote ya kuzolea taka kwenye nchi yetu yaagizwe kutoka kwenye shirika hili. Tukisema *ambulance* zote zitengenezwe kwenye shirika hili, magari ya Majeshi

yetu ya Jeshi la Polisi, Magereza yote yaagizwe toka shirika hili, ninaamini shirika linao uwezo, tumetembelea pale tumeona, tukiamua ku - *invest* pale ninaamini watatengeneza vitu kwa ajili ya nchi yetu na tutaweza kuuza hata nje ya nchi.

Mheshimiwa Spika, hivyo, ninaiomba Serikali iweze kulipatia fedha shirika hili nina amini kabisa katika uchumi wa nchi yetu kwanza litatengeneza ajira nyingi sana.

Mheshimiwa Spika, nilikuwa na hayo machache ya kuchangia. Ninapenda kuunga mkono hoja hii na tupo pamoja Wanakamati tutaendelea kushirikiana nao. Ahsante sana kwa kunipa muda huu. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Elibariki Immanuel Kingu, atafuatiwa na Mheshimiwa Jesca Msambatavangu, Mheshimiwa Maimuna Pathan ajiandae.

**MHE. ELIBARIKI I. KINGU:** Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa nitumie nafasi hii kukushukuru sana wewe Kiongozi wetu wa Muhimili huu kwa kazi kubwa ya kulitumikia Taifa kwa njia ya Muhimili wako unayoifanya. Pia, nikushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuchangia Wizara hii muhimu kabisa ambayo inagusa maslahi mapana ya amani, ulinzi, usalama na maendeleo ya Taifa letu kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, nitumie fursa hii kumpongrza sana Amiri Jeshi Mkuu wa Majeshi ya Ulinzi na Usalama Dkt. Samia Suluhu Hassan, ni wazi toka Dkt. Samia Suluhu Hassan ameingia madarakani chini ya uongozi wake, mipaka ya Taifa letu iko salama, ndani na nje Taifa letu liko salama, pale ambapo pamejitokeza mambo ambayo yangeweza kufanya *instability* ya amani ya Taifa letu Rais wetu kupitia Vyombo vyake vya Ulinzi na Usalama wameendelea kusimama imara, Taifa letu liko salama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nitumie fursa hii kumpongeza sana Waziri wetu wa Ulinzi, Kaka yangu Mheshimiwa Innocent Bashungwa, kwa unyenyekevu wake na uzalendo wake mkubwa uliompelekea Rais

kumwamini na kumpa kuongoza Wizara hii muhimu sana katika Taifa letu. Hongera sana Mheshimiwa Bashungwa, endelea kuwa mnyenyekevu namna hiyo, uendelee kuwatumikia Watanzania kwa maslahi ya Taifa letu na kwa maslahi ya *welfare* ya watu wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninaomba nitoe ushauri ufuataao kwa Taifa langu na kwa Wizara yangu hii muhimu ninayoipenda sana. Kwanza kabisa, takwimu zinaonesha mwaka 2016 vijana waliohitimu Kidato cha Sita walikuwa 65,000. Takwimu za mwaka jana zinaonesha vijana waliohitimu Kidato cha Sita walikuwa takribani 95,000. Ninaomba nitoe wito kwamba pawepo na mwingiliano wa Wizara zifuatazo:-

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Ulinzi, Wizara ya Kilimo, Wizara inayoshughulikia Mambo ya Vijana ambayo iko chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu, pamoja na Wizara ya Mifugo.

Mheshimiwa Spika, ninachokisema hiki ni kwamba amezungumza Kaka yangu Mheshimiwa Cosato Chumi, vijana wanaohitimu JKT, tunazungumza habari ya kujenga ajira za vijana, hili jambo ni rahisi sana, fedha ambazo Serikali inazitenga katika Wizara ya Kilimo, pakiwepo na mikakati kati ya Wizara ya Ulinzi, Wizara ya Kilimo, Wizara ya Mifugo pamoja na Wizara hii iliyoko chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu inayoshughulikia mambo ya vijana, tunaweza tukafanya mkakati rahisi sana.

Mheshimiwa Spika, fedha za kilimo za kimkakati kwa vijana ambazo sasa hivi, kwa mfano Wizara ya Kilimo walikuwa wanakimbizana kwenda kule kwenye maeneo yetu kutafuta vijana ni jambo jema, nataka nikwambie kwa nidhamu ambayo Jeshi letu la Wananchi wa Tanzania inalijenga kwa vijana wa Kitanzania, vijana wale huwa wanachukuliwa wanajenga *component* ya uzalendo wa nchi nzima. Wanachukuliwa kutoka Jimboni kwangu, wanachukuliwa Mtwara, Mwanza na maeneo yote ya nchi na wengi wao wanatoka vijijini, kuna ugumu gani vijana hawa JKT wakatafutiwa mashamba ya kuzalisha, wakaingizwa kwenye kilimo?

Fedha zinazotokana na bajeti tunapeleka kwenye kilimo, tatizo la ajira tunalolizungumza litatafutiwa *solution* ya kudumu tutakuwa tumelitibu tatizo la ajira. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, natoa wito na ninawaomba Wizara, nina imani Rais ameteua vijana mahiri tunawaamini, Kaka yangu Mheshimiwa Katambi tunajua uwezo wako, Kaka yangu Mheshimiwa Mavunde Kijana mwenzangu tunajua uzalendo na uwezo wako, Mheshimiwa Bashungwa tunajua uzalendo na uwezo wako. Fanyeni *coordination* ya vijana wa JKT haya mabilioni Mama Samia aliyoyatoa mama yetu aandike *record* ya ku-*recruit* vijana wengi katika kuwapa ajira wanaotokana na Sekta ya Kilimo kupitia JKT. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hili nakuambia likifanyika jambo la kulia kwa sababu hamna ajira litakuwa historia na jambo hili nalizungumza ni mara ya tisa mchango huu nautoa katika Bunge hili lako Tukufu, ninawaomba Mawaziri wangu tekelezeni jambo hili litapata baraka na mtafanikiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo la pili, pamoja na kumpongeza Kaka yangu Jacob Mkunda, Jenerali wetu na Kiongozi wetu wa Majeshi yetu, ninatoa wito kuwa dunia inabadilika, sayansi na teknolojia inabadilika, ninaamni kabisa Jeshi letu ni Jeshi lenye nidhamu limefanya ukombozi wa mataifa ya Kusini, limefanya ukombozi wa kulinda mataifa mengi dunia, natoa wito ni wakati sasa ya kuli - *modernize* Jeshi letu liwe na vifaa vya kisasa, adui akitaka kuweka mguu kwenye nchi yetu wakati wowote tunao uwezo wa kukabiliana naye. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, natoa wito, Rais wetu sasa hivi anatekeleza miradi ya kimkakati, tunajenga mradi wa Bwawa la Mwalimu Nyeyere, tunajenga mradi wa *SGR* tunataka kwenda kwenye uchumi wa bahari, tunahitaji bahari yetu iwe salama, tunahitaji miundombinu tunayojenga iwe salama. Kwa maana hiyo, ninatoa wito tununue vifaa vya kisasa vya kijeshi tuwe na ma – *artillery* ya kisasa tuwe na *anti-aircraft* ya kisasa ili kusudi tuwe na

uhakika. Taifa letu lina ulinzi na usalama wakati wote na Mungu aendelee kuwapigania wazalendo wetu wanaotoa maisha yao kwa ajili ya kulinda Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo la tatu ninalotaka kulisemea ni wakati muafaka sasa Jeshi letu la Wananchi lipewe fursa ya kujenga chuo cha kisasa, Chuo Kikuu cha kisasa kitakachoweza kutoa mafunzo ya teknolojia ya kisasa Jeshini. Itakayoweza kutoa mafunzo kwa wanajeshi wetu kuji-*equip* na teknolojia za kisasa kwa sababu dunia imebadilika. Mambo ya kutumia mavifaru yale ya mwaka 1961 yameshapitwa na wakati, dunia sasa hivi imekwenda mbele. Ninatoa wito Jeshi letu litengewe bajeti kwa siku zinazokuja, wajengewe chuo cha kisasa kitakachoweza kutoa mafunzo ya kiutalaam ya Wanajeshi wetu ambao baadhi yao ndiyo watakwenda kui-*feed* Nyumbu, hao baadhi yao watakwenda ku-*feed* vyuo vyetu vya kisasa ambavyo Jeshi letu linavimiliki kwa maslahi ya Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo la mwisho siyo kwa umuhimu lakini ni la mwisho, nilikua naomba nitoe ushauri. Naomba hili ya vijana nililolizungumza wa JKT katika miradi niliyoitaja tuwekeane malengo. Tuseme kwa mfano, mwaka huu umemaliza vijana 95,000 katika sekondari zetu za *high school*, tunaweza tukasema mwaka huu tunaweka *project* ya miaka kumi, mwaka huu wa kwanza tutaanza na asilimia 33, mwaka unaokuja asilimia 40 na kuendelea, nataka nikuambie Mawaziri hawa wazalendo vijana wenzangu watakuwa wamesaidia Taifa hili kuweka *record* kubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwisho kabisa niwapongeze sana Jeshi la Wananchi wa Tanzania, nimeona leo Mabregedia Jenerali wanawake, nimeona leo wanawake wakitajwa humu kwenye Jeshi lao lakini kubwa zaidi nimefarijika sana na mimi nataka niwaambie nasi humu Bungeni tunae Brigedia Tulia. Huko nje mnaupiga mwingi na sisi humu ndani yuko Brigedia Tulia anaendelea kufanya kazi ya kizalendo na hivi karibuni Taifa na watu wake tunamuombea Brigedia huyu akaongoze chombo kikubwa duniani akawe Rais wa Bunge la Dunia, ama namna gani jamani Wabunge? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia niwaombe Jeshi la Wananchi wa Tanzania hawa Makamanda tumewaona wamekuja hapa, tumeona wamechukua mikanda ya medeni kwenye kupigana, wapo akina Simbu wamechukua medani kwenye riadha. Jeshi Kamanda Mkunda nakuomba unanisikiliza Kaka yangu pamoja Waziri hembu nendeni mkawa - *promote* hawa vijana. Tunataka tuwaone kwa kazi kubwa wanayoifanya vijana hawa waje Bungeni wamechafuka nyota, wanaleta sifa na heshima kwa Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, nakushukuru, Mungu Ibariki Tanzania, Mungu libariki Jeshi la Wanachi wa Tanzania, Mungu mbariki Amiri Jeshi, Rais Mama yetu Daktari Samia Suluhu Hassan, amani ya Taifa letu iendelee kutawala. Ahsanteni kwa kunisikiliza. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Jesca Msambatavangu atafuatiwa na Mheshimiwa Maimuna Pathan, Mheshimiwa Patrobass Katambi ajiandae.

**MHE. JESCA J. MSAMBATAVANGU:** Mheshimiwa Spika, ahsante, nashukuru kwa kunipa nafasi hii na mimi niungane na Waheshimiwa Wabunge wenzangu katika kulipongeza Jeshi letu kwa kazi kubwa wanayofanya, hasa kuhakikisha usalama wa nchi yetu na ulinzi wa nchi yetu tunakuwa salama sana.

Mheshimiwa Spika, leo ningeomba niongelee kipengele cha JKT, yapo mambo mengi yanatuumiza akili, tunachanganyikiwa hatujui tunafanya nini, kumbe tuna vyombo humu ndani ambavyo hatujavitumia sawa sawa na kama tungevitumia matatizo yetu makubwa yanayotukosesha usingizi, mambo kama ajira kwa vijana, mambo kama maadili kwenye Taifa letu, mambo kama uzalendo, mambo kama ukakamavu, tayari tungekuwa tumeweza kwa kiasi kikubwa sana kuyatatua.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri amesoma utekelezaji wa Ilani kile kipengele (H) na wote hapa tupo kutekeleza Ilani ya Chama cha Mapinduzi, na Chama cha Mapinduzi kina viongozi makini wenye uelewa mkubwa wanaoona mbali sana. Wametuelekeza au wamekuelekeza Mheshimiwa Waziri katika utekelezaji wa Ilani (H), kuimarisha Jeshi la Kujenga Taifa (JKT) na Jeshi la Kujenga Uchumi (JKU) ili viwe vyombo vya kuwapatia vijana ujuzi wa kujiajiri na kuajiriwa na pia kuwa vyombo mahiri vya huduma na uzalishaji mali hasa katika ujenzi wa kilimo, ufugaji, uvuvi na maeneo mengine. (I) inasema hivi, ili uweze kutekeleza hilo (H) lazima sasa kupanua na kuongeza idadi ya Kambi za JKT na JKU. Ili kuwezesha vijana wengi zaidi, wakiwemo wahitimu wote kwa sababu JKT ina makundi mawili ya vijana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tuna vijana tunawachukua kwa mujibu wa sheria na tunao vijana tunaowachukua kwa kujitolea. Wale wa kwa kujitolea ndiyo Ilani inasema kuwawezesha wengi, wale wa mujibu wa sheria Kidato cha Sita ni wote. Utalitekelezaje hili lazima uhakikishe kwamba unapanua na kuongeza Kambi za JKT na JKU.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri ukisimama hapa utuambie safari hii unafanya nini katika kuongeza makambi, tunataka vijana wote wanaomaliza Kidato cha Sita waende JKT. Tunataka uongeze idadi ya vijana walioko mitaani waende JKT, kwa sababu JKT kwanza ina majukumu, *objectives* zake iliyopewa. *Objective* ya JKT namba moja ni malezi kwa vijana wetu, *objective* nyingine ni kuzalisha mali, kuwafundisha vijana wetu kuondokana na *mentality* ya kufikiria kwamba kazi za ofisini ni bora kuliko kujiajiri, kuzalisha mali lakini ni ulinzi wa Taifa letu. Kutoa mafunzo ya uhakika kwa vijana wetu kuhakikisha kwamba wanakuwa wazalendo, wakakamavu, kuendelea kulinda Taifa letu. Malezi ya vijana, kuwa na vijana wenye nidhamu, wakakamavu, wenye kujitegemea, wenye uwezo wa kufanya kazi ili kuleta maendeleo kwenye nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kumbe ni wakati muafaka sasa kama alivyosema kaka yangu Mheshimiwa Kingu, kumbe Wizara nyingine hizi zilitakiwa zifanye *coordination* na JWTZ na JKT kupeleka programu zao waseme sisi tunayo programu ya kuwafundisha vijana kupitia *BBT* hawa hapa. Kwa sababu Mheshimiwa Waziri kinachosumbua sasa hivi kwa vijana wetu, shule tumejenga nyingi, vyuo vingi ujuzi wanao, kinachosumbua ni ukakamavu, ni nidhamu na kujitegemea, hivi watavipata kule! Tunao Maafisa Kilimo *yes*, tumewadahili kwenye vyuo vya kilimo lakini Afisa Kilimo anaogopa nyoka, na nyoka wanaishi mashambani, akapate ukakamavu jeshini. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, tuna vijana tumewafundisha sasa hivi tumewapelea *BBT* watajifunza vizuri na mimi nashukuru nimetembelea kituo kimoja wanafanya vizuri lakini akishika jembe, akinyanyua tu jembe analiangusha lina mkata, ukakamavu haupo. Tunao vijana wengi tunawafundisha au tunawadahili wanakwenda vyuo vikuu wanamaliza *form six*, wanakuwa wasomi wazuri, madaktari wazuri lakini uzalendo hakuna. Mtu anaona bora mgonjwa afe yeye akimbie na dripu akauze. Kwa hiyo, kumbe mwarobaini wetu ni JKT na wazazi wetu waliliona hilo na ndio maana nikawa najiuliza ni kwa nini Waziri Mkuu Hayati Rashidi Kawawa aliamua kwenda JKT, ni kwa nini Mzee Aboud Jumbe aliamua kwenda JKT, ni kwa nini Mzee wangu mimi Adam Sapi, Spika wa kwanza wa Bunge hili aliamua kwenda JKT. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kule ndiko alikopata uzalendo na ukakamavu, wakajifunza nidhamu, leo tuna vijana tumewaendeleza sayansi na teknolojia Mheshimiwa Nape alikua anazindua minara 700 tunaweka huko lakini wengine wanatumia tu kutukanana au kutukana viongozi wetu au kui - *defend* Serikali yetu. Tusipowapeleka hawa JKT kujifunza uzalendo haina maana uwekezaji tuliofanya.

Mheshimiwa Spika, Serikali lazima mkae kama kitu kimoja mkubaline kwamba chombo kilichopitishwa kisheria na Bunge Tukufu kwa ajili ya malezi rasmi ya vijana wetu ni JKT, hatuhitaji tu akili

za darasani *Intelligent Quotient*, ukishamjengea *mental structure* tunahitaji *physical structure* yake kwenye *performance*. Ana akili nzuri ni Afisa Kilimo mzuri lakini kuna mahali atatakiwa a -*demonstrate* ashike jembe achimbe, amuoneshe mkulima namna ya kufanya lazima huyu awe mtu makini, awe mtu mkakamavu, awe mtu mzalendo, awe ni mtu mwenye nidhamu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, JKT lazima iwezeshwe Waheshimiwa Wabunge, hiki ndiyo chombo kinachotuunganisha vijana wetu kama Taifa pekee yake. Huku kwingine tukiungana tunaungana kama Vyama vya Siasa, tunaungana kama CCM, tuna *green brigade* wetu, wanaungana kama CHADEMA wana *red brigade*. Huku ndiko tunakounganishwa kama Watanzania, tunaongea maslahi ya Watanzania, huku ndiko tunapelekwa bila ukabila, huku ndiko tunakopelekwa bila kujali itikadi za imani zetu. Tunakwenda kuambiwa sisi ni Watanzania *we are blessed to be Tanzanians*, tunaijenga Tanzania. Vijana wetu lazima wakue na *mentality* hiyo, wasifikirie tu kuona kwamba nchi zingine wanafanya vizuri, wanaishi vizuri natamani kutorekea huku, natamani kutorekea huku. Haina maana nchi hii, humu humu ndiyo nchi ya asali na maziwa hapa hapa.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri nikuombe sana JKT, halafu kulala kule JKT namshukuru Mungu alinipa *privilege* nikaenda. Majengo ya JKT wala hayahitaji gharama kubwa wala *is not a mansion* kama hili Bunge letu. Wao wanapiga tu yale mahanga, bati na nini na nini, Waziri utuambie ukija hapa, CCM imekuelekeza hapa, wewe unajenga kambi ngapi? Vijana wengi tunataka kuona wanapungua mitaani unaniambia…

**SPIKA:** Kengele ya pili imeshagonga Mheshimiwa.

**MHE. JESCA J. MSAMBATAVANGU:** Ninataka kuona unanimbia Mheshimiwa Jesca leta vijana toka Iringa tuwapeleke JKT, wakajifunze uzalishaji mali, uzalendo na jinsi ya kulitumikia Taifa na kujitegemea wao wenyewe.*(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Jesca Msambatavangu kengele ya pili imeshagonga.

**MHE. JESCA J. MSAMBATAVANGU:** Mheshimiwa Spika, ahsante, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Waheshimiwa Wabunge sikutaka kumkatiza Mheshimiwa Jesca Msambatavangu wakati akichangia. Ukiwa unachangia unamwambia Waziri anashindwa hata kuandika jambo ama kama amewaza jambo kwa sababu una mtazama yeye na yeye inabidi akusikilize wewe kwa kukutazama. Maana ukimwona anaandika utaona ama anamuuliza wa jirani kwamba hivi hapa ni vipi utaona kama hasikilizi mchango wako, ndiyo maana kwa Kanuni zetu wewe unazungumza na Spika, yeye anakuwa anasikiliza. Ukiwa unaongea naye yeye moja kwa moja anashindwa kukutayarishia majibu ya hoja zako. Maana kila saa anakuangalia wewe, kwa hiyo haandiki sasa, maana ukishamwita Waziri anasikiliza, Waziri anasikiliza. Mimi ndiyo kazi yangu kukusikiliza Waziri muache afanye ya kwake atakuja kuwajibu hapa. *(Makofi)*

## MICHANGO KWA MAANDISHI

**MHE. JUMA OTHMAN HIJA:** Mheshimiwa Spika, napenda kukushukuru wewe kwa kunipatia nafasi hii ya kutoa mchango wangu katika hotuba hii ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kwa mwaka wa fedha 2023/2024. Hii ni Wizara muhimu katika nchi yenye dhamana ya utulivu, amani na usalama.

Pili, napenda kumpongeza Rais wetu Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan kwa namna anavyoongoza nchi yetu kwa umakini mkubwa sana na namuombea kila la kheri katika uongozi wake huu.

Mheshimiwa Spika, napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Wizara hii pamoja na watendaji wake wote kwa namna walivyotayarisha hotuba hii kwa ubora wa hali ya juu na hatimaye

kuiwasilisha hotuba hii katika Bunge lako tukufu kwa ufasaha na umakini mkubwa sana.

Mheshimiwa Spika, mimi katika kuchangia hotuba hii napenda kuchukua nafasi ya kuipongeza Wizara hii kwa kutekeleza kazi zake kwa utararibu mzuri. Wizara inaendelea kuimarisha amani na utulivu katika nchi yetu. Wananchi tunaishi kwa usalama, wananchi wanafanya mambo yao ya kujiletea maendeleo bila ya wasiwasi wala bughudha yoyote.

Mheshimiwa Spika, Wizara hii ni kiungo kikubwa kati ya nchi yetu na nchi jirani. Kazi hii kwa mtazamo wangu wanaifanya vizuri sana, wanaimarisha mipaka ya nchi yetu na nchi jirani. Nawaomba waendelee na kufanya kazi zao kwa mujibu wa utaratibu na sheria za nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, mimi leo mchango wangu ni kuipongeza tu Wizara hii kwa utendaji wake mzuri.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. MAIMUNA A. PATHAN:** Mheshimiwa Spika, naomba kuchukua nafasi hii kumshukuru Mungu kwa kunipa pumzi ya uhai, pia nachukua nafasi hii kumpongeza Rais wetu Mama Samia Suluhu Hassan kwa kazi zake anazozifanya kwa kasi Sana kwa kipindi kifupi, aidha nikupongeze wewe kwa kuendesha Bunge letu kwa weledi mkubwa pasipo kupindapinda.

Mheshimiwa Spika, naomba kupongeza pia juhudi za Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa pamoja na Jenerali Jacob John Mkunda, pia nampongeza Luteni Jenerali Salum Haji Othman kwa kupandishwa cheo na kuteuliwa kuwa Mnadhimu Mkuu wa Jeshi letu.

Mheshimiwa Spika, nina ombi kwa Serikali yetu Sikivu, kuna maeneo katika Wilaya ya Nachingwea ambayo baada ya ku-*review* mipaka ya Kikosi cha Jeshi Majimaji yalichukua maeneo

ambayo yalikuwa yanamilikiwa na wananchi wa Nampemba kwa miaka yote tangu enzi za mababu na mababu.

Mheshimiwa Spika, maeneo yale wazee wetu wengi wameweka mashamba ya mikorosho ambayo yanawapatia riziki kwa miaka yote. Ombi langu kwa Serikali kwa kuwa wameyachukua yale maeneo na watu wameyahudumia na kuwa tegemeo la maisha yao, naomba sana wale watu wafikiriwe wapewe hata kifuta jasho kwa kuwa maeneo hayo yalikuwa ni tegemeo kwa maisha yao.

Mheshimiwa Spika, ombi lingine ni kwa wananchi wanaozunguka maeneo ya JKT Nachingwea; maeneo kama ya Mapochelo, Mkukwe na mengineyo nao pia wameathirika sana baada ya kupanua na ku-*review* maeneo ya Jeshi la Kujenga Taifa (JKT) Nachingwea niombe sana Serikali yetu ijitahidi kuwapa kifuta jasho wananchi wale.

Mheshimiwa Spika, wananchi wale yale maeneo yalikuwa ni tegemeo lao katika kuendesha maisha yao, niombe sana wananchi hawa wa maeneo haya ambayo nimeyataja wapewe kifuta jasho ili waweze kwenda kutafuta maeneo mengine ya mashamba kwa ajili ya kuendeleza maisha yao.

Mheshimiwa Spika, najua Serikali yetu ni sikivu ijitahidi kuwasaidia wananchi wale wako kwenye hali mbaya sana.

Mheshimiwa Spika, ombi langu lingine ninaomba Kikosi cha Jeshi *Farm Seventeen* kilitunza viongozi wengi sana waliokuwa wanapigania uhuru nchi za Kusini mwa Bara la Afrika, niombe Serikali yetu ikumbuke maeneo yale kufanya matengenezo na marekebisho kwa kuwa yamekuwa machakavu sana.

Mheshimiwa Spika, ahsante na naunga mkono hoja.

**SPIKA:** Mheshimiwa Spika, Maimuna Pathan atafuatiwa na Mheshimiwa Patrobass Katambi, mtoa hoja ajiandae.

Mheshimiwa Pathan hayupo? Mheshimiwa Patrobass Katambi atafuatiwa na mtoa hoja.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU (MHE. PASCAL P. KATAMBI):** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa nafasi hii. Ninashukuru sana nami niungane na wenzangu kuwapongeza sana Wizara ya Ulinzi lakini pia nimshukuru na kumpongeza sana Amiri Jeshi Mkuu Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa kuiongoza Nchi yetu vizuri na mpaka sasa tunaona amani na salama tunayo na tunaendelea kujenga uchumi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninakushukuru pia wewe kwa kunipa nafasi hii zaidi nichangie tu kidogo kwenye eneo moja, Kwanza niwape *confidence* ya Serikali kwenye eneo hili, imezungumzwa na Waheshimiwa Wabunge vizuri sana hapa kuhusiana na hoja mbalimbali wote ni nia njema ya kutaka kuboresha vyombo vyetu hivi vya ulinzi na usalama na hasa Jeshi letu hili.

Mheshimiwa Spika, Vyombo vya Ulinzi na Usalama vinatambulika kwenye Katiba kwa mujibu wa Ibara ya 147 (1) na (2) lakini pia ni jambo ambalo liko kwenye orodha ya Muungano katika orodha namba tatu na sambamba na hilo vyombo hivi vya ulinzi na usalama Amiri wake Mkuu kwa mujibu wa Ibara ya 148 ya Katiba ni Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na si mwingine ni Dkt. Samia Suluhu Hassan. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunatambua Serikali upande wa umuhimu kubwa wa Jeshi hili la kwetu hapa la ulinzi na usalama, kwa kutambua umuhimu huo kwa sababu jeshi hili limefanya kazi kubwa ya kulinda mipaka ndani na nje ya nchi lakini pia kulinda viongozi wetu, kulinda uchumi wetu ili isitokee wakati wowote hali ambayo itapelekea kupoteza usalama wa Nchi na hivyo kurudi nyuma katika uchumi na hata kupoteza maisha au usalama wa watu wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika suala hilo niweze kueleza tu kwenye maeneo ambayo yamezungumzwa na Waheshimiwa Wabunge. Kwanza limezungumzwa hapa suala la kuhusiana na kodi. Niwape tu uhakika na kuwathibitishia Waheshimiwa Wabunge kwamba michango yote ambayo wameizungumza hasa kwenye maeneo ya kodi kwenye vifaa vya Jeshi lakini pia maslahi megine ya vyombo vyetu hivi vya ulinzi na usalama si yote ambayo tunaweza tukayazungumza hadharani hapa, kwa sababu Bunge lako Tukufu hili linaenda *public,* lakini kuna mambo niwahakikishie na kuwapa *confidence* Waheshimiwa Wabunge kwamba kama Serikali tumeyachukua tunaheshimu sana na kupokea mchango wao kwa moyo mkunjufu ili tuweze kufikisha na viongozi hawa Mheshimiwa Waziri mwenye dhamana husika atakutana na Waziri wa Fedha lakini pia wataongozwa na viongozi na timu nzima, kwa ajili ya kuyaangalia pia masuala haya ya kikodi yamekaaje na kuweza kuyaweka sawa sawa ili kuimarisha Jeshi letu ambalo lina heshima kubwa sana ndani na nje ya Nchi.

Mheshimiwa Spika, mnakumbuka kwenye *peace keeping mission* mara nyingi Tanzania tumekuwa tukipata *record* nzuri sana ya kufanya vizuri katika kazi za Kimataifa ambazo zimekuwa zikitokea katika Ukanda wa Afrika hata katika ngazi ya Kimataifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia tunatambua kwenye eneo lingine la masuala ya wastaafu ambao ni Wanajeshi, wanapopumzika sasa tunatambua wanakuwa wamechangia na wamefanya kazi kwa kweli kubwa kwa kuweka mchango wao kwa masuala ya kiusalama lakini pia ujenzi wa Taifa katika suala la uchumi. Mimi pia katika eneo hili nieleze na kuwaambia Waheshimiwa Wabunge kwa sababu Mawaziri wenye dhamana husika hapa pengine hawapo lakini kwa hatua hii kwa sababu sisi tuko hapa kuwakilisha hili, tunalichukua nalo na tutaenda kufanya kazi ya kufanya mapitio upya ya wastaafu wetu wa vyombo vya ulinzi na usalama ambao bado wana changamoto za kuhusiana na kupata mafao yao au kupewa stahiki zao ili kuweza kuhakikisha kwamba basi tunaona na

kuheshimu mchango wao katika kipindi chote ambacho wamefanya kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini pia katika maeneo mengine ambayo yamechangiwa na Waheshimiwa Wabunge kuhusiana na suala la fursa za ajira kwa ajili ya vijana wetu na namna ya kuweza kuunganisha na kutengeneza *teamwork* pamoja na Jeshi hili kwa maana ya Wizara ya Ulinzi. Hili nalo tunalichukua kwa ajili ya kulifanyia kazi na hivi yote ni kwa sababu ya maslahi mapana ya Taifa letu lakini nizidi kuhakikishia Watanzania wote wanaonisikiliza lakini pia Bunge lako Tukufu. Sisi Serikali tuko imara tukiongozwa na Dkt. Samia Suluhu Hassan ambaye ndiye Amiri Jeshi Mkuu katika vyombo vya ulinzi na usalama wakati wote, tutasikiliza kwa unyenyekevu na tutaenda kutoa huduma inayostahiki kwa mujibu wa mambo yale ambayo yatakuwa yamepangwa ili kuweza kuhakikisha mipango na mikakati inawekwa sawa sawa ili kuweza kuhakikisha Taifa letu linakuwa salama pia tunaendelea kuulinda uchumi wetu wa Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hatutakuwa na uchumi wala hatutakuwa na shughuli kama usalama utakuwa hatarini, kwa hiyo usalama ni kipaumbele namba moja cha Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, ahsante kwa muda wako, naomba kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Waheshimiwa Wabunge sasa nimuite Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, Mheshimiwa Innocent Bashungwa aje ahitimishe hoja yake. *(Makofi)*

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ili niweze kuhitimisha hotuba yangu. Kabla sijaendelea nianze kwa kukushukuru wewe kwa kuliongoza Bunge letu kwa weledi mkubwa. Nafahamu umekuwa kiongozi bora wa Bunge letu la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa vile pia kule Mbeya Mjini wananchi wanakupa ushirikiano. Natumia nafasi hii kuwashukuru Wanambeya Mjini na

kuendelea kuwaomba waendelee kukupa ushirikiano, Taifa linakutegemea. Kwa kweli tunakushukuru sana kwa uongozi wako mahiri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia naishukuru sana Kamati ya NUU inayoongozwa na Mheshimiwa Vita Kawawa, Makamu Mwenyekiti Vincent Mbogo pamoja na Wanakamati. Tunawashukuru sana kwa namna ambavyo mnaendelea kutuelekeza na kutushauri ili Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa iendelee kuwa ni Wizara ambayo inamsaidia vyema Mheshimiwa Rais na Amiri Jeshi Mkuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia nawashukuru sana Waheshimiwa Wabunge ambao mmechangia katika kikao hiki. Tunawashukuru sana kwa ushauri wenu ulikuwa *very constructive*. Tunawashukuru kwa madini ambayo mmetupatia, yanaenda kutuimarisha kama Wizara ili tukajipange vizuri kuendelea kuhakikisha tunamsaidia Mheshimiwa Rais na Amiri Jeshi Mkuu, kuendelea kuyasaidia majeshi yetu, kuendelea kujenga ustawi na kujiimarisha.

Mheshimiwa Spika, kama Dada yangu Mheshimiwa Jesca alivyosema, pia Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa ni sehemu ya kutekeleza Ilani ya Chama cha Mapinduzi kama alivyoinukuu. Kwa hiyo, nawashukuru Waheshimiwa Wabunge kwa ushauri na maoni ambao ametupa. Nawashukuru hata wale ambao hawajapata nafasi ya kuchangia kwa sababu ushiriki wao na *support* yao kama tulivyo hapa ni sehemu ya mchango. Kwa hiyo, nawashukuru sana Waheshimiwa Wabunge wote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niendelee kumshukuru Mheshimiwa Rais na Amiri Jeshi Mkuu, mpendwa wetu, Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa kweli anafanya kila aina ya jitihada kuhakikisha majeshi yetu na vyombo vya ulinzi na usalama vinaendelea kutimiza wajibu wake. Yapo mambo makubwa ambayo Mheshimiwa Rais anawezesha vyombo vya ulinzi na usalama, lakini kama mnavyojua, yapo ambayo tunaweza tukayaweka wazi na yapo ambayo yanaendelea kuwa *classified,* lakini Mheshimiwa Rais na Amiri Jeshi

Mkuu anafanya kazi kubwa sana ya kuviwezesha vyombo vyetu vya ulinzi na usalama. Tunamshukuru.

Mheshimiwa Spika, vile vile tunamshukuru Mheshimiwa Rais, kwenye dira yake ya kuwezesha kukua kwa diplomasia ya kiuchumi. Kama mnavyofahamu, Diplomasia ya Kiuchumi inapofanikiwa hata Diplomasia ya Ulinzi inafanikiwa. Kwa hiyo, nasi upande wa Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa tunaendelea kumshukuru Mheshimiwa Rais kupitia Diplomasia ya Kiuchumi pia ametusaidia kuimarisha Diplomasia ya Ulinzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wakati nchi yetu ina amani ambayo tunaipata kwa gharama kubwa ya wanajeshi na vyombo vyetu vya ulinzi na usalama kuendelea kushirikiana wakiwezeshwa na Mheshimiwa Rais na Amiri Jeshi Mkuu, wakati wa amani ndiyo wakati wa kujenga uchumi wa Taifa letu. Kwa hiyo, tuendelee kumpa ushirikiano Mheshimiwa Rais na Amiri Jeshi Mkuu, Waheshimiwa Wabunge wenzangu pamoja na Watanzania ambao mnanisikiliza. Mheshimiwa Rais ametengeneza mazingira wezeshi ya kuzalisha, kuendesha shughuli za kiuchumi, sasa tushikamane naye bega kwa bega kuhakikisha tunaendelea kujenga nchi yetu, kujenga uchumi na kuhakikisha kwa kweli Mheshimiwa Rais tuna kila sababu ya kumuunga mkono kwa asilimia mia moja ili azidi kutenda maajabu.

Mheshimiwa Spika na Waheshimiwa Wabunge, mnaona kwa namna ambavyo tunapata miradi ya maendeleo kwenye majimbo yetu. Tutembee kifua mbele tuwe na Mheshimiwa Rais wetu Dkt. Samia Suluhu Hassan, tumpe moyo, tushikamane naye bega kwa bega. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa niende kwenye kujibu hoja ambazo zimejitokeza kwenye mijadala, na kwa sababu ya muda sitaenda hoja baada ya hoja, lakini niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge kila hoja tumeichukua, tunaenda kuifanyia kazi. Kamati ya NUU ni Kamati ambayo iko makini sana. Wana mfumo wa *monitoring and evaluation.* Hoja ambazo zilijadiliwa hata kwenye miaka ya fedha iliyopita, wana utaratibu wa kusema hii bado, hii tayari, hii hebu

tueleze. Kwa hiyo, niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge kupitia Kamati ya NUU tutaendelea kufanyia kazi haya ambayo mmechangia na kutuelekeza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nianze na suala la ajira JKT. Huku jeshini tunakuita kujiandikisha, siyo ajira, lakini kwa sababu ya kuelezea tulichukulie hivyo hivyo "ajira", lakini huku tunajiandikisha kwa sababu mwanajeshi anajiandikisha kwa sababu ya kuwa tayari kutumikia Taifa lake na mahali popote na kwa gharama yoyote ikiwemo maisha yake. Kwa hiyo, tunaendelea kuwashukuru sana askari wetu pamoja na maafisa kwa kujitoa kwa ajili ya Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika ajira za JKT nimefanya uchambuzi, 45% ya vijana ambao wanajiunga na JKT ndio wanapata fursa ya kuajiriwa na vyombo vya ulinzi na usalama. 55% kwa sababu vyombo vya ulinzi na usalama nafasi ni chache, ndiyo hiyo JKT inawafundisha ujuzi wa ufundi stadi ili warudi wakajiajiri au kupitia mifumo mingine ya Serikali waweze kusaidiwa kujiajiri.

Mheshimiwa Spika, nikiri kwamba Waheshimiwa Wabunge kama walivyochangia, tunalo jukumu la kushirikiana kuhakikisha hii 55% ambayo inarudi mtaani, kwa kadiri inavyowezekana tunashirikiana kuipunguza. Hapa mmetupa mawazo tufanye nini ili kuweza kupunguza hii 55% ya vijana ambao wanahitimu kwa kujitolea JKT lakini wanarudi mtaani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nakubaliana na mawazo ya Bunge kwamba, kama nilivyosema kwenye hotuba yangu, sisi kupitia JKT tayari tumekaa na Wizara ya Kilimo, tayari tumekaa na Wizara ya Mifugo na Uvuvi na Waheshimiwa Marais wetu; Mheshimiwa Rais wetu Dkt. Samia Suluhu Hassan pamoja na Mheshimiwa Rais wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Mheshimiwa Dkt. Hussein Ally Mwinyi, kwenye mkakati wa kuhakikisha Uchumi wa Bluu unakuwa ni sehemu ya kuzalisha ajira na kujenga uchumi wa nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia kupitia Wizara ya Mifugo na Uvuvi tumekaa na tunaendelea kuchambua namna ambavyo tunaweza kushirikiana kama ile *MoU* ambayo tumeisaini na Wizara ya Kilimo vile vile tulisaini *MoU* na Wizara ya Mifugo na Uvuvi ili kutekeleza haya ambayo mmetushauri. Hivyo hivyo, hata kwenye Sekta ya Viwanda tutafanya hivyo. Pia mmetuboreshea zaidi kwamba tunahitaji kukaa hata na Ofisi ya Waziri Mkuu, Vijana tujadili na tuwe tuna mkakati wa pamoja ambao ikiwezekana tuulete mbele ya Kamati ambazo zinasimamia watupe ushauri halafu uwe ni mkakati wa pamoja wa kutekeleza Ilani ya Chama cha Mapinduzi kuzalisha ajira za vijana wengi. Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge, hili tumelichukua ngoja tukalifanyie kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusu suala la *exemption,* hili naizungumzia pamoja na *bonded warehouse*. Mheshimiwa Naibu Waziri wa Fedha yupo, tutakaa tuangalie namna bora ya kuweza kulifanyia kazi jambo hili. Ni jambo ambalo linahitaji uchambuzi na kuangalia *fiscal implications* na nini zikoje, hata Kamati imeshauri hivyo hivyo kwa sababu ni jambo zito. Nikiri hata kwenye upande wa majeshi yetu, tukiweza kulitekeleza bila kuathiri *fiscal projection* za Serikali, litaleta weledi na ufanisi mkubwa kwenye majeshi yetu. Kwa hiyo, hili tumelichukua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niwathibitishie na kuwahakikishia Waheshimiwa Wabunge, jukumu kubwa na la msingi la majeshi yetu ni kulinda Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Hata kwenye masuala ya ajira, *formula* ya 21 kwa 79 inazingatiwa kwa 100%. Kwa hiyo, ningependa kumtoa wasiwasi kaka yangu Mheshimiwa Ussi Pondeza, labda ni kwa sababu za kimawasiliano tu lakini majeshi yetu yanaheshimu Katiba yetu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Tutakaa pamoja na ndugu zetu upande wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kuhakikisha kwamba hili jambo hata kama kuna *miscommunication,* linakaa sawa. Ila niwathibitishie kwamba tunaheshimu na kusimamia Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia lilijitokeza suala la Shirika la Nyumbu, mmeelezea vizuri kwamba mashirika haya ukiangalia sababu za kuasisiwa kwake bado ni mashirika muhimu. Tumshukuru Mheshimiwa Rais na Amiri Jeshi Mkuu alituelekeza na tukaandaa mpango kazi wa miaka 10 ya Shirika la Nyumbu, lakini baada ya kufanya mapitio, tumeona tunaweza tukafanya vizuri zaidi. Kwa hiyo, tunafanya mapitio ya mkakati huu wa mpango wa miaka 10 ili Shirika la Nyumbu liweze kujikita kwenye mambo ambayo yataleta tija kama tulivyo-*discuss* hapa.

Mheshimiwa Spika, sambamba na mkakati huo, tayari Shirika la Nyumbu liko kwenye mjadala wa kutengeneza magari ya Zimamoto zaidi kusaidia Wizara ya Mambo ya Ndani. Tumetengeneza magari ya Zimamoto matatu, tuliyafanyia *testing,* yanafanya kazi nzuri. Hata Shirika la *SCANIA* lilipokuja Shirika la Nyumbu, kwa sababu tunatumia *engine* za *SCANIA,* ilibidi waje wafanye *accreditation, engine* isiingie kwenye *body* ambayo inaenda kufanya vitu ambavyo ni *substandard. SCANIA* walipofika Shirika la Nyumbu walishangaa, wakasema kama Shirika la Nyumbu linaweza likatengeneza magari ya Zimamoto yenye ubora wa kimataifa namna hii, kwa nini mnaendelea ku-*import? (Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, jambo hili hata Kamati ya NUU wameliona, tunaendelea kushirikiana kuangalia namna bora tutakavyoshirikiana na Wizara ya Mambo ya Ndani kufanya *import substitution* ya magari ya Zimamoto taratibu kwa kadiri ya uwezo wa uzalishaji ndani ya Shirika la Nyumbu utakavyoruhusu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vile vile hata Shirika la Mzinga tunasema mazao ya msingi, lakini tukija huku kwenye Kamati wanaelewa mazao ya msingi ni yapi? Tunaendelea kuangalia mashirika mengine kwenye nchi rafiki ambazo tunashirikiana nazo kwenye masuala ya kiulinzi kuliwezesha Shirika la Mzinga kuweza kuzalisha mazao ya msingi zaidi yanayozalishwa hivi sasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika na Waheshimiwa Wabunge, vile vile, tunaandaa sheria ambayo tutaileta Bungeni hapa ya *Defense*

*Industry*. Sheria ambayo itakuwa *facilitative* kwa mashirika yetu ya kiulinzi, sambamba na kuyajengea ustawi wa kufanya vizuri zaidi na kwa kuingia *partnership* na mashirika mengine ya kiulinzi kwenye nchi ambazo ni rafiki, tunashirikiana nazo kiulinzi. Pia sheria hii itaangalia namna ya ku-*facilitate* uwekezaji wa sekta binafsi katika sekta ya ulinzi. Ndiyo maana kwenye hotuba yangu nilisema, Wizara pamoja na kuandaa sheria hii, pia tumeanza kubainisha maeneo ambayo tutaweka *exclusive zone* kwa ajili ya uwekezaji wa sekta ya ulinzi sambamba na hii sheria ambayo tutaileta mbele ya Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Sera ya Ulinzi, nawaomba Waheshimiwa Wabunge, kwenye hili naomba mtupe muda ili tulifanyie uchambuzi zaidi. Ukiangalia historia ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, wakati nchi yetu inapata uhuru, Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa ilikuwa ni Wizara moja pamoja na Wizara ya Mambo ya Nje. Walikuwa wanatumia sera moja na kulikuwa kuna sababu za msingi. Kwa hiyo, ni vizuri tukafanya uchambuzi, tukashirikiana na Wizara ya Mambo ya Nje kuangalia wazee hawa walipokaa na kutengeneza hii sera ambayo ni pacha, inatoa *guidance* kwenye masuala ya kiulinzi kwa sababu tunapolinda mipaka ya nchi ni mipaka ya nchi yetu dhidi ya nchi jirani. Kwa hiyo, suala hili ni lazima liwe na mtazamo wa ndani kulinda mipaka, lakini pia liwe na sura ya mambo ya nje.

Mheshimiwa Spika, pamoja na Waheshimiwa Wabunge, kwa hiyo, jambo hili kwa msukumo wa Bunge hili kupitia Kamati ya NUU, ilitufanya twende *deep* zaidi kuangalia na tukagundua kwamba hili jambo inabidi twende taratibu tufanye uchambuzi na tushirikiane kwa kina na Wizara ya Mambo ya Nje ili tuweze kuwa na sera ambayo itaweza kukidhi yale ambayo tunatarajia sera iweze kusaidia Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa.

Mheshimiwa Spika, suala la ajira upande wa JKT nimeshalisema na kama tukifanya kama mlivyotushauri, itakuwa ni sehemu ya mkakati wa kutengeneza ajira milioni nane ambazo tumeziahidi kwenye Ilani ya Chama cha Mapinduzi.

Mheshimiwa Spika, vile vile katika michango ya Waheshimiwa Wabunge, mlisema nitakaposimama hapa nielezee tutajenga makambi mangapi ili kuwezesha vijana wanaomaliza *Form Six* kwa mujibu wa sheria kuweza kwenda JKT wote, lakini vile vile hata vijana ambao wanajitolea kuweza kupeleka idadi kubwa zaidi kuliko ilivyo sasa.

Mheshimiwa Spika na Waheshimiwa Wabunge, takwimu za JKT zinaonesha miundombinu ambayo tunayo kwa ajili ya kupokea vijana wanaomaliza *Form Six* bado tunapokea wachache kuliko miundombinu inavyoweza ku-*support*. Kwa hiyo, nawaomba Waheshimiwa Wabunge tuendelee kuhamasisha vijana ambao wanatakiwa kwenda JKT wanapomaliza *Form Six* kwa mujibu wa sheria watii matakwa ya kisheria hayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, takwimu zinaonesha tunapokea takribani 22,000 na wakati tuna uwezo wa kupokea 26,000. Kwa hiyo, kuna *gap* ya 4,000 lakini mtaani mtazamo ni tofauti. Upande wa vijana ambao ni kwa mujibu wa sheria, utakuta wanasema walitaka kwenda, lakini miundombinu haitoshi. Hii changamoto ya kutotosha kwa miundombinu ni kwa upande wa vijana ambao wanajitolea. Hilo nikiri changamoto ipo na tutakaa na Wizara ya Fedha na Mipango kuangalia namna ambavyo tunaweza tukasaidiwa ili kuweza kuongeza miundombinu kuweza ku-*accommodate* vijana wengi zaidi ambao wanajitolea waweze kupata fursa ya kupata mafunzo ya JKT. Kwa hiyo, hili tunalichukua ili tukalifanyie kazi.

Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema, mawazo yalikuwa ni *constructive*. Waheshimiwa Wabunge mmetupa ushauri mzuri, tumechukua yote na itoshe kusema kwamba tutaenda kuyafanyia kazi.

Mheshimiwa Spika, nimalizie kwa kuwashukuru sana Waheshimiwa Naibu Mawaziri kwa ushirikiano ambao wamenipa katika kuwasilisha hotuba hii. Vile vile nimhakikishie Mheshimiwa Mathayo, mtani wangu, tutaenda Musoma tuangalie maeneo haya

ambayo ameyataja na tushirikiane kama nilivyosema, lazima tuangalie pande zote mbili. Majeshi yetu yanahitaji maeneo ya kufanyia mazoezi na kujiandaa kivita. Kwa mtazamo wa macho ya kiraia, unaweza ukaona eneo la jeshi ni kubwa, lakini kwa mtazamo wa kitaaluma ya kijeshi ni eneo dogo na majeshi yetu hayawezi kwenda nchi ya nje eti waazime eneo kwa ajili ya kufanya mazoezi. Hiyo itakuwa siyo jeshi. Kwa hiyo, mazoezi lazima wafanyie humu humu ndani ya nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nawaomba Waheshimiwa Wabunge tuendelee kushirikiana, tutatue migogoro ya ardhi baina ya wananchi wetu na majeshi, lakini pia mtusaidie kutoa elimu kwa wananchi wetu, tuheshimu maeneo ya jeshi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia nimalizie. Kulikuwa na maombi maalum ya Waheshimiwa Wabunge wawili; Mheshimiwa Mathayo kwamba twende *site,* nitakuja.

Pia kaka yangu Mheshimiwa Rashid Abdalla Rashid, nitakuja Pemba tukaangalie maeneo ambayo umeyataja tutembelee ile skuli ambayo umesema tuitembelee. Nitumie nafasi hii kuwapongeza vijana kwa kazi nzuri wanayoifanya ya ku-*perform* vizuri na kupata heshima ya *performance* nzuri ya skuli hii. Basi nitakapokuja tutaangalia hizo changamoto za migogoro uliyoitaja ili tutafute namna bora ya kutatua changamoto hizo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, nakushukuru tena kwa kunipa nafasi.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WANAWAKE NA MAKUNDI MAALUM:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, hoja imeungwa mkono. Ahsante sana. Katibu.

**NDG. RUTH MAKUNGU – KATIBU MEZANI:** Kamati ya Matumizi.

**SPIKA:** Kamati ya Matumizi.

## KAMATI YA MATUMIZI

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa tukae, Katibu.

**NDG. RUTH MAKUNGU – KATIBU MEZANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ya Matumizi inaanza na Kitabu cha Pili Fungu 57 Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa. Katika kitabu ni ukurasa wa 503 na katika Kishikwambi ni ukarasa wa 502.

## KITABU CHA PILI

## MATUMIZI YA KAWAIDA

### Fungu 57 - Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa

Kifungu 1001 - *Administration and Human Resources Management*.......................................Sh. 20,450,513,400

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, kifungu hiki kina mshahara wa Waziri kuna Mheshimiwa Mbunge anataka ufafanuzi juu ya jambo mahususi la kisera, Mheshimiwa Sophia Mwakagenda.

**MHE. SOPHIA H. MWAKAGENDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante mimi nataka ufafanuzi kutoka Waziri. Ninatambua kabisa Mwanajeshi yoyote ni lazima apitie *course* na mafunzo ili aweze kufanya vizuri. Sasa kumekuwa kuna shida kidogo wanapokwenda *course* wanakatwa fedha hadi wanakosa wakati mwingine fedha

za chakula, ni takriban 300,000 na vitu kama hivyo. Tunafahamu wao ni muhimu sana waende *course* ili waweze kupanda cheo. Sasa ninaomba tu ufafanuzi wako, tunajua kwamba kama watakuwa wanakatwa na jeshi, kwa sababu umesema inakosa fedha, hawapewi fedha za maendeleo labda inaweza ikawa sababu. Lakini nataka kujua kabisa unaji-*commit* vipi kuwasimamia kwamba angalau waweze kulipiwa wanapokwenda *course* na iweze kuwasaidia kuendelea na *course* zingine na wengine na wengine? Ninaomba ufafanuzi niweze kufahamu.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Sophia sisi ndio tumeisoma hii bajeti na Bunge limepelekewa kwenye Kamati na Kamati imekubaliana na Serikali inachosema. Kwenye ngazi hii tukitaka Waziri atoe ufafanuzi sisi ndio Bunge hapa ndio tufanye maamuzi kwamba pesa hizi hazitoshi ziongezwe na hapo tungeongozwa na kamati yetu kwamba wamefikia mahali walipoona hizi pesa kwa kweli na mafunzo ya wanajeshi hazitoshelezi. Sasa tukisema Waziri afanye *commitment* kwenye pesa ambazo hazimo humu kwenye vitabu sisi ndio tuseme. Sasa tuongozwe hapo na Kamati yetu, maana Kamati ndiyo inatuongoza na mawazo yake haya. Kamati yetu imesemaje Mheshimiwa Sophia kwenye hoja hiyo?

**MHE. SOPHIA H. MWAKAGENDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nilitaka mahususi kwenye suala la elimu. Kwa sababu natambua tunawekeza. Ili Jeshi letu liende kisasa ni lazima waende kwenye *course* na kujifunza. Kwa hiyo ninataka maelezo mahususi kwenye masuala ya kujielimisha.

**MWENYEKITI:** Ehe sasa kwenye kujielimisha, unajua umetoa maelezo marefu na mimi nilikuwa nakusikiliza. Umetoa maelezo ya kujielimisha ungekuwa umeishia hapo tungataka Waziri atueleze Serikali ina mpango gani kuhusu kuwapeleka kusoma ama kwenye *course* hao wanajeshi, lakini umesema kuna suala la utoshelevu wa fedha, nimekusikia sawa sawa au hapana; maana umeelezea hoja yako kwa kuioanisha na utoshelevu wa fedha hapo ndio napopata shida.

**MHE. SOPHIA H. MWAKAGENDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tunarudisha kwenye Kamati ninaamini wametusikia na watalifanyia kazi, nimeondoa hoja yangu.

**MWENYEKITI:** Haya ahsante sana, kwa hiyo jamani kuna kazi ambazo ni za kwetu sisi tuzifanye sisi. Tukishasema kwamba hapo fedha haitoshi Kamati yetu ilete taarifa hapa. Kwamba fungu hili limetengewa fedha hazitoshi sisi ndio tusimame hapa Waziri wa Fedha asimame aseme ili sisi tuipeleke kwenye Kamati ya Bajeti ikaongeze huko fedha. Sasa suala la pesa kwa kweli kwa ngazi hii ni la kwetu sisi. Nadhani hapo tutakuwa tumeelewana vizuri. Mheshimiwa Waziri baada ya ufafanuzi sasa alioutoa baadaye nadhani umeelewa. Kwa hiyo hoja ya msingi ni ile ya mafunzo kwa ajili ya wanajeshi, kwamba Serikali iwe na mpango fulani, yaani humu tukiwa tunasoma humu tuone fedha zinaongezeka; na ninyi ni lazima muwe mmeomba ili Bunge liweze kufanya maamuzi pamoja na kwamba kuna hayo masharti huwa mnapewa, lakini tujulisheni sisi ili sasa tuweze kufanya kazi yetu vizuri, ahsante sana.

Waheshimiwa Wabunge, tunaenda kwenye mafungu, Katibu.

**NDG. RUTH MAKUNGU – KATIBU MEZANI:**

**Fungu 57 – Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa**

Kifungu 1001 – *Administration and Human Resources Management Division*.......................Sh. 20,450,513,400
Kifungu 1002 – *Finance and Accounts Unit*……………........Sh. 320,000,000
Kifungu 1003 – *Policy and Planning Division*…................Sh. 843,240,000
Kifungu 1004 – *Internal Audit Unit*…….............................Sh. 331,577,000
Kifungu 1005 – *Procurement Management Unit*.............Sh. 279,040,000
Kifungu 1006 – *Legal Service Division*……........................Sh. 263,757,200
Kifungu 1007 –*Government Communication Unit*..........Sh. 218,400,000
Kifungu 1009 – *Information and Communication Technology Unit*......................................Sh. 450,200,000
Kifungu 2001– *Industries, Construction and Agriculture Division*…………………......Sh. 419,380,000

Kifungu 2002 – *Military Research and Development Division*……….......................................Sh. 980,021,400
Kifungu 2004 – *Estate Management and Building Consulting Division*………….....……….…Sh. 441,510,000

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)*

**Fungu 39- Jeshi la Kujenga Taifa**

Kifungu 1001 – *The National Service Force*..............Sh. 468,397,562,000

*(Kifungu kilichlotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)*

**Fungu 38- Ngome**

Kifungu 1001 – *National Defence Headquarter (NDHQ)*……….........Sh. 2,258,132,201,051
Kifungu 1006 – *Defence Forces Headquarter Command (DFHQC)*………...........…Sh. 2,605,375,200
Kifungu 1007 – *Land Forces Command (LFC)*………...Sh. 3,901,543,000
Kifungu 1008 – *Air Forces Command (AFC)*…………....Sh. 3,636,107,050
Kifungu 1009 – *Navy Command (NC)*……….…............Sh. 2,145,232,600
Kifungu 1010 – *Military Hospitals (MH)* ……….…............Sh. 3,318,291,100

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)*

**KITABU CHA NNE**

**MIPANGO YA MAENDELEO**

**Fungu 57 – Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa**

Kifungu 1003 – *Policy and Planning Division*….................Sh. 400,000,000

Kifungu 1009 – *Information and Communication Technology Unit*...……………..........................………Sh. 2,000,000,000
Kifungu 2001– *Industries, Construction and Agriculture Division*………………..........................……Sh. 11,800,000,000
Kifungu 2002 – *Military Research and Development Division*……...........................…...........Sh. 131,948,780,312
Kifungu 2004 – *Estate Management and Building Consulting Division*……...…..........................……Sh. 13,851,219,688

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)*

**Fungu 39 – Jesh la Kujenga Taifa**

Kifungu 1001 – *The National Service Force*................ Sh. 13,965,535,000

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)*

**Fungu 38 – Ngome**

Kifungu 1001 – *National Defence Headquarter (NDHQ)*….....................…..Sh. 48,867,636,000
Kifungu 1008 – *Air Forces Command (AFC)*......................................Sh. 0

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)*

**NDG. RUTH MAKUNGU – KATIBU MEZANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ya Matumizi imemaliza kazi yake.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, Bunge linarejea.

*(Bunge Lilirejea)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tuketi. Mtoa hoja, taarifa. *(Makofi)*

**T A A R I F A**

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:** Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la Februari 2020 Kanuni ya 123(3)(a) na (b) naomba kutoa taarifa kwamba Bunge lilikaa kama Kamati ya Matumizi, limekamilisha kazi yake; naomba Taarifa ya Kamati ya Matumizi ikubaliwe na Bunge.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WANAWAKE NA MAKUNDI MAALUM:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, hoja imeungwa mkono na sasa nitawahoji. Waheshimiwa Wabunge wanaoafiki Hoja ya Mheshimiwa Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024 waseme ndio, wasioafiki waseme sio, wote wameafiki. *(Makofi)*

*(Hoja Ilitolewa lamulie)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tumefika mwisho wa kuitazama Bajeti ya Wizara hii na hivyo baada ya kuwahoji na Bunge zima kusema ndio. Kwa hoja hii ya Mheshimiwa Waziri nitumie sasa fursa hii kutangaza rasmi kwamba Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024 yamepitishwa rasmi na Bunge. *(Makofi)*

*(Bajeti ya Serikali kwa Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024 Yalipitishwa na Bunge)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, hivyo nitumie pia fursa hii kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri, Katibu Mkuu na Watendaji wote chini ya Wizara hii ikiwa ni pamoja na majeshi yetu ambayo yako chini ya Wizara hii, tunawapongeza sana sana kwa kazi nzuri mnayoifanya. Pia tunawatakiwa kila la heri katika utekelezaji wa

yale ambayo mmeyasema kwenye hotuba yenu na hata yale ambayo hamjatuambia, tunawatakia kila la kheri katika utekelezaji wa hayo yote. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, mimi niishukuru sana Kamati yetu ya Mambo ya Nje ya Ulinzi na Usalama kwa kazi nzuri wanayoifanya kwa ushirikiano wanaoutoa, Mwenyekiti, Makamu Mwenyekiti na Wajumbe wote wanafanya kazi nzuri sana hatujasikia changamoto ya mambo ya hapa na pale, maana hii Kamati ni ya muhimu sana. Kwa hiyo tunawashukuru sana wawakilishi wetu kwenye Kamati hii mnafanya kazi nzuri.

Waheshimiwa Wabunge, ambao mmepata nafasi ya kuchangia na hata wale ambao hamjapata nafasi ya kuchangia Mheshimiwa Waziri yupo mnaweza kupeleka mawazo yenu atayasikiliza na watayafanyia kazi. Kwa hiyo na ninyi wote kwa pamoja tunawashukuru sana lakini mmetoa pongezi nyingi na mimi niungane nanyi Waheshimiwa Wabunge. Mmetoa pongezi nyingi kwa Mheshimiwa Rais na pongezi zenu hizo zimeungwa mkono kwa dhati kabisa na Mheshimiwa Waziri namna ambavyo Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. Samia Suluhu Hassan anaweka mkazo yeye kama Amiri Jeshi Mkuu wa Majeshi yetu ya Ulinzi, namna ambavyo anaweka mkazo kwenye Wizara hii na pia kuipatia pesa ambazo zinatosheleza yale mahitaji yao.

Waheshimiwa Wabunge, haya ambayo kuna hapa na pale basi Waheshimiwa Wabunge tuelewe kwamba yale ambayo hayajafikiwa asilimia 100, lakini yale ambayo yanatuhitaji kabisa sisi kuwa salama msiwe na wasiwasi Mheshimiwa Rais anafanya kazi yake vizuri kama kiongozi mkuu wa mambo haya yote.

Mheshimiwa Waziri na mimi niungane na Waheshimiwa Wabunge kukupongeza wewe kipekee kwa utulivu na kwa kweli kwa kufanya kazi nzuri, tunakutakia kila la heri. Sasa kwa majeshi yetu yote yanafanya kazi nzuri lakini bajeti ambayo iko chini ya Wizara yako ni JKT pia na Jeshi la Wananchi wa Tanzania, viongozi hawa ambao wanatuongoza huko tunawashukuru sana. Wote hao

pengine tukimtaja Jenerali Mkunda anafanya kazi nzuri na tunamtakia kila la heri katika utekelezaji wa majukumu yake. Na kwa kweli tumefurahi leo kuwaona wastaafu inaonesha namna ambayo yeye anawasikiliza hao wastaafu wakiwa na mawazo hapa na pale hata ambayo wao pengine wangetamani kuyatekeleza wakati wa kipindi chao hawakuweza maana yake wanapata nafasi ya kumwambia kuna hili, kuna lile.

Waheshimiwa Wabunge, pia wakiendelea kuwa karibu na jeshi hivi tunafurahi tunajua kwamba mambo yetu yako salama zaidi. Kwa hiyo tunampongeza sana, na kwa sababu bado yupo anasikiliza tunakupongeza sana kwa kazi nzuri na kwa ushirikiano na wenzako waliopita, na tunaamini na majeshi mengine yatakuwa yanafanya hivyo pia kuzungumza na wale waliopita.

Waheshimiwa Wabunge, la mwisho katika haya yamezungumzwa hapa kuhusu mafunzo yale ambayo Waheshimiwa Wabunge tunakwenda huko pia watumishi wa Bunge. Ni muhimu kila Mbunge kujipangapanga, hasa wale ambao wanamwomba Mwenyezi Mungu kuwarejesha kipindi kijacho wawe wamejipanga vizuri hasa wale ambao wanaogopa kwenda kukata nywele jeshini wawe wanajipanga vizuri.

Waheshimiwa Wabunge, kwa kweli Bunge liko tayari kabisa kuwapeleka kwa ajili ya hayo mafunzo, na tumeona mabadiliko kwa wale ambao walikwenda kwenye hayo mafunzo hawajarudi vile walivyokwenda. Sasa hapa nimetoa mfano wa nywele sio hoja ya nywele pekee mambo mengine mazito mazito wamekuwa wakakamavu zaidi, uzalendo umeongezeka, na pia wanawahi sana Bunge kuonesha kwamba mambo ya muda kule wamefunzwa vizuri na yale makosa madogo madogo ambayo Wabunge wengine tunayafanya humu ndani. Mimi huwa nawatazama wale ambao wameenda JKT yale makosa madogo madogo hawayafanyi yale tunayofanya humu ndani. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, kwa hiyo naamini tukipata fursa Wabunge wengi ya kwenda huko Bunge letu litakuwa na nidhamu

zaidi lakini litakuwa na uzalendo zaidi. Si kwamba sasa hauko upo lakini zaidi zaidi. Kwa hivyo wale ambao wamekwishakwenda hebu wasimame kidogo, wale ambao wameshakwenda eeh, wale ambao wamekwenda kwenye mafunzo. Hata kama ulienda zamani wewe simama tu na wewe. Sasa tusikilizane hawa wamesimama kwa sababu kama walishaenda maana yake hawatarejea tena huko. Kwa hiyo ndiyo nia hiyo, lazima wapewe heshima yao. Sasa sisi ambao hatujakwenda hawa tuwatazame vizuri ili tuwe tunawaulizauliza maswali kwamba kule tukienda tutakutana na nini.

Waheshimiwa Wabunge, kwa kweli tunashirikiana vizuri na JKT na tunaamini wale ambao hamjapata fursa mkileta maombi kwetu tutawapeleka, msiwe na wasiwasi na tunao utayari huo. Vivyo hivyo tunafanya kwa watumishi pia.

Baada ya kusema hayo Waheshimiwa Wabunge naahirisha shughuli za Bunge mkapa kesho saa tatu kamili asubuhi.

*(Saa 7.50 Mchana Bunge liliahirishwa hadi Siku ya Alhamisi, Tarehe 25 Mei, 2023, Saa Tatu Asubuhi)*